

**ULINGANISHAJI WA FANI ZA KIUTENDI KATIKA NYIMBO ZA  
HARUSI MIONGONI MWA JAMII YA WATAVETA NA  
WASWAHLI**

**NA**

**JOSEPH LEDEMI MAKANGE**

**C50/66782/2011**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA  
MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU  
CHA NAIROBI.**

**2015**

## **IKIRARI**

Tasnifu hii ni matokeo ya juhudini zangu za utafiti na si kazi ya mtu mwingine. Kazi hii haijawahi kuwasilishwa kwa mahitaji ya shahada ya uzamili katika chuo kikuu kingine chochote.

### MTAHINIWA

Sahihi..... Tarehe.....  
Joseph Ledemi Makange

Tasnifu hii imeandikwa na kutolewa ili kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

Sahihi..... Tarehe.....  
Prof. Rayya Timammy

Sahihi..... Tarehe.....  
Dkt. Hezron Mogambi

## **TABARUKU**

Kazi hii ninamtabarukia marehemu mamangu mpendwa Haikaeli Lalaseri Machende, kwa juhudini zake za kunilea, kunielimisha, kunifunza haja ya uvumilivu maishani, kunishauri na kuniunga mkono kwa lolote nililoazimia kufanya.

Tabaruku nyingine ni kwa mke wangu Chanza Ledemi na watoto wetu Mshighati, Nabhwari, Masila, Meshack na Harrison. Familia yangu iliniunga mkono kwa hali na mali wakati wa kipindi kigumu nilipokuwa nikiendelea na masomo yangu, nawatachia kheri na baraka za Mwenyezi Mungu.

## **SHUKRANI**

Kwanza natoa shukrani kwa Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na siha njema. Pili, nawashukuru wazazi wangu marehenu Haikeli Lalaseri Machende na Petro Makange Ledemi kwa msaada wao wa hali na mali ili kuhakikisha ya kuwa ninapata elimi.

Tatu, shukurani za dhati natoa kwa familia yangu, mke wangu Chanza Ledemi na watoto wetu Mshighati, Nabhwari, Masila, Meshack na Harrison kwa uvumilivu wao na kunihimiza hasa wakati mambo yalipokuwa yananiendea segemnege.

Nne, shukrani jazila ziwafikie wasimamizi wangu Prof. Rayya Timammy na Dkt. Hezron Mogambi. Hawakuchoka kuisoma kazi yangu mara kwa mara. Mungu awape kila la kheri na mafanikio zaidi katika kazi zenu.

Tano, nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipopeleka shukrani zangu kwa walimu wangu walionifunza: Dkt. Iribi Mwangi, Dkt. Jefwa Mweri, Prof. John Habwe, Dkt. Swaleh Amir, Bw. Basilio Mung'ania ,Dkt. Evans Mbuthia, Dkt. Zaja Omboga na Prof. Kineene Wa Mutiso. Nawashukuru kwa kuninoa mpaka nikanoleka.

## **IKISIRI**

Nafasi ya fani za kiutendi katika nyimbo za harusi mionganoni mwa jamii ya Waswahili na Wataveta ni utafiti wenyewe gharadhi ya kuonyesha jinsi fani za kiutendi zinavyotumiwa katika nyimbo zinazoimbwa wakati wa harusi.Tulichokusudia kufanya katika utafiti wetu ni kulinganisha fani za kiutendi katika nyimbo za harusi mionganoni mwa jamii ya Wataveta na ile ya Waswahili.Malengo ambayo tulikusudia kuangazia ni kubainisha aina mbali mbali za fani za kiutendi,kuonyesha umuhimu wa fani za kiutendi, kubainisha kuwepo au kutokuwepo kwa fani za kiutendi katika nyimbo za harusi na kuonyesha nyimbo mbalimbali zinazoimbwa katika sherehe za harusi mionganoni mwa jamii ya Waswahili na Wataveta.Dira iliyotuongoza kuangazia mada yetu ni nadharia ya Sosholojia ya Utendaji iliyoasisiwa na Bronislaw Malinowski kutoka Uhlanzi na Radcliffe-Brown kutoka Uingereza.Vile vile tulitumia mtazamo wa viziada lugha wa Okpewho (1992) katika kuelezea fani za kiutendi katika nyimbo za harusi mionganoni mwa jamii ya Waswahili na Wataveta.Katika utafiti wetu tuliongozwa na nadharia tete mbili.Kwanza, tulitaka kubainisha ya kwamba fani za kiutendi ni za aina mbalimbali katika jamii ya Wataveta na ile ya Waswahili.Pili, tulitaka kudhibitisha ya kwamba fani za kiutendi katika nyimbo za harusi zina uhusiano mionganoni mwa jamii ya Wataveta na ile ya Waswahili.Mbinu ya utafiti iliyotumiwa ni ile ya sampuli lengwa.Tuliweza kutembelea maktabani na kusoma baadhi ya tasnifu zilizoandikwa.Ushauri wa wahadhiri wetu ulitufaa sana kwani ulikuwa mhimili mkuu wa kazi hii.Utafiti wetu ulimalizikia nyanjani ambapo tuliwahoji watu kumi wenyewe umri kati ya miaka thelathini hadi themanini(30-80) kutoka katika jamii ya Wataveta na ile ya Waswahili.Tulihudhuria harusi tatu kutoka katika jamii hizi na tukachagua nyimbo tano (5) kutoka kila jamii.Utafiti huu umedhihirisha kuwepo kwa uhusiano katika fani za kiutendi katika nyimbo za harusi mionganoni mwa jamii hizi mbili kama vile: minenguo ya mwili,kiitikio,kunyamaza kimya na ishara za uso.Utafiti huu pia umebaini ya kuwa kuna fani za kiutendi katika nyimbo za harusi mionganoni mwa jamii hizi mbili ambazo hazina uhusiano, kama vile: maleba na matumizi ya vidole na mikono.

## YALIYOMO

IKIRARI .....	ii
TABARUKU .....	iii
SHUKRANI.....	iv
IKISIRI .....	v
<b>SURA YA KWANZA .....</b>	<b>1</b>
1.0 Utangulizi.....	1
1.1.0 Tatizo la Utafiti .....	7
1.2.0 Malengo ya Utafiti .....	8
1.3.0 Sababu za Kuchagua Mada ya Utafiti.....	8
1.4.0 Nadharia Tete.....	10
1.5.0 Upeo na Mipaka.....	10
1.6.0. Misingi ya Nadharia.....	11
1.6.1 Misingi na Mihimili ya Nadharia ya Utendaji .....	11
1.7.0 Yaliyoandikwa Kuhusu Somo la Utafiti .....	17
1.7.1 Wanaozungumzia Nyimbo Kijumla .....	17
1.7.2. Yaliyoandikwa Kuhusu Nyimbo za Aina Maalum .....	18
1.7.3 Yaliyoandikwa Kuhusu Utendaji Au Fani za Kiutendaji .....	20
1.8.0 Njia za Utafiti.....	21
1.8.1 Uchanganuzi wa Data .....	23
<b>SURA YA PILI.....</b>	<b>24</b>
<b>UTARATIBU WA KUOA NA NYIMBO ZINAZOHUSIKA NA UTARATIBU HUO MIONGONI MWA JAMII YA WATAVETA.....</b>	<b>24</b>
2.0 Utangulizi .....	24
2.1.0. Taratibu za Kuoa Katika Jamii ya Wataveta.....	24
2.1.1. Maana Ya Harusi / <i>Ngasu</i> .....	25
2.1.2. Dhana ya Ndoa / Kupenda/Kuobhoa / <i>Lukundo</i> .....	26
2.1.3. Utaratibu wa Kulipa Mahari / <i>Ngosa</i> .....	26
2.2.0. Urafiki / <i>Bhumbuye</i> / <i>Kurera</i> .....	27
2.2.1. <i>Mawa ma Kukonya</i> / Sherehe ya Kukonyeza .....	28
2.2.2. <i>Kuomba Moto</i> / <i>Uposo</i> .....	28
2.2.3. Sherehe ya Kutahiriwa / <i>Ngasu ya Kitabhani</i> / <i>Kuingija Mmbora Kingasu</i> .....	30

2.2.4. <i>Ngasu ya Ludabhano/Mafunzo ya Makungwi</i> .....	31
2.2.5. <i>Ngasu ya Kutaha Mawa / Kumtambulisha Mvulana</i> .....	31
2.2.6. <i>Maria / Hatua Zinazofuatwa Kabla ya Harusi</i> .....	32
2.3.0. <i>Kuitangija / Kuwakaribisha Wazazi wa Msichana Kuona Mji Anakokaa Mvulana</i> .....	32
2.3.1. <i>Kuaika Mwai / Kuomba Kumweka Mwana Mwali Ndani</i> .....	34
2.3.2 <i>Kuaika / Kumweka Mwanamwali Ndani</i> .....	34
2.3.3. <i>Kutika Ngunga / Kupeleka Vazi</i> .....	38
2.3.4. <i>Kudidingishwa/ Kumpeleka Bibi Harusi Nyumbani kwa Mume</i> .....	38
2.3.5 Hitimisho.....	48
<b>SURA YA TATU.....</b>	<b>50</b>
<b>TARATIBU ZA KUOA NA NYIMBO ZINAZOHUSIKA KATIKA UTARATIBU WA KUOA KATIKA JAMII YA WASWAHILI.....50</b>	
3.0 Utangulizi .....	50
3.1.0. Taratibu za Kuoa Katika Jamii ya Waswahili .....	50
3.1.1. Maana ya Harusi.....	50
3.1.2. Umri wa Kuoa Na Muda wa Maandalizi ya Harusi .....	51
3.1.3. Kuchagua Mchumba .....	51
3.1.4. Utaratibu wa Kulipa Mahari.....	53
3.1.5. Kuchumbia .....	54
3.1.6. Uposo .....	55
3.1.7. Kupeleka Begi .....	56
3.1.8. Kufuga Ukuti.....	58
3.1.9. Kueka Goma au Kutia Utি .....	58
3.2.0. Nikaha ya Siri / Kuozwa kwa Siri .....	60
3.2.1. Nikaha ya Dhahiri / Kuozwa Dhahiri.....	60
3.2.2. Gwaride .....	61
3.2.3 Limatul - Harus (Chakula cha Mchana).....	61
3.2.4 Fungate ya Harusi na Kuosha Moo .....	62
3.3.0 Hitimisho.....	62

<b>SURA YA NNE .....</b>	<b>64</b>
<b>ULINGANISHAJI WA FANI ZA KIUTENDI KATIKA NYIMBO ZA HARUSI</b>	
<b>MIONGONI MWA JAMII YA WASWAHILI NA WATAVETA .....</b>	<b>64</b>
4.0 Utangulizi .....	64
4.1.0 Utendaji .....	64
4.1.2 Kunyamaza Kimya .....	75
4.1.3 Kiitikio .....	77
4.1.4. Ishara za Mikono na Vidole .....	79
4.1.5. Minenguo ya Mwili.....	82
4.1.6 Maleba.....	85
4.1.7 Vigelegele.....	87
4.2.0. Hitimisho.....	89
<b>SURA YA TANO .....</b>	<b>90</b>
<b>MUHTASARI WA UTAFITI, CHANGAMOTO NA MAPENDEKEZO .....</b>	<b>90</b>
5.0 Utangulizi .....	90
5.1.0 Muhtasari wa Utafiti .....	90
5.1.1. Changamoto Tulizokumbana Nazo Katika Utafiti Wetu .....	91
5.1.2 Mapendekezo .....	92
<b>MAREJELEO .....</b>	<b>93</b>
<b>VIAMBATANISHO .....</b>	<b>99</b>
(i) Nyimbo za Harusi za Wataveta .....	99
(ii) Nyimbo za Waswahili .....	114
(iii) Picha za Harusi za Jamii ya Wataveta.....	122
(iv) Picha za harusi za Jamii ya Waswahili.....	127
v) Orodha ya Majina ya Waliohojiwa.....	133

## SURA YA KWANZA

### 1.0 Utangulizi

Utafiti huu unashughulikia ulinganishaji wa fani za kiutendi katika nyimbo za harusi miongoni mwa jamii ya Wataveta wanaoishi katika kaunti ndogo ya Taveta katika kaunti ya Taita/Taveta na zile za Waswahili wanaoishi katika eneo la Baghani, Kuze na Mkanyageni katika Kaunti ya Mombasa.Katika kutekeleza malengo ya utafiti, kazi hii inatoa maelezo ya kijumla kuhusu historia fupi ya jamii ya Wataveta kisha kuelezea ile ya Waswahili.

Kulingana na wazee wa kitaveta waliohojiwa na mtafiti, Wataveta wanasemekana walitoka katika sehemu ya milima ya Taita.Wanadai ya kwamba hii ndiyo sehemu ambayo walitawanyika baada ya kutoka Shungwaya ambako ndiko chimbuko la Wabantu.Taveta ni mahali ambapo wenyeji wa sehemu hii huitwa Wataveta na hili ndilo jina ambalo husimamia wingi wa kabila hili ambalo ndio wenyeji.Kuambatana na utafiti uliofanywa na Momanyi (2015:17) anasema ya kwamba:

Wataveta ni kundi mojawapo la kibantu, kwa hivyo Kitaveta ni mojawapo ya lugha za kibantu. Tunapozungumzia kundi kubwa la jamii ya kibantu, hatuna budi pia kuelezea kule kundi hili lililokotoka na msambao wake katika janibu mbalimbali za Afrika.Kitaveta kilitokana hasa na kundi la kibantu linaloitwa Niger-Congo(Niger-Kordofanian). Hili ni kundi kubwa miongoni mwa makundi ya jamii za Kiafrika.Kitanzu kimojawapo cha kundi hili ni Shambala.Kitanzu hiki kinatokana na kikundi-mame finyu cha Bantu (Central-Narrow Bantu), kinachojumuisha ukanda wa Iringa-Lamu.

Isitoshe kulingana na wazee wa Kitaveta waliohojiwa wanadai ya kwamba Wataveta ni jamii ndogo sana ambayo haitambuliwi sana na Wakenya wengi.Ijapokuwa kuna baadhi ya watu wanaojumuisha Wataveta na Wataita kama jamii moja.Ukweli ni kwamba hizi ni jamii mbili tofauti zenyelugha na desturi tofauti.Mtazamo huu uliweza kutokea pengine kwa sababu makabila haya yanapatikana katika wilaya moja ya Taita/Taveta na Wataita ni wengi kuliko Wataveta na walijaaliwa kupata elimu ya watu wa Magharibi mapema kuliko Wataveta.Isitoshe, jamii ya Wataveta haikuweza kujulikana sana kama makabila mengine nchini Kenya kwa sababu ni wataalamu wachache mno ambao wameandika kuhusu historia yao,utamaduni wao,fasihi na chimbuko lao.Hali ambayo imechangiwa na ukosefu wa wataalamu wengi kujitokeza

kuandika habari kuhusu jamii hii.Hata hivyo,idadi ya Wataveta asilia ni ndogo mno. Kulingana na sensa iliyofanywa mwaka 2009, idadi ya Wataveta asilia ilikuwa 26,715. Hivyo basi kuwa mionganoni mwa makabila ya Kenya ambayo yako hatarini kuangamia. Hii inatokana na sababu kwamba hamna vitabu vingi vilivyoandikwa kuihusu jamii hii na vile vile vijana wengi hawazungumzi lugha hii. Kulingana na wazee wa Kitaveta waliohojiwa na mtafiti ni kweli kwamba kabilia la Wataveta lipo na ni mionganoni mwa makabila ya Kenya kwani lina utamaduni wao likiwa na fasihi na historia yao.

Kwa mujibu wa wazee wa Kitaveta waliohojiwa,kuna makabila mengine ambayo huishi Taveta.Hii inamaanisha ya kwamba kuna idadi kubwa ya watu wenyewe asili mbalimbali wanaoishi mionganoni mwa jamii hii kwani sensa ya mwaka 2009 ilionyesha ya kwamba kuna zaidi ya watu 50,000 wanaoishi Taveta. Kwa mfano kuna Wadigo wanaoishi katika kitongoji cha Bura-Ndogo na sehemu ya njini, Wakamba wanaopatikana kwa wingi katika maeneo ya Challa na Njukini, Wapare katika sehemu za Madarasani, Mata na Eldoro nao Wataita wanapatikana takriban katika maeneo yote ambayo Wataveta wanapoishi,kuna pia Wachagga na Wamaasai.

Wataveta wanaishi maeneo kati ya mbuga ya wanyama ya Tsavo Magharibi na mpaka wa Kenya naTanzania,karibu na nyanda za chini za mlima wa Kilimanjaro upande wa kaskazini.Jamii zilizo jirani na Wataveta ni Wataita walio upande wa mashariki mwa Taveta,Wapare na Wagwenyo waishio kusini mwa Taveta, Wachaga na Wamasai waishio kaskazini magharibi. Wataveta wana koo mbalimbali. Kwa mfano *Bhamnene*, *Bharuttu*, *Bhamare*, *Bhazirai*, *Bhandighiri na Bhasuya*, wote wakiishi katika maeneo yanayokaribiana.Ikumbukwe ya kwamba kulikuwa na mfumo wa kiutawala ambao uliongozwa na misingi ya Rika au *Irika*. Kila *Irika* lilikuwa na kiongozi wao ambaye alijulikana kama *Mfumwa* au Chifu. Kulingana na wahojijiwa, *Irika* la mwanzo kabisa lilikuwa ni lile la Maitoto ambalo kiongozi wake hakuweza kukumbukwa hata mwaka aliotawala haujulikani na wahojijiwa. Hata hivyo,baadhi ya wazee waliohojiwa waliweza kukumbuka marika kwa mfano: Meriati likiongozwa na *Mfumwa* au Chifu Bharisanga,*Seuri* likiongozwa na *Mfumwa* Tilikia Simba, *Lutareto* likiongozwa na *Mfumwa* Lesareyo Warisanga,*Lukitati* likiongozwa na *Mfumwa* Nathaniel Mbelle nalo *Lukalikali* likiongozwa na *Mfumwa* Richard Kimbwarata ambaye alitawala kipindi cha ukoloni na baada ya kupata Uhuru.Baada ya kupata Uhuru kulichaguliwa *wafumwa* au Chifu wawili, Richard Kimbwarata akiongoza kanda ya Kimorigo naye

*mfumwa* Ramadhani Leshamta akiongoza kanda ya Challa. Kwa mujibu wa afisa mtendaji katika kaunti ndogo ya Taveta aliyeojiwa alieleza ya kwamba kwa sababu za kiutawala maeneo haya yamegawanywa katika vijishehemu mbalimbali ili kufanya huduma kuwa karibu zaidi na mwananchi.

Katika shughuli za uzalishaji mali, Wataveta hujishughulisha zaidi na kilimo pamoja na ufugaji wa mbuzi, ng'ombe, kondoo na nyuki. Kulingana na utafiti uliofanywa na Clara Momanyi (2015: 35) anasema ya kwamba:

Udongo wa volkano wenye rutuba, Mto Lumi,  
chemichemi za Njoro na msitu mkubwa katika eneo  
hili vilichangia katika ukulima na ufugaji.

Kufika kwa wamishonari na wakoloni katika mji wa Taveta katika miaka ya 1890 kulibadilisha hali ya kimaisha na kiuchumi miongoni mwa jamii ya Wataveta. Kwa mfano, Taveta ilikuwa kama makutano ya wafanya biashara katika biashara ya pembe za ndovu ama kuelekea Tanganyika au Mombasa. Wataveta walifahamika kumwogopa Chifu Mandara kutoka Uchagani nchini Tanzania ambaye alikuwa na ndoto ya kutaka kuinyakua Taveta na kuitawala misafara ya biashara ya pembe za ndovu ambayo ilikuwa ikipitia katika eneo hili. Hii ndiyo sababu Wataveta katika karne ya kumi na tisa waliwakaribisha wamishonari pamoja na wakoloni ili wawatawale katika eneo lao ili wajikinge na mashambulizi aghalabu kutoka kwa kundi hatari la jamii ya Wamaasai lilojulikana kama Kwavi na kiongozi kutoka Uchagani aliyeitwa Mandara.

Zamani, Wataveta walikuwa wakilima kando kando ya mto Lumi ambapo kitovu chake ni ziwa Challa huku wakiishi na mifugo wao ndani ya nyumba kwa kuhofia kushambuliwa na wizi wa ng'ombe. Katika kilimo, Wataveta hulima mazao ya aina mbalimbali kama vile ndizi, mahindi, mpunga, nyanya na matunda ya aina mbalimbali. Hata hivyo chakula chao cha asili ni ndizi na ugali ambao ultokana na unga wa ndizi ujulikanao kama *bhughai bhwa makafi*.

Wataveta ni baadhi ya makabila ya pwani ambayo yameendelea kudumisha utamaduni wao, ijapokuwa kutokana na maingiliano na makabila mbalimbali wanaotangamana nao na matumizi ya mfumo wa kiutandawazi, imewalazimu

Wataveta kuacha baadhi za tamaduni zao na kuiga zile za magharibi wakidharau tamaduni zao kwa kuziona kuwa duni na kwamba hazifai na ni za kishenzi.

Utaratibu wa kuoa na kuolewa ulikuwa wa kipekee mno katika jamii hii.Kwa mfano, mwanamume hangeweza kuoa mpaka abaleghe.Kwa sababu ya idadi ndogo ya wasichana wa kuoa wakati huo, mzazi wa kiume wa mvulana angeweza kutuma maombi kwa mama ambaye alikuwa ni mjamzito kuomba kwamba atakapojifungua mtoto na awe ni wa jinsia ya kike basi angeolewa na mvulana wa mzee aliyemposa. Shughuli hii ilijulikana kama *kuchunga kilinga* yaani kuvishwa pete.Mtoto anapozaliwa na kwa bahati mbaya awe wa kiume basi mwanamume aliyemposa angeweza kuendelea kusubiri mpaka atakapozaliwa mtoto wa kike.Mwanamume huweza kubadilisha msichana mwingine wa kuchumbia endapo mwanamke wa kwanza hakuonyesha dalili za kupata mtoto wa kike.Hata hivyo mambo haya hayaendelei tena siku hizi kwani idadi ya wasichana imeongezeka na vijana kuwa na haki ya kuweza kujichagulia wachumba.

Mahari katika jamii ya Wataveta huwa ni makubaliano baina ya pande mbili za bwana na bibi harusi.Mahari hutolewa na mwanamume na hukabidhiwa wazazi wa msichana.Kuna zawadi hutolewa ya kipekee kwa wazazi wa msichana ambaye binti yao angepatikana akiwa bikira.Mwanamke hutolewa mahari kama vile chakula, mifugo, pombe na hata nguvu kazi kwa kumjengea baba mkwe nyumba ya kiasili yaani *msonge*.

Katika masuala ya imani, Wataveta wana imani kuhusu Mungu *Izubha* aliye juu kwenye mawingu.Vile vile wana imani kuhusu miungu ambao wanawatambikia.Kuna mungu wa kiume ambaye hukaa upande jua linapochomoza na yule wa kike hukaa mahali ambapo jua hutua.Wataveta waliamini ya kwamba zamani Mungu alifikiwa kwa kupanda ngazi yaani *muukwa* na watu waliweza kwenda huko juu kuongea na Mungu.Mungu alikuwa karibu sana na watu kiasi hata cha kuweza kumlenga na manati.Wamaasai waliweza kuvamia maeneo waliyokuwa wakiishi Wataveta na kuikata ile ngazi na kumfanya Mungu kwenda mbali sana nao.Hata hivyo wale wote waliokata ngazi au *muukwa* waliangamia. Waliamini kuhusu ufufuo wa wafu ambapo mzee aliyefariki muda mrefu mifupa yake hutolewa na kuwekwa katika hori kisha kuhifadhiwa darini huku fuvu la kichwa chake likiwekwa mahali maalum ambapo watu wa ukoo huo huweka mabaki ya jamii zao.Vile vile Wataveta wanaamini

mambo ya kishirikina kama vile uchawi.Idadi kubwa ya Wataveta ni Wakristo ambao ni takriban asilimia 72 ilihali asilimia 10 hivi wako katika dini ya Kiislamu.Nalo baraza la utawala wa kiasili lililoundwa liliitwa *njama*.Lengo hasa la kubuniwa kwa baraza hili ni pamoja na kusuluhisha mizozo ya kiukoo na kimbari,kujadili mambo yaliyohusu ardhi na umilikaji wake pamoja na kutekeleza jukumu la korti ya kiasili.Mamlaka ya asasi hii yalififishwa na serikali ya kikoloni ambayo ilisimamia uteuzi wa *mfumwa* au chifu na kuweka mamlaka yake chini ya utawala wa kikoloni, kama anavyosema Clara Momanyi (2015:47) kwamba:

Ilipofikia mwaka wa 1952 mamlaka ya serikali kuu ya Njama yalififishwa na serikali ya kikoloni na chifu hakuwa tena akiwajibikia Njama kikamilifu kama ilivyokuwa desturi ya mfumwa.Mamlaka ya asasi hii yalizoroteka zaidi wakati serikali ya mkoloni ilipomteua Chifu Nathaniel Mbelle kuwa chifu wa Wataveta.

Katika mwaka wa 1978 serikali kuu ya *njama* ilivunjiliwa mbali na serikali kuu ya Kenya.Hata hivyo Wataveta wamekuwa na njia mbalimbali za kuonyesha na kuelezea hisia zao kwa kila hali zao za kimaisha.Miongoni mwa njia hizi ni kupitia kwa nyimbo. Nyimbo zilitumiwa katika kuombea mvua, kufurahia ushindi katika vita, kupata mavuno mengi, kusherehekea harusi au kupata mtoto na kubembeleza mtoto akilia. Wataveta hutumia fani za kiutendi katika kupidisha ujumbe kwa umma. Baadhi ya ishara hizo ni maleba, ishara-uso, minenguo, vicheko na vigelegele.

Kulingana na wazee wa Kiswahili wa Mombasa waliohojiwa na mtafiti walieleza ya kwamba Kiswahili ni mionganini mwa lugha ambazo chimbuko lake ni la Wabantu. Jamii inayozungumza lugha hii ni Waswahili. Wazee hawa wanakubaliana ya kwamba lugha hii ina maneno ya kukopa kutoka katika lugha mbalimbali. Mionganini mwa lugha hizo ni Kiarabu pengine kwa sababu ya matumizi ya kitabu kitakatifu cha Quran ambacho kiliandikwa kwa lugha ya Kiarabu kwa matumizi ya dini ya Kiislam.Kulingana na Masebo J.A. na Nyangwine N. (2007:23) wanasema

kuhusu suala la mahali hasa ambapo ndiyo chimbuko la lugha ya Kiswahili wataalamu wanahitafiana. Wengine wanadai ya kwamba lugha ya Kiswahili inatokana na Kingozi, lugha ya Kaskazini Mashariki mwa Kenya na wengine wanasema kuwa Kiswahili chimbuko lake ni Kishomvu kilichozungumzwa na watu wa Bagamoyo Mzizima eneo linalojulikana kwa jina la Dar es salaam hadi Kilwa.

Kwa ujumla madai ya wataalamu hawa hayajawahi kuthibitishwa na mtu yeote kwa hoja makini. Mtaalamu aliyewahi kutoa hisia ya kwamba pengine lugha ya Kiswahili ilianzia katika sehemu mbalimbali za upwa wa Afrika Mashariki ni Freeman-Greenville (1970) Katika makala yake ya Medieval for Swahili alidai ya kuwa lugha ya Kiswahili ilianza na kuinukia katika upwa wote wa Afrika Mashariki kama ambavyo baadhi ya maneno na majina ya watawala na maafisa wa serikali yanavyojitokeza katika masimulizi mbalimbali ya Historia ya Pate yanavyoonyesha. Hata hivyo maelezo ya Freeman-Greenville yanaashiria ya kwamba lugha ya Kiswahili haikuanzia sehemu moja maalum. Massamba na Wenzake (1999:52) wanasema,

Watu walioishi katika maeneo mbalimbali katika upwa wa Afrika Mashariki walikuwa wakizungumza lugha zao mbalimbali. Lakini kwa kuwa lugha hizi zote zilikuwa za Kibantu zilikuwa hazitofautiani sana. Sasa basi, katikakuwasiliana wao kwa wao katika masualaya kibiashara wasemaji wa lugha hizo mbalimbali walilazimika kurahisisha lugha zao kwa kiasi fulani ili waweze kuelewana na wenzao. Katika kurahisisha lugha zao hizo katika maeneo mbalimbali kukazuka lugha moja iliyoelewaka kwa watu wote wa eneo hilo.

Hali hii ilitokea katika sehemu yote ya upwa wa Afrika Mashariki kuanzia Kaskazini hadi Kusini. Matokeo yake yakawa ni lugha ambazo baadaye zilikuwa zikijulikana kama lajaja za Kiswahili. Hivi ndivyo ilivyotokea lajaja ya Kibajuni, Kipate sehemu za Pate, Kiamu katika Lamu, Chichifundi, Kimvita katika sehemu za pwani ya Kaskazini mwa Mombasa, Kimakunduchi, Kihadimu, Kitumbatu katika sehemu za Unguja na Pemba. Hilo ndilo likawa chimbuko la lugha ya Kiswahili kama tujuavyo leo. Ukizichunguza kwa makini lajaja hizo za Kiswahili ni dhahiri kuwa ni lugha kamili zinazojitegemea. Vile vile lajaja hizo zinafanana zaidi na lugha nyingine za Kibantu kuliko zinavyofanana na lajaja ya Kiswahili sanifu ambayo ina maneno mengi ya mkopo.

Mapinduzi kule Amerika yalisababisha upanuzi wa biashara ambapo Waamerika walianzisha biashara na watu wa Pwani ya Afrika Mashariki. Waamerika walibadilisha nguo na watumwa pamoja na pembe za ndovu. Waarabu kutoka pwani ya Afrika mashariki na hasa masultani wa Zanzibar ndio waliosimamia biashara hizo za watumwa na pembe za ndovu.

Waswahili wa Mombasa wana kabilo tisa ambazo zilizanzisha asasi zao wenye kiongozwa na Tamim na kamati ya wazee. Kabilo hizi tisa ni pamoja na makabilo yafuatayo; Wa-mvita, Wa-Jomvu (Wa-Junda), Wa-Mtwapa (Wa-Mutwafi), Wa-Kilifi, Wa-Pate, Wa-Shaka, Wa-Faza, Wa-Katwa na Wa-Gunya (Wa-Bajuni). Miji hii tisa au makabilo tisa waliunda uhusiano na makabilo mengine jirani nao kwa mfano: Wa-Giriama, Wa-rabai, Wa-chonyi, Wa-jibana, Wa-ribe, Wa-kauma na Wa-kambe ambao walipojumuishwa na Wa-Digo na Wa-Duruma walijulikana kama Wa-mijikenda. Mji wa kwanza wa Waswahili ulijengwa zaidi ya milenia moja wakati ambao wabantu hasa waafrika walipohamia na kufanya makazi yao katika mwambao wa pwani.

Kulingana na wazee wa Kiswahili waliohojiwa na mtafiti wanakubaliana ya kwamba Waafrika hawa walikuwa wamefikia kuwa na mila, utamaduni na imani mmoja ya dini ya Kiisilamu na hivyo basi kuitwa Waswahili. Kulingana na wazee wa Kiswahili waliohojiwa wanadai ya kwamba Waswahili wa kwanza walijulikana kama Washirazi kwa misingi ya kwamba walikuwa na uhusiano na Waarabu kutoka Shirazi. Kiuchumi Waswahili ni wavuvi wa samaki. Chakula chao kilikuwa ni samaki na wali. Waswahili waliweza kutambuliwa kwa mavazi yao na viatu vya makubadhi vilivyokuwa wazi na kofia na kanzu.

### **1.1.0 Tatizo la Utafiti**

Wasomi mbalimbali wamefanya tafiti kuhusu Fasihi Simulizi ya Kiafrika, mionganini mwao akiwa ni Wamitila (2002) ambaye anasema ya kwamba fasihi simulizi ni mali ya jamii. Anaeleza ya kwamba hakuna mtu ye yote katika jamii ambaye anaweza kudai kwamba fani hii ni yake. Fasihi huwa inapokezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Vizazi hivi ndivyo huhifadhi fasihi ili kupokezwa kwa vizazi vitakavyokuja. Maoni haya yanaturelekeza kufahamu kwamba, nyimbo za harusi kutoka jamii fulani, zilizotofautiana na zile za jamii nyingine. Kwa hivyo, fasihi simulizi huangazia masuala ya jamii nzima lengwa na sio ya mtu au aila fulani pekee. Hata hivyo kuna wale ambao walifanya utafiti katika nyanja mahususi ya fasihi simulizi kama vile Timammy (2002), Beja (2000) na Gitonga (2009). Kazi zao zimetupatia msukumo na mwelekeo mwema wa kutaka kufanya uchunguzi zaidi kuhusu fasihi simulizi ya Kiafrika. Hivyo basi tukaamua kufanya utafiti kuhusu ulinganishi wa fani za kiutendi kati ya nyimbo za harusi mionganini mwa jamii ya Wataveta na ile ya Waswahili ambao unahitaji kufanyiwa uchunguzi.

Tulikusudia kutafiti jinsi fani za kiutendi katika nyimbo za harusi zinavyotumiwa katika kuwasilisha ujumbe miongoni mwa jamii ya Wataveta na ile ya Waswahili. Sababu kuu ya utafiti huu ni kulinganisha jinsi fani za kiutendi kama vile uso ishara, minenguo ya mwili, mikonyezo, vigelegele na ukariri hutumiwa katika kuwasilisha ujumbe kwa hadhira katika nyimbo za harusi miongoni mwa jamii ya Wataveta na ya Waswahili. Utafiti huu ulijikita katika fani za kiutendi katika nyimbo za harusi na tumetumia mtazamo wa viziada lugha ambao ulielezewa na kufafanuliwa na Okpewho (1992). Na vile vile tumetumia nadharia ya Utendaji ya Bronislaw Malinowski katika kuelezea fani za kiutendi katika nyimbo za harusi miongoni mwa jamii ya Wataveta na Waswahili. Katika kazi hii tumekusudia kuziweka bayana fani za kiutendi katika nyimbo za harusi miongoni mwa jamii za Wataveta na za Waswahili. Hiki kikiwa ni kimojawapo cha vipengele ambavyo havijawahi kushughulikiwa kwa kina katika kazi nyingine zilizotangulia.

### **1.2.0 Malengo ya Utafiti**

Lengo kuu la utafiti ni kulinganisha fani za kiutendi katika nyimbo za harusi za jamii ya Wataveta na ya Waswahili; kwa,

- i. Kubainisha aina mbalimbali za fani za kiutendi katika nyimbo za harusi miongoni mwa jamii ya Wataveta na ya Waswahili.
- ii. Kuonyesha umuhimu wa fani za kiutendi katika nyimbo za harusi miongoni mwa jamii ya Wataveta na za Waswahili
- iii. Kubainisha kuwepo au kutokuwepo kwa uhusiano wa fani za kiutendi kati ya nyimbo za harusi za jamii ya Wataveta na za Waswahili.
- iv. Kuonyesha nyimbo mbalimbali zinazotumiwa katika harusi miongoni mwa jamii ya Wataveta na za Waswahili.

### **1.3.0 Sababu za Kuchagua Mada ya Utafiti**

Fasihi simulizi hutumiwa na jamii nyingi za kiafrika kama njia ya kipekee ya kuhifadhi tamaduni zao. Fani zitumiwazo ni pamoja na nyimbo, methali, misemo, ngano, hurafa, ushairi na kadhalika. Fasihi Simulizi yaelekea kupotea miongoni mwa jamii ya Wataveta na ile ya Waswahili kwa sababu ya mwingiliano mkubwa wa jamii hizi na makabila mbalimbali ya humu nchini. Baadhi ya wanajamii hawa huzitazama tamaduni zao kama ni duni na hazifai, hivyo basi kuiga tamaduni za kimagharibi

ambazo huziona kuwa ni bora. Isitoshe, kuingizwa kwa mifumo ya maendeleo ya Kimagharibi na maendeleo ya kiutandawazi imezifanya jamii nyingi kupuuza tamaduni zao, hasa wakiziona kama ni mambo ya kishenzi yaliyopitwa na wakati. Na hii ndiyo sababu ya kuamua kuufanya huu utafiti ili kuihifadhi.

Fani za kiutendi katika nyimbo za harusi hazijashughulikiwa na msomi yejote katika jamii ya Wataveta, kinyume na jamii ya Waswahili ambapo Timammy (2002) ana sura nzima ambayo ameellezea kuhusu fani za kiutendi katika nyimbo za harusi mionganoni mwa jamii ya Waswahili. Hata hivyo ulinganishaji wa fani za kiutendi katika nyimbo za harusi mionganoni mwa jamii ya Waswahili na ile ya Wataveta ni swala ambalo bado halijashughulikiwa. Pengo hili ndilo lililotupelekea kushughulikia swala la fani za kiutendi katika nyimbo za harusi mionganoni mwa jamii ya Wataveta na Waswahili kama mada ya utafiti.

Nyimbo hutumiwa kutekeleza majukumu mbalimbali mionganoni mwa wanajamii yakiwemo kufundisha, kuonya, kuhubiri, kuelekeza na hasa kushawishi. Fauka ya hayo, nyimbo hutumia fani za kiutendi katika kuwasilisha ujumbe. Kama asemavyo Okpewho (1992:42).

Watambaji katika fasihi simulizi huweza kutumia mbinu mbalimbali za masimulizi pamoja na matumizi ya kawaida ya mdomo kuwasilisha maneno, ili kuzingatia uaminifu wa maneno. Kwa hiyo ni muhimu kutathmini umuhimu wa fani za kiutendi ambazo huenda sambamba na nyimbo. Mionganoni mwa hizo ni pamoja na miondoko, ishara za usoni, kitiikio, maleba, vicheko, sauti, milio na kadhalika. Mbinu hizi hutumiwa kwa njia ambayo huendeana sako kwa bako na ujumbe au maneno ya msimulizi(tafsiri yetu)

Uimbaji hausaidii tu katika kupitisha ujumbe bali hata kutimiza lengo la mwimbaji na mtazamaji na pia kufanya shughuli zote za utambaji kufana na kuwa na mguso kwa watazamaji. Hii ndiyo sababu ilinivutia kuchagua mada ya fani za kiutendi katika nyimbo za harusi ili kuendeleza utaratibu huu ambao umetafitiwa kwa kiasi fulani na unahitaji utafiti zaidi mionganoni mwa jamii hizi. Kuna haja yakufanya utafiti zaidi kuhusu fani za kiutendi katika fasihi simulizi. Mulokozi (1996:34) anasema,

bado tunahitaji maandishi mengi Zaidi yanayotokana na utafiti wa uwandani.

Utafiti huu utatusaidia kukusanya data na kuzihifadhi katika maandishi, kwani mambo mengi ya fasihi simulizi bado yamehifadhiwa vichwani mwa watu kama sehemu ya kutunzia kumbukumbu. Utunzaji wa kumbukumbu wa namna hii siyo thabiti. Kwani wakati wowote data hizo huweza kupotea au kusahaulika kutokana na maradhi au hata kifo.Kimsingi, utafiti huu unatoa mwongozo kwa wasomi wengine ambao wangependa kufanya utafiti katika nyanja hii ya fasihi simulizi ya jamii ya Waswahili na ile ya Wataveta katika kuyajaza mapengo yaliyosalia.Isitoshe, nyimbo zilizokusanywa katika jamii ya Wataveta zimetafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili ili ziweze kufaidi jamii zingine na vile vile watafiti wengine waweze kutambua umuhimu wa fani za kiutendi za nyimbo za harusi mionganoni mwa jamii ya Wataveta na ya Waswahili.

#### **1.4.0 Nadharia Tete**

Utafiti huu ulikuwa na nadharia tete zifuatazo,

- i) Kwamba, fani za kiutendi ni za aina mbalimbali katika jamii ya Wataveta na ile ya Waswahili.
- ii) Kwamba, fani za kiutendi zina uhusiano kati ya jamii ya Wataveta na ile ya Waswahili.

#### **1.5.0 Upeo na Mipaka**

Utafiti huu ulihusu ulinganishaji wa fani za kiutendi kati ya nyimbo za harusi za jamii ya Waswahili na Wataveta.Tulikusanya nyimbo tano kutoka kwa kila jamii hizi.Utafiti huu ulijikita katika vijiji vya Kiwalwa, Abori, Mahoo na Mboghoni katika Kaunti ya Taita-Taveta na mitaa ya Baghani, Mkanyageni na Kuze katika Kaunti ya Mombasa. Tulifikia uamuzi wa kuvichagua vijiji na mitaa hii kwa sababu wenyeji wa sehemu hizi bado wanafanya sherehe za harusi wakizingatia tamaduni zao na pia bado wanakumbukumbu za kutosha kuhusu sherehe za harusi za jamii zao. Nyimbo ziliteuliwa kulingana na majukumu yake mionganoni mwa wanajamii.

## **1.6.0. Misingi ya Nadharia**

### **1.6.1 Misingi na Mihimili ya Nadharia ya Utendaji**

Nadharia tunayoitumia katika utafiti wetu ni ile ya Sosholojia ya Bronislaw Malinowski 1884-1952 kutoka Uhlanzi na Radcliffe-Brown (1881-1955) kutoka Uingereza. Hawa walichunguza jamii mbalimbali katika Pasifikasi na waliandika mengi kuhusu jamii hizo. Nadharia ya Sosholojia ilijikita katika masuala ya jamii peke yake. Hii ilitokana baada ya kugundua dosari zilizofanywa hapo kabla. Kwa mfano, dosari za kutoa matamko juu juu na ya kijumla zaidi. Kauli hizo mara nyingi zilitupilia mbali vipengele kadhaa vya maisha kama vile lugha na mienendo mingine; hakika vilitofautisha jamii moja dhidi ya nyingine. Kwao, tofauti zilizokuwepo baina ya jamii moja na nyingine ziliwu na maana zaidi kuliko kufanana kuliko kuwepo. Kwa hiyo wanasholojia waliazimia kuchunguza kila jamii kwa wakati na nafasi yake kwa kurekodi kila kilichopatikana katika jamii husika.

Bronislaw Malinowski (1932) katika utafiti wake alisisitiza ya kwamba ni muhimu kuchunguza mienendo ya kitabia ya wanajamii na uhusiano wao na wanajamii katika ushikamano wa utamaduni wao na kujihusisha katika masuala yote ya jamii. Alisisitiza ya kuwa ni muhimu kuhusisha njanja ya utendaji na utazamaji wakati wa shughuli yoyote ya utendaji mbele ya hadhira. Kupitia kwa kazi zake Malinowski aligundua ya kwamba ndoa za kitamaduni na zile za kidini bila kujali usasa wake ni muhimu katika jamii na huwa ni kigezo muhimu cha kuleta mshikamano katika jamii.

Radcliffe Brown (1957) aliyeishi kati yamiaka 1881-1955 aliamini ya kwamba utamaduni na uzingativu wake hujenga usawa katika jamii na huwa kwamba kila mara huhusisha mtu binafsi katika utamaduni. Kanuni za jamii hutawaliwa na mienendo na tabia na hutawala namna ambavyo kila mmoja wetu anavyojiwasilisha mbele ya mwenzake.

Nadharia ya Sosholojia ni taaluma inayochunguza mfumo wa kijamii, yaani mahusiano ya wanajamii, mfumo wa kiutawala wa kijamii, maendeleo ya kijamii na kadhalika. Baada ya kugundua ya kwamba nadharia ya ubadilikanaji taratibu na ya msambao zina upungufu, ndipo nadharia hii ikaibuka. Nadharia ya kisosholojia ina mihimili mitatu ambayo ni ule wa umahususi na sio umajumui, mkazo katika utendaji na mhimili unaosisitiza dhima ya fasihi simulizi katika jamii.

Wanasosholojia walijikita zaidi katika mhimili wa kiutendaji. Tofauti na ilivyokuwa kwa wanadamaria wa nadharia zilizotangulia ambao hawakuwa na haja ya kufanya utafiti kuhusu utendaji wa fasihi simulizi kwa sababu waliamini kuwa watendaji hawa walikariri tu mambo waliyoyapata kutoka kwa mababu zao siku za nyuma na kwamba wao wenyewe hawakuyaelewa. Pia, waliamini ya kwamba watambaji hawa walikuwa wajinga na washamba kabisa kiasi kwamba hawakuwa na uwezo wa kuongeza ubunifu wowote katika sanaa hizo. Wanasosholojia waliweka msisitizo katika kuchunguza watendaji katika fani mbalimbali za fasihi simulizi. Kutokana na msisitizo wao huu imebainika kuwa fanani wa fasihi simulizi wana ujuzi na ustadi wa kiutendaji katika sanaa husika. Jambo hili limetusogeza mbele kidogo katika kuelewa fani za kiutendaji katika fasihi simulizi. Wanasosholojia walidiriki na kuthubutu kudokeza kuhusu sifa za ndani za kimtindo katika fasihi simulizi ya Kiafrika. Hivyo basi, wanaamini ya kwamba uamilifu wa fasihi simulizi uko hai na haufi na kwamba unababilika kulingana na maendeleo ya jamii husika. Kutokana na mawazo ya wanadamaria hii ni wazi kwamba asili ya fasihi simulizi ya Kiafrika ni ndani ya jamii za Kiafrika zenyewe na si vinginevyo.

Waasisi wa nadharia ya utendaji kama vile Bauman (1992) Schechner (1988) na Foley (1995) wanashikilia kuwa wahakiki sharti wachunguze zaidi ya matini moja na kuhakiki utendaji kuambatana na matini husika. Waasisi hawa wametambua mihimili kadhaa ambayo husaidia katika uhakiki na ufasiri wa utendaji. Kulingana na Bauman (1992) msingi wa nadharia ya utendaji ni uumbaji wa mawasiliano, Bauman anaeleza ya kwamba kuna ubunifu wa kipekee katika utendaji. Kupitia maelezo yake tunabaini kwa kiasi kwamba katika kila muktadha wa nyimbo za harusi katika jamii ya Waswahili na Wataveta kuna utendaji ambao hulenga zaidi jinsi fani za kiutendi zinavyowasilishwa. Kulingana na Fine (1984:65) kuna dhana ya utamaduni katika utendaji. Utamaduni huhusishwa na fani za kiutendi. Hivyo basi utendaji waweza kutofautiana kutoka utamaduni mmoja hadi mwengine.

Nadharia ya utendaji katika fasihi simulizi imesisitizwa na wataalamu kadhaa wakiwemo Njogu na Chimerah (1999:4-5) wanapotoa kauli kuwa:

sauti ni chombo muhimu sana cha fasihi simulizi. Utendaji ni uti wa mgongo wa fasihi simulizi. Licha ya utendaji, hadhira ya fasihi simulizi hushiriki moja kwa moja katika upelekaji mbele wa masimulizi kwa kuuliza, kuelekeza, kuimba, kujibu na kadhalika. Isitoshe msimulizi

aweza kuipa nguvu lugha yake na masimulizi yake kwa kutumia ishara na kubadilisha sauti. Sauti ni chombo muhimu sana cha fasihi simulizi.

Utendaji ndio uti wa mgongo wa fasihi simulizi ya Kiafrika. Utendaji hufanikisha ujumbe wa fani za kiutendi za fasihi simulizi. Utendaji wa kisanii huwezesha mawasiliano baina ya mwasilishaji au msanii au fanani na hadhira. Katika jamii nyingi za kiafrika, utendaji ulijumuisha shughuli za kawaida za kila siku kama vile kuzaliwa kwa mtoto, kupewa jina mtoto na kuoa na kadhalika.

Kulingana na Matti (1997:53) anasema utendaji katika jamii za Kiafrika ulikuwa mojawapo wa kanuni za maisha ya kila siku. Hata hivyo kila utendaji una dhima yake kwa wanajamii. Kulingana na Schechner (1976:4) ambaye alikuwa mionganoni mwa waasisi wa nadharia ya utendaji anashikilia kwamba utendaji wowote ni tukio la aina yoyote ile ambalo linalohusu hadhira pamoja na uigizaji kwa sababu ya mipaka kati ya utendaji na sanaa katika shughuli za kila siku ni ya kidhahania. Wananaadharia wa utendaji wanaamini kwamba utendaji kama kiungo cha fasihi simulizi hutokana na shughuli halisi za kijamii.

Nadharia ya utendaji ni nadharia muhimu katika maswala ya uwezo wa binadamu katika kuwasiliana na haiwezi kueleweka barabara bila kutambua kikamilifu dhima ya fani za kiutendi na mienendo mingine ya tabia za maisha ya binadamu. Utendaji kama tabia ya kijamii inayolindwa na jamii huwa na tathmini ya mara kwa mara na tathmini yenye huwa hasa katika muktadha wa nyimbo za harusi amba o hufanywa na hadhira ili kufanikisha mawasiliano. Nyimbo nyingi za kiafrika huwa ni sanaa ya kiutendaji. Wataalamu kama vile Nandwa na Bukenya (1990), Kipury (1983) na Miruka (1994) wanaelekea kukubaliana kuwa hadhira huitikia utendaji, yaani utendaji huathiri kwa kiwango kikubwa hadhira ya nyimbo. Alembi (2002:35) anashikilia kuwa utendaji huingiliana kiwazi ili kuwasilisha usanii hai na wenye taathira kubwa kwa wahusika. Mtazamo wa viziada lugha wa Okpewho (1992:48) utatumia katika kuelezea viziada lugha. Kwa mfano, ishara za uso, mikono, uchezaji na ishara mbalimbali kama anavyosema Okpewho (1992:48)

Msanii katika fasihi simulizi hutumia mbinu mbadala mbali na mdomo katika kuwasilisha maneno yake. Katika kuzingatia ufaafu wa maneno hata hivyo ni vyema kuchunguza umuhimu au uimara ili tuweze kuzingatia vifaa vinavyoandamana na nyimbo husika. Lengo hapa ni kuweza kubaini mahali tutakapopata habari au tunaweza

kuzithibitisha.Fani za kiutendi katika nyimbo ni sharti zizingatiwe kwani ni muhimu mno katika kupertisha ujumbe.

Mbinu hizi za kiutendi huandamana na msanii na hutambuliwa kama viziada lugha kwa kuwa huandamana bega kwa bega na matini au maneno katika fasihi (Tafsiri yetu)

Mtazamo wa Okpewho (1992) utatufaa kwa sababu viziada lugha au fani za kiutendi huonyesha mambo yanayofanywa na viungo mbalimbali vya mwili wa mwanadamu. Fani hizi ni muhimu sana hasa katika mawasiliano. Hakuna mawasiliano yoyote mwafaka yanayokosa matumizi ya viziada lugha kwani mawasiliano huhitaji ujumlishaji wa ala ongezi ambazo huchuja mawasiliano.Fani za kiutendi ambazo hutawaliwa na mzungumzaji katika nyimbo za harusi mionganoni mwa jamii ya Wataveta na Waswahili ni pamoja na maleba, vigelegele, uso- ishara na minenguo.

Fani za kiutendi hizi hubeba ujumbe kutoka kwa mwimbaji hadi kwa watazamaji. Kulingana na Bukenya et al, (2010:34) wanasema ya kwamba

viziada lugha vinahusiana na matumizi ya lugha,minenguo ya mwili,ishara uso,nyimbo na densi.Vile vile ni mbinu inayofaa katikamatumizi ya sauti na minenguo katika utendaji ili kutoa tafsiri ya na kudumisha taharuki katika utendaji. (Tafsiri yetu)

Kimsingi, matumizi ya viziada lugha husababisha nyimbo zivutie na kuleta uhai kwa watazamaji.Nyimbo mbalimbali za harusi mionganoni mwa jamii ya Wataveta na ile ya Waswahili hutumia viziada lugha kama njia inayowasilisha ujumbe.Kwa mfano, katika jamii ya Wataveta kuna nyimbo ambayo hutumia ishara za vidole katika kumsuta bibi harusi.Aidha, bibi harusi anapokaribia langoni mwa nyumba ya bwana harusi, watu wa pande zote husutana;

**Mwai wenyu ni msisiri sa imuura**

**Ni imura raa**

**Mwai wenyu ni mjiru sa ikaa**

**Ni ikaa raa**

**Mwai wenyu nimsisiri sa sipoku**

**Ni sipoku raa**

**Mwai wenyu ni kiangi**

**Ni kiangi raa.**

## **TAFSIRI**

**Mke wenu ni mwembamba mshale**

**Na ni mshale kweli**

**Mwanamwali wenu ni mweusi kama makaa**

**Ni makaa kweli**

**Mwanamwali wenu ni mwembamba kama sipoku**

**Mwanamwali wenu hatulii**

**Hatulii kweli**

Waimbaji wanapofika katika sehemu ya mshale au spoku huinua vidole vyao virefu juu wakionyesha jinsi bibi harusi alivyomwembamba kwa kukosa kulishwa vizuri nyumbani kwao. Wanapofikia mahali pa kusema ni mtembezi, huinama chini huku wakitingisha sehemu zao za makalio upande wa kulia na kushoto kuonyesha jinsi ambavyo bibi harusi walivyomfahamu kwa kuranda randa ovyo ovyo na wanaume. Viziada lugha kwa mtazamo wa Okpewho (1992) tutakaoutumia katika kueleza viziada lugha kwa mfano; Ishara za uso, mikono, uchezaji na ishara mbalimbali za mwili. Katika kiwango cha viziada lugha mambo yafuatayo yatachunguzwa:

(i) Fani za kiutendi katika nyimbo za harusi ni pamoja na mwenendo wa ishara za uso, mikono au sehemu yoyote ya mwili ikiwa ni njia mojawapo ya kuonyesha mfululizo wa mafanikio na matendo kama yanavyojitokeza katika utendaji.

(ii) Minenguo ya mwili ndio ambao unakaribiana sana na uigizaji wa mtendaji katika masimulizi. Minenguo ya mwili ni njia muhimu ya kuufanya utendaji kuwa katika hali ya juu na ya kuvutia. Baadhi ya minenguo katika utendaji huwa na dhamira mahususi ya kuelezea vitendo katika nyimbo na inaweza kuelezea ujumbe kwa njia ya vitendo hata bila kutumia maneno. Kama anavyosema Okpewho (1992:48).

Umuhimu wa kuhusisha minenguo na uigizaji katika matini ya fasihi simulizi ni mbinu tosha na ya wazi mara nyingi masimulizi ya utendaji maneno yanayofunguliwa ni mbinu ya kijumla ambayo hubuniwa ili kufurahisha masikio na macho.

Leo katika masimulizi ya utendaji maneno hupatiwa maonyesho ya kimsingi na mara nyingi maonyesho haya ndio hutumiwa katika kuonyesha umuhimu wake (tafsiri yetu).

(iii) Mbinu nyingine ya viziada lugha itakayotumiwa ni uso-ishara kama anavyoidhinisha Okpewho (1992:48):

Elementi ya uimara ni muhimu sana kwa sababu ni vyema pawena usawa kati ya nyimbo na maneno katika utendaji wa masimulizi. (tafsiri yetu)

Nyimbo huunga mkono masimulizi ya maneno kwa njia ambayo sio tu kwa kupitisha ujumbe unaokusudiwa pekee lakini pia kufanya utendaji uweze kuvutia.

(iv) Tutazama pia maleba kama vile nguo na vifaa vile vingine ambavyo hutumiwa katika uchezaji.

Viziada lugha hutoa mwongozo wa fani za kiutendi na fani zisizo tendi na hujenga msingi imara wa mwenendo wa lugha ya kawaida kama anavyosema Abercrombie (1968:55);

Tunaongea na ala za matamshi lakini tunawasilisha ujumbe kwa kupitisha viungo vyetu vya mwili..... (tafsiri yetu).

Dhana ya viziada lugha huandamana unyo unyo na lugha ongezi, hujihusisha nayo na huzalisha pamoja nayo mbinu mbalimbali za mawasiliano. Elimu kuhusu mienendo ya viziada lugha ni sehemu ya mafunzo ya mazungumzo ya majibizano. Mtumizi wa mazungumzo ya lugha ya majibizano hawezi kutumia lugha kikamilifu ili kueleweka pasipo matumizi ya elementi za viziada lugha ziweze kutambuliwa.

Kimsingi, mwimbaji katika nyimbo huhitaji kupokea hisia za watazamaji wake mara kwa mara ili kumhakikishia ya kwamba wanamfuata na wanakubaliana na yale ambayo anayotamka na kwamba wako tayari kuendelea kumsikiliza.

Mwimbaji hutambua ya kwamba yuko pamoja na wasikilizaji wake pale ambapo anaona ishara zikitendeka kama vile: ishara za kichwa, miguu na ishara za macho. Fauka ya hayo, mwimbaji pamoja na msikilizaji sharti waweze kutofautisha lengo na matumizi ya jukwaa hususani ni wakati gani ambao washirika wataimba na ni wakati gani ambao mtribu ataimba.

## **1.7.0 Yaliyoandikwa Kuhusu Somo la Utafiti**

### **1.7.1 Wanaozungumzia Nyimbo Kijumla**

Kuna tafiti mbalimbali zilizofanywa na wasomi kuhusu nyimbo za harusi za makabila mbalimbali.Kwa mfano Mbiti (1991) anasema ya kwamba nyimbo, methali, hekaya na hadithi zinapatikana katika jamii nyingi za Kiafrika.Fani hizi huwa zinatokea katika kipindi maalum na huwa na ujumbe unaobainika katika kipindi hicho. Maoni ya Mbiti yalitunufaisha katika utafiti huu kwa sababu yalifafanua kwamba nyimbo hutokea katika kipindi fulani mahususi. Mbiti alijishughulisha na utanze wa methali,hadithi na hekaya tofauti na utafiti huu ambao ulihusu ulinganishaji wa nyimbo za harusi mionganoni mwa jamii za Waswahili na Wataveta.

Mulokozi (1989) anaeleza kuwa nyimbo hutumika kuburudisha watu kwenye sherehe au wakati wa mapumziko, kuonya, kufunza, kuarifu, kunogesha hadithi, kuomboleza, kubembeleza mtoto alale, kuchapua kazi na kutia hamasa vitani.Nyimbo hizi alizweka katika nui kuu nne ambazo ni Tumbuizo, Tukuzo, Chapuo na Tendi au Tenzi. Katika kila nui alitazama muktadha unaofungamana na wimbo huo na nafasi ya maudhui ya nyimbo hizo kwa hadhira.Mulokozi ametoa maelezo ya kijumla kuhusu nyimbo na anatofautiana na utafiti wetu kwa sababu sisi tulijikita katika fani za kiutendi katika nyimbo za Waswahili na Wataveta.

Balisidya (1989), alitafiti kuhusu nyimbo na kusema kuwa ni tungo za kishairi zinazotumia melodia, mahadhi, kongosie, mapigo na muwala. Alitazama kiundani na kugundua kwamba nyimbo zipo katika viwango mbalimbali kama vile bembea, tahlili, tumbuizo, nyimbo za ngoma, miviga, nyimbo za michezo na nyimbo za siasa.Kipengele cha utafiti alichoshughulikia Balisidya kinatofautiana na chetu kwa sababu sisi tulishughulikia fani za kiutendi katika nyimbo za harusi mionganoni mwa jamii za Waswahili na Wataveta ilihali yeye alishughulikia aina mbalimbali za nyimbo.

Senkoro (1987) amechunguza na kuona kuwa chimbuko la nyimbo lilikuwa ni kazi. Wimbo ulimpa mtu ari na nguvu ya kufanya kazi. Wimbo ulikuwa na nguvu za kichawi zilizomfanya mtu asahau uchovu na asijali jasho jingi mwilini wala jua kali angani.Pia wimbo ultumika kuwahamasisha wanajamii kuungana na kufanya kazi kwa pamoja. Senkoro alitoa maelezo kuhusu umuhimu wa nyimbo katika jamii hali

sisi tumejikita katika fani za kiutendi katika nyimbo za harusi miongoni mwa jamii za Wataveta na Waswahili.

Akivaga na Odaga, (1982) wanasema ya kwamba nyimbo na uchezaji ni mambo ambayo yanajulikana sana na watu wengi miongoni mwa jamii za Kiafrika. Karibu shughuli zote za kijamii huandamana na nyimbo na uchezaji. Nyimbo huimbwa wakati wa kazi, vita, sherehe za kuoana na kutahiri vijana, kuo, matambiko, kuzaliwa au kifo, kumpatia mtoto jina, kusifu viongozi na hata mpenzi. Nyimbo na Uchezaji huwa ni viungo muhimu mno katika maisha na fikira za watu. Kupitia kwa nyimbo watu huweza kujisifu, kujifunza, kucheka, kuomboleza, kuliwaza, kuhimiza na hata kupitisha ujumbe wa siri. Wao wameelezea umuhimu wa nyimbo na kuzigawa kulingana na utendaji wa kazi zake katika jamii. Isitoshe, wametoa mifano mbalimbali ya kutoka katika jamii mbalimbali za Kiafrika kama vile: Wagirama, Wamaragoli, Wadawida na Wabukhusu. Hata hivyo, wana mifano miwili ya nyimbo za siasa kutoka katika jamii ya Waswahili lakini hii inatofautiana na utafiti wetu kwa sababu sisi tulijikita katika fani za kiutendi miongoni mwa jamii ya Waswahili na Wataveta. Hata hivyo kazi zao zilitusaidia katika kukusanya na kuziweka nyimbo katika makundi ambayo yanahuksika.

Finnegan (1977) kwenye utafiti alioufanya kuhusu fasihi simulizi katika Afrika amebainisha kuwa nyimbo huimbwa wakati wa kazi mbalimbali kwa mfano; uwindaji, pia nyimbo huimbwa wakati wa sherehe mbalimbali, kama vile harusi. Hivyo basi kutofautiana na utafiti wetu kwa sababu sisi tulijikita katika ulinganishaji wa fani za kiutendi katika nyimbo za harusi miongoni mwa jamii za Waswahili na Wataveta. Hata hivyo tulinufaika sana katika kubainisha nyakati mbalimbali ambazo nyimbo huimbwa.

### **1.7.2. Yaliyoandikwa Kuhusu Nyimbo za Aina Maalum**

Timammy (2002) ameshughulikia nyimbo za harusi na sherehe mbalimbali za ndoa na umuhimu wa ndoa kuanzia wakati wa kuposwa kwa msichana hadi siku ya harusi miongoni mwa jamii ya Waswahili. Maeleo ya Timammy yalitufaa sana kwa sababu yalituwezesha kupata baadhi ya nyimbo za harusi miongoni mwa jamii ya Waswahili na kuelewa taratibu za ndoa katika jamii ya Waswahili na vile vile kupata baadhi ya fani za kiutendi katika nyimbo za harusi miongoni mwa jamii ya Waswahili. Tofauti

na kazi yetu ni kuwa twalinganisha fani za kiutendi zipatikanazo katika nyimbo za harusi za Waswahili na Wataveta.

Kavugha (1977) alichunguza mila na desturi za Wapare na kuona kuwa, katika kabilia la Wapare siku ya harusi ni siku ya shangwe. Ndugu, jamaa na marafiki wa maharusi huja nyumbani kwa bwana harusi kwa shangwe huku wakiimba. Mada ya Kavugha inatofautiana na yetu kwa sababu alijikita zaidi katika tamaduni za kabilia la Wapare na sisi tunashughulikia ulinganishaji wa fani za kiutendi mionganoni mwa jamii ya Wataveta na ile ya Waswahili.

Mwakasaka (1977), naye alifanya utafiti wa nyimbo katika kabilia la Wanyakyusa lililoko nchini Tanzania. Katika utafiti wake aliona ya kwamba sanaa ya kutunga nyimbo inahitaji kipawa maalumu, ujuzi wa kuwasilisha mawazo kiufundi na mawazo makubwa ya picha. Pia anasema kwamba wakati mwingine nyimbo huandamana na vifaa vya kimuziki. Maoni ya Mwakasaka yalitusaidia kubainisha sifa alizonazo mutribu wa nyimbo na mavazi ambayo hutumiwa katika kucheza ngoma za nyimbo za harusi. Tofauti ni kuwa alishughulikia kabilia la Wanyakyusa hali sisi tunashughulikia makabila ya Waswahili na Wataveta.

Sunkuli na Miruka (1990), katika Mulokozi (1996) wameelezea kuhusu nyimbo za jando (nyiso), kuwa kusudi la nyimbo hizi ni kuwaasa wari kuhusu majukumu yao mapya ya utu uzima, kuwadhihaki waoga, kuwaandaa wari kuyakabili maumivu ya kimwili (kama tohara, kutolewa bikira) watakayoyapata, kuuaga utoto na kusisitiza dhima ya kiutu uzima inayowakabili wari. Mada yake ni tofauti na yetu kwa sababu ye ye alishughulikia madhumuni ya nyimbo za nyiso kwa ujumla wake na sisi tunashughulikia fani za kiutendi katika nyimbo za harusi kati ya jamii ya Waswahili na Wataveta.

Mazigwa (1991), ametazama zaidi nyimbo zinazoimbwa katika sherehe kama vile harusi, sherehe za kumtoa mwari katika makabila ya Wazaramo na Waluguru. Nyimbo hizo huchukua maudhui mazito mazito ambayo huonyesha maisha yaliyomo katika jamii, migogoro na matatizo mbali mbali yanayozuka katika jamii. Nyimbo huelimisha, hukosoa na kurekebisha jamii inapokuwa inaelekea kuzama katika dimbwi la upotofu wakati jamii inapokuwa inaelekea kuiacha falsafa yake. Mada ya Mazigwa ilitusaidia katika kuujenga mhimili imara wa kuweza kubainisha baadhi ya

nyimbo zinazoimbwa katika harusi. Kazi yetu inatofautiana na yake kwani zaidi tunaangalia fani za kiutendi katika nyimbo za harusi za jamii hizi mbili.

Ngure (2003), ameelleza kuwa nyimbo za harusi huimbwa wakati wa furaha katika jamii nyingi. Lakini zipo nyimbo pia zinazoimbwa kuelezea masikitiko ya kuondoka kwa binti alikozoea na kwenda asikokujua. Maoni haya yalitufaa sana kwa sababu yanarejelea kigezo cha kubainisha nyimbo zinazotumiwa katika kumwaga binti ambacho pia ni kipengele muhimu mno katika utafiti wetu.

Beja (2002) alifanya utafiti kuhusu tamaduni za Mijikenda ambapo nyimbo hutumika. Alielezea aina mbalimbali za nyimbo zinazohusiana na utaratibu wa matanga na mazishi kama vile kifudu, mwandzele na kadhalika. Vile vile anaelezea ya kwamba nyimbo ni utungo wa fasihi simulizi ambao huwakilisha ujumbe kwa kutumia sauti na matendo ya waimbaji. Utafiti wake unatofautiana na wetu kwa sababu yeye alichunguza nyimbo za mbolezi katika jamii ya Mijikenda ilihali wetu unashughulikia fani za kiutendi katika nyimbo za harusi za jamii za Waswahili na Wataveta. Hata hivyo utafiti wake umenufaisha utafiti wetu kwani ultuelekeza kupanga aina mbalimbali za nyimbo zilizoimbwa wakati wa shughuli za harusi katika jamii za Waswahili na Wataveta.

### **1.7.3 Yaliyoandikwa Kuhusu Utendaji Au Fani za Kiutendaji**

Mubima (1997) anasema ya kwamba masimulizi mengi ya nyimbo za Kiafrika yanaweza kugawika katika makundi mawili. Kuna kundi la masimulizi ya nyimbo ambayo hufanywa kwa kutumia vyombo vya muziki kama vile ngoma, kupuliza pembe na upigaji wa vijiti na kundi la pili hutumia ishara za mwili kama vile uso ishara, minenguo, vicheko na maleba kama ilivyo katika jamii ya Wataveta na Waswahili. Maelezo haya yalitunufaisha sana katika utafiti wetu kwa sababu yameweza kuelezea aina mbalimbali za fani za kiutendi ambazo ndilo swala tunalolishughulikia.

Miruka (1994) Alichunguza mambo mbalimbali ya fasihi simulizi katika kiwango cha matendo na uchanganuzi. Alijadili mambo yanayohusiana na ushairi na akayagawanya katika makundi mbalimbali kisha akaelezea mahusiano yake. Vile vile alizungumzia kuhusu umuhimu, muundo mtindo na utendaji wa mashairi. Yeye alishughulika zaidi na masuala ya mashairi kwa ujumla katika fasihi simulizi. Hivyo

basi kutofautiana na utafiti wetu kwa sababu sisi tulijikita katika fani za kiutendi katika jamii za Waswahili na Wataveta. Hata hivyo kazi yake ilitusaidia kutambua aina mbalimbali za fani za kiutendi.

Nkweru (1998), amezitazama nyimbo za harusi kama kundi mojawapo la nyimbo za sherehe. Kulingana na Nkweru, nyimbo nyingi za harusi zimejaa sana mambo ya mapenzi na ishara mbali mbali zinazowaelekeza wanaharusi kuhusu maisha yao ya pamoja na kupendana. Kuna nyimbo ambazo huimbwa katika tukio la kupokea mahari na zingine katika tukio lenyewe la kufunga ndoa. Maoni ya mtalaamu huyu yamekuwa msingi thabiti wa utafiti wetu hasa tunapochunguza aina mbalimbali za maleba yanayotumiwa katika nyimbo za harusi mionganoni mwa jamii ya Wataveta na Waswahili.

### **1.8.0 Njia za Utafiti**

Mikakati ya utafiti huu ilianza maktabani ambapo tulirejelea makala mbalimbali yalioandikwa kuhusu mada inayotafitiwa. Mbali na makala tulipitia vitabu mbalimbali ili kupata mwongozo wa kushughulikia kazi yenyewe . Wahadhiri wa chuo pia walihusishwa ili kutoa mwongozo wa jinsi utafiti ulivyoshughulikiwa. Isitoshe, ilitubidi kupitia tasnifu mbali mbali ili kupata taswira ya mambo yote ambayo yanahusiana na mada yetu. Utafiti huu ulikamilika baada ya kukusanya data nyanjani.

Nyanjani tuliteua watu wachache ambao walitufaa katika kupata maelezo kuhusu jamii ya Wataveta na vile vile na ile ya Waswahili. Tuliteua na kuwahoji watu kumi (10) kutoka jamii ya Waswahili na kumi (10) kutoka jamii ya Wataveta. Tulichagua makundi mawili ambayo ni ya vijana ambao walitufaa maelezo kuhusu mipango yote ya harusi katika kipindi hiki na kundi la wazee ambao nao pia walitupatia utaratibu wa mipango ya harusi ya wakati wao. Tulichagua watu wenye umri wa miaka thelathini hadi themanini (30-80) Tulikusudia kuchaguwa nyimbo tano (5) kutoka kwa kundi la vijana na nyimbo tano (5) kutoka kwa kundi la wazee. Tulifanya hivyo kwa kundi la vijana kwa makusudi kuwa wamepevuka kiakili na wameshuhudia utaratibu wa sherehe za ndoa mara kadhaa. Kwa hiyo wana ufahamu wa mambo haya. Vijana hawa watatoa maelezo kuhusu mipango yote ya harusi. Tulifikia mwelekeo huu tukizingatia ya kwamba nyimbo za harusi mionganoni mwa jamii ya Wataveta na Waswahili huimbwa na watu wa jinsia mbalimbali na umri tofauti tofauti. Uteuzi wa watribu

ulizingatia weledi wa wahusika katika maswala ya nyimbo za harusi katika jamii husika.

Nyimbo hizi zilichaguliwa kuambatana na umaarufu wake katika harusi za jamii ya Wataveta na Waswahili. Tulifanya uchunguzi wetu kwa kutumia tarakilishi ambazo zilitusaidia kufanya upekuzi kutoka kwa mtandao. Utafiti huu umefanywa katika kaunti ndogo ya Taveta na katika kaunti ya Mombasa. Mombasa imeteuliwa kwa sababu Waswahili wametanda kwingi katika pwani ya Kenya. Hata hivyo tukumbuke ya kwamba kuna Waswahili wa Mombasa, Lamu, Unguja na hata Zanzibar. Hawa wote wana tofauti zao ndio maana nikaamua kuchagua sehemu moja nayo ni Mombasa. Taveta imeteuliwa kwa sababu ndio eneo pekee ambalo wanapatikana Wataveta kwa wingi na vile vile bado wanaendeleza tamaduni zao za kuoza watoto wao. Nilihudhuria sherehe za harusi tatu (3) kutoka jamii ya Waswahili na Wataveta ili kupata kujua namna sherehe za harusi zinavyoendeshwa, kusikia nyimbo zinazoimbwa na kubainisha aina mbalimbali ya fani za kiutendi.

Ushauri kutoka kwa wahadhiri hasa wasimamizi katika utafiti huu umechangia katika ufanisi wa shughuli nzima ya utafiti. Tulifikia mwelekeo huu tukizingatia ya kwamba nyimbo za harusi miongoni mwa jamii ya Wataveta na Waswahili huimbwa na watu wa jinsia mbalimbali na umri tofauti tofauti. Niliteua mtribu mmoja mmoja kutoka katika jamii ya Wataveta na Waswahili. Uteuzi wa watribu ulizingatia weledi wa wahusika katika maswala ya nyimbo za harusi katika jamii husika. Washiriki walitambuliwa kwa kuwadadisi wahusika na vilevile kuwatazama wakiimba. Mbinu ya kuwatazama waimbaji na hata watazamaji kuambatana na mtazamo wa hisia zao kulingana na nyimbo na sherehe yenyewe ilimsaidia mtafiti katika ubainishaji wa nyimbo na fani za kiutendi katika jamii ya Wataveta na Waswahili. Mtafiti alitumia vinasa sauti na kuhifadhi nyimbo ili kuzifanya uchanganuzi baadaye. Vinasa sauti pia vilitumiwa kunasa sauti na nyimbo ili kuzichanganua fani za kiutendi katika nyimbo za harusi miongoni mwa jamii ya Wataveta na ile ya Waswahili. Kimsingi, video ilitumika kubainisha fani za kiutendi kama vile: uso-ishara ,mwendo na maleba.

### **1.8.1 Uchanganuzi wa Data**

Uchanganuzi wa data ulichunguza na kutambua data iliyokusanywa ili kuweza kutumika katika utafiti wetu ili kupata usahihi wa data iliyokusanywa. Mtafiti alizichuja data zilizokusanywa ili kupata data iliyofaa katika utafiti wetu. Uchanganuzi wa data ulihusisha nadharia ya Sosholojia ya utendaji kulingana na Bronislaw Malinowski (1944) na Radcliffe Brown (1952) na vile vile tulitumia mtazamo wa viziada lugha kulingana na mawazo ya Okpewho (2002). Mionganoni mwa nyimbo ambazo tulizozikusanya tulichunguza nyimbo tano pekee kutoka jamii ya Waswahili na tano kutoka kwa jamii ya Wataveta. Nyimbo hizi zilitarajiwaa kubainisha aina mbali mbali za fani za kiutendi na umuhimu wake mionganoni mwa jamii hizi mbili. Tuliangalia fani za kiutendi katika nyimbo za harusi mionganoni mwa jamii ya Wataveta na Waswahili. Utafiti huu ulituwezesha kubainisha viziada lugha vinavyohusishwa na nyimbo za harusi za jamii ya Wataveta na ile ya Waswahili.

### **1.8.2 Hitimisho**

Kimsingi, katika sura hii tumeshughulikia mambo kadhaa kuhusu utafiti wa fani za kiutendi katika nyimbo za harusi mionganoni mwa jamii za Wataveta na Waswahili. Tumelezea historia fupi ya jamii hizi mbili, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, nadharia tete, misingi ya nadharia, yaliyoandikwa kuhusiana na mada ya utafiti, mbinu za utafiti na uchanganuzi wa data.

## **SURA YA PILI**

### **UTARATIBU WA KUOA NA NYIMBO ZINAZOHUSIKA NA UTARATIBU HUO MIONGONI MWA JAMII YA WATAVETA.**

#### **2.0 Utangulizi**

Katika sura ya kwanza, tulishughulikia maswala kuhusu tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, sababu za utafiti, nadharia tete, upeo na mipaka ya utafiti, misingi ya nadharia, mtazamo wa viziada lugha, yaliyoandikwa kuhusu somo la utafiti, njia za utafiti na uchanganuzi wa data. Katika sura ya pili tumejikita katika utaratibu wa kuoa na nyimbo zinazohusika na utaratibu huo miongoni mwa jamii ya Wataveta.

Nyimbo za harusi tulizozichagua katika jamii ya Wataveta kwanza ziliandikwa katika lugha ya Kitaveta kisha tulizitafsiri kwa lugha ya Kiswahili. Sio kila hatua inayotekelawa katika utaratibu mzima wa kuoa katika jamii ya Wataveta huandamana na nyimbo. Kipengele cha kumweka mwanamwali ndani ndicho hasa hutumiwa katika kuanzisha uimbaji wa nyimbo. Hata hivyo nyimbo hizi huimbwa na vijana ambao tayari wamekwishafunga ndoa au watu wazima. Malengo makuu ya matumizi ya nyimbo katika utaratibu wa kuoa ni kupilisha ujumbe wa mafunzo kwa wanajamii na hususan kwa maharusi.Kama anavyosema Nandwa (2010:71),

nyimbo huliwaza fahamu za watendaji na washiriki wale  
wengine na huwapa mwelekeo wa kujitambua na  
kujamini.(tafsiri yetu)

Kwa maana hiyo basi, matumizi ya nyimbo huweza kurudiwa kila mara katika hafla ya sherehe za harusi.

#### **2.1.0. Taratibu za Kuoa Katika Jamii ya Wataveta**

Nyimbo za harusi katika jamii ya Wataveta huimbwa na watu wa jinsia zote lakini waimbaji sharti wawe wamekwisha tahiriwa na vile vile wawe watu ambao wamekwisha oa au watu wazima wenye kumbukumbu za nyimbo hizo. Kwa maana hiyo basi sherehe ya harusi ilikuwa jambo la lazima. Siku hiyo wanawake na wanaume huwa hawatangamani katika uimbaji. Zamani nyimbo za harusi ziliikuwa na watribu wanaume na ndio waliokuwa na ujuzi wa kuzitunga na hata kuziimba ilihali wanawake walishiriki katika upokeaji pekee.Hata hivyo siku hizi mambo

yamebadilika kwani wanawake ndio huimba nyimbo hizi huku wanaume wakiwa watazamaji na washangiliaji tu.

Zamani idadi ya wasichana katika jamii ya Wataveta ilikuwa ndogo ikilinganishwa na idadi ya wavulana waliozaliwa katika kipindi kimoja mahususi. Hali hii ilisababisha wazazi wa wavulana kuanza kuwaombea watoto wao wa kiume uposo wakiwa na umri mdogo. Isitoshe, wakati mwingine maombi haya yalifanywa hata mama akiwa mjamzito. Wavulana waliweza kuozwa wakiwa na umri mdogo sana. Katika mipangilio yote ya sherehe ya kuoa kulikuwa na aina ya vyakula ambavyo vilithaminiwa sana. Sherehe isingeweza kukamilika bila vyakula hivyo kupikwa. Miongoni mwa vyakula hivyo ni ugali uliotokana na ndizi zilizopondwa pondwa na kutoa unga yaani *bhughai bhwa makafi*. Mboga iliyotumiwa na ambayo ilikuwa maarufu sana ilitokana na majani yaliyojulikana kama *lufuriani*.

Kando na ugali huu kuna ndizi hasa aina ya mshale ambayo hupikwa na kutolewa nzima nzima na huliwa na nyama. Shughuli yote hutawaliwa na unywaji wa pombe hasa ile iliyotengenezwa kwa asali yaani *mawa ma nzoke*, pombe iliyotokana na ndizi yaani *nalu*, pombe iliyotengenezwa kwa miwa yaani *njashi*. Mipango yote ya matayarisho ya kuoa huongozwa na wazazi wa mvulana. Hata hivyo kwa sababu watu wengi wamejiunga na Ukristo au Uislamu, pombe haitumiki tena na badala yake watu hutumia kinywaji cha soda. Ni familia chache mno ambazo ungewapata wakitumia pombe katika shughuli za kuoa.

### **2.1.1. Maana Ya Harusi / Ngasu**

Harusi kulingana na jamii ya Wataveta ni sherehe ya kitamaduni ambayo huwaleta watu wa jinsia na tabaka mbalimbali kuwa mahali pamoja. Malengo ya harusi yametanda kwingi kwani hufanyika ili kuadhimisha jambo muhimu katika jamii. Hivyo basi utaratibu wa kuoa husherehekewa na wanajamii wote na huitwa harusi au *ngasu*. Kwa hiyo sherehe mbalimbali au *ngasu* hufanyika wakati vijana wa kiume na kike wanapooana. Kulingana na wazee wa Kitaveta waliohojiwa walieleza ya kwamba mipangilio ya harusi inaweza kuanza hata mama akiwa mjamzito.

### **2.1.2. Dhana ya Ndoa / Kupenda/Kuobhoa / Lukundo**

Wazazi wa mvulana na wale wa msichana ndio hutoa mchango mkubwa sana katika swala la kupenda na kumwoa msichana. Wazazi wa mvulana ndio huwaendea wazazi wa msichana na kuwaomba uposo. Utaratibu wa uposo unapovunjika mvulana huweza kujitafutia mchumba mwenyewe. Hata hivyo anapompata msichana wa kuoa humweleza mzazi wake wa kiume ambaye hutoa maamuzi ya mwisho kuhusiana na uchumba wao.

Upendo wa wana ndoa hawa wawili ulitawaliwa na wazazi wa mvulana ambao huwa na maamuzi yote kuhusu unyumba wao. Mashtaka ya kutolewana baina yao yalitatuliwa na wazazi wao. Mwanamume hangeweza kumpiga au hata kumgombeza mke wake mbele ya babake. Kufanya hivyo kungeleta shida kubwa na mvulana angeweza kupigwa na mzazi wake. Mambo haya yalichangiwa na dhana ya kwamba wazazi ndio walioshughulika na utaratibu wa kumtafuta na kumwoza mwanamke. Kwa hiyo, hawangemruhusu mumewe amnyanyase. Mvulana hakuwa na haki mbele ya wazazi wake kwani alifanya alivyotakiwa na mzazi wake pasipo kubisha. Tangu jadi, ndoa ya Kitaveta ilihuisha sherehe kadha wa kadha. Hata hivyo kanuni hizi zimegeuka na hazitumiki tena kwani wavulana na wasichana wana maamuzi yao wenyewe ya kujichagulia na kuamua wachumba ambao wangeishi nao.

Hali hii imesababishwa na ongezeko la wasichana katika jamii kinyume na ilivyokuwa hapo awali. Vile vile, kupata elimu ya Kimagharibi na hasa vijana kuingiliana wakiwa vyuoni na katika mahali pao pa kazi, kumewapatia fursa ya kuweza kujichagulia wachumba. Isitoshe, mabadiliko ya ulimwengu kuhusu utandawazi yamewafanya watu kuachana na baadhi ya tamaduni zao na kuiga tamaduni za Kimagharibi.

### **2.1.3. Utaratibu wa Kulipa Mahari / Ngosa**

Sehemu kubwa ya mahari katika jamii ya Wataveta huwa ni mali ya baba. Mama wa msichana hupewa sehemu ndogo mno. Wazazi wa mvulana ndio hushughulika zaidi na utaratibu wote wa kulipa mahari. Kulingana na tamaduni za Wataveta ulipaji wa mahari huwa ni swala ambalo halina mwisho kwani ukwe ulifanywa kwa njia ya urafiki *bhumbuye* ambao ulijengwa zaidi katika misingi ya sherehe zilizoandamana na unywaji wa pombe pamoja na ulaji wa vyakula. Mahari huanza kwa ujenzi wa

nyumba ambayo mvulana humjengea mkwewe. Mvulana asipojenga nyumba ukweni hutoa mtamba mmoja wa ng'ombe *au mori mmwe*. Siku hizi watu hutoa pesa ambazo huwa ni makubaliano kati ya familia zote mbili. Baba mkwe hutoa mtamba mmoja endapo hakutimiza matakwa ya vipengele vyote vya malipo ya mahari yaani *mori ya mawa*. Siku msichana huenda kwa mume wake hutangulizwa mtamba mmoja wa ng'ombe ambaye huitwa ng'ombe ya *kubhekia au mori ya kumkosa mghosi*. Vile vile, mvulana hutoa mbuzi watatu ambao huwa ni wa majina.

Mbuzi hawa hukabidhiwa mamake msichana ili waitane *bhakeri*. Siku hiyo mbuzi mmoja huchinjwa na mmoja hupewa ndugu yake msichana wa kiume. Pia kuna ng'ombe wa *bhakitengi* ambaye huchinjwa nyumbani kwa baba mkwe. Siku hiyo bwana harusi huenda nyumbani kwa baba mkwe akiandamana na mtoto wake wa kiume. Jioni hiyo mvulana hurudi nyumbani na mguu wa nyuma wa ng'ombe. Vilevile huwa kuna *mughoma wa fungade*. Baba mkwe hutengeneza pombe ya asali kisha humpelekea babake mvulana ambaye hutoa ng'ombe aina ya mugoma kwa babake msichana. Fauka ya hayo, kuna mbuzi wawili ambao mvulana humpatia babake msichana ili kubadilisha jina ambalo mtoto wa kike alistahili kumwita babake kutoka kwa bhakuo hadi *mkwea*. Pia, kuna ng'ombe wa *mondo* ambaye huchinjwa nyumbani kwa mvulana halafu sehemu nusu ya ng'ombe hupelekwa kwa wazazi wa msichana.

## 2.2.0. Urafiki / Bhumbuye / Kurera

*Bhumbuye* au urafiki ni utaratibu unaozingatiwa wakati wa kuoa msichana akiwa mtoto mdogo au hata wakati mwingine mama akiwa mja mzito. Utaratibu huu unahu mbinu ya kumlea au *kumrera mmbora* akiwa katika umri mdogo mpaka atakapofikia umri wa kwenda kwa mume wake. Mamake mvulana huendeleza urafiki na mamake msichana ambaye ana uja uzito mpaka atakapoifunguwa. Baada ya kujifungua mamake hutembelewa na kina mama kutoka upande wa mvulana. Wanapokaribishwa mamake mvulana huomba kumsalimia mtoto huku akiwa na dhamira ya kutaka kujua jinsia ya mtoto. Anapotambua ya kwamba jinsia ya mtoto ilikuwa ni ya kike basi hufurahi sana na hushangilia kwa vigelegele kwa sababu mtoto wake alikuwa amepata mke. Hata hivyo, anapogundua ya kwamba mtoto ni wa kiume urafiki unaweza kusitishwa au kuendelea mpaka pale mahali ambapo mama

atakajifungua mtoto mwingine au mama huenda kumtafutia mtoto wake msichana katika boma lingine.

Hata hivyo kwa sababu ya mabadiliko ya hali ya kimaisha na mwingiliano wa sera za Kimagharibi utaratibu wa kuoa uliotumiwa zamani hautumiwi tena. Siku hizi mvulana ndiye hutafuta mchumba wake mwenyewe kisha huwafahamisha wazazi wake. Mvulana humtambulisha mchumba kwa wazazi wake kisha huenda vile vile kwa wazazi wa msichana ili nao waweze kumtambua. Wazazi wa mvulana humtuma mzee kwa wazazi wa msichana kupeleka ujumbe wa uposo.

Ujumbe huwa ni kuwafahamisha wazazi wa msichana ya kwamba msichana wao ameposwa na mvulana wa kutoka katika jamii iliyomtuma. Babake msichana hupokea ujumbe huo na kumtaka mzee aliyetumwa kwenda ili akajitayarische kumtembelea akiandamana na wazazi wa mvulana.

### **2.2.1. *Mawa ma Kukonya / Sherehe ya Kukonyeza***

*Mawa ma kukonya* au sherehe ya kukonyeza ni hafla fupi mno inayoandaliwa kwa ajili ya babake msichana. Mzazi wa msichana hushikwa ghafla bila taarifa na mzee ambaye hutumwa na babake mvulana. Wazee hawa wawili huandamana mpaka nyumbani kwa babake mvulana. Hafla hii haihudhuriwi na watu wengi ila watu wa karibu sana na familia ya mvulana na tena sio wote ila huchaguliwa. Baada ya kula na kunywa babake msichana hutaka kujua sababu za mwaliko ambapo hujibiwa ya kwamba walitaka kuomba uposo au *kuomba kitanga*. Ikumbukwe ya kwamba msichana bado hajatahiriwa yaani ni *ngale* na kwamba hamna utaratibu wowote muhimu ambao hufanywa.

### **2.2.2. *Kuomba Moto / Uposo***

Wazazi wa mvulana ndio humchagulia mtoto wao wa kiume mchumba kwa kuwaendea wazazi wa msichana *kuwaomba moto* au uposo. Ikiwa msichana amechuchuka shughuli hii hujulikana kama kuomba moto na endapo msichana atakuwa bado hajachuchuka shughuli hii hujulikana kama *kuomba kitanga*. Kama tulivyotaja hapo awali wakati mwingine uposo hufanywa hata wakati mama akiwa mjamzito. Hata hivyo, mtoto anapozaliwa akiwa mwanamume, wazazi walioomba uposo wangeweza kuendelea kusubiri hadi mama apate mtoto mwingine kwa matumaini ya kwamba angejifungua mtoto wa kike. Ikitokea ya kwamba mtoto

aliyekuwa ameposwa amefariki kabla ya kuolewa wazazi wa mvulana hupeleka madebe mawili ya pombe yaani *mbuta mbiri ja mawa* na vyakula. Hufanywa hivi ili kuwathibitishia wazazi waliofiwa ya kwamba bado uhusiano ungeendelea yaani *kuilikia mondo*. Kusubiri huku kulisababishwa na uhaba wa wasichana na vile vile sifa za kipekee za jamii ya msichana. Hata hivyo, wakati mwengine wazazi wa mvulana huweza kwenda kutafuta uposo mahali pengine yaani *kubigha lumoroghwa*.

Baada tu ya mama kutambua ya kwamba mtoto aliyezaliwa ni wa kike, mamake mvulana akiandamana na wanawake wachache hufunga safari rasmi kwenda kumpongeza mama aliyejifungua. Katika safari hiyo kina mama huchukua zawadi za vyakula kama vile: unga wa ndizi uliojulikana kama *makafi, nzoke* yaani asali, ndizi aina ya mshale, kibuyu cha maziwa, nyama ya ng'ombe, mafuta yaliyochujwa kutokana na maziwa ya ng'ombe yaani *ngorino* na mahindi. Mamake mvulana hubeba pete iliojulikana kama *luse au kilinga* ambayo huitumia kumvisha mtoto huyo mkononi. Utaratibu huu huwa na madhumuni ya kuzuia mvulana mwengine kutofika pale na kuomba uposo. Mvulana anapokuwa mkubwa hujumuika katika shughuli mbalimbali nyumbani kwa kina msichana kama njia mojawapo ya matayarisho ya kumposa mchumba wake.

Mvulana humsaidia baba mkwe katika shughuli mbalimbali kama vile kulisha mifugo na kurina asali. Ujenzi wa nyumba ya aina ya mviringo yaani *mkolosai* ulikuwa mojawapo ya malipo ya mahari na kila mvulana alipaswa kujenga nyumba hiyo ndiyo ingetumiwa na wasichana wa mji huo kulala na ndiyo ambayo mvulana alitakiwa kuuvunja mlango wake siku ambayo angekuja kumweka msichana wake ndani yaani *kumwaika mwai nyumbeni*. Jamaa wa familia hizi mbili hutembeleana katika hali ya kukuza urafiki wao. Hata hivyo, kufikia wakati huu hamna utaratibu ambao hufanywa rasmi kwani mtoto bado alikuwa ni mdogo yaani mwana *bado dumu yoho hena mwanje yaani sinia au hesina kutara mbande hena mabhee* yaani kuhesabu vifaranga kabla mayai hayaanguliwa. Kwa sababu ya kupanda kwa gharama ya kimaisha na mabadiliko ya kiuchumi wavulana wengi hawajengi nyumba ukweni ila hupeleka ng'ombe wa kike ambaye hajazaa yaani moli moja au pesa ambazo huwa sawa na mtamba mmoja wa ng'ombe. Utaratibu rasmi wa uposo huanza pale ambapo msichana anapoanza kuota matiti yaani *kudung 'usha mabhee*.

Utaratibu uliotumiwa hapo awali wa kuomba uposo umebadilika. Wazazi wa mvulana huwatembelea wazazi wa msichana kwa siku ambayo hupangwa na wote. Siku hiyo kina mama hubeba zawadi kama vile: sukari, unga wa ngano na mahindi, ndizi, maharagwe, mchele na kadhalika. Mbali na zawadi hizi huwa na kapu la mama ambalo zawadi zake lazima ziletwe kama watavyokubaliana kwani hukaguliwa siku ile ya sherehe. Miongoni mwa zawadi ambazo ni za lazima ni pamoja na blanketi mbili, moja la mama na lingine la baba, debe moja la unga wa ndizi yaani *mchu wa makafi, mahemba* yaani mahindi, *madio* yaani ndizi, *Iseto la kingasu* yaani vazi la harusi na la *kibhanyumba* yaani leso mbili.

Vile vile hubeba kesi mbili au nne za soda ambazo huwa ni za kuelezea ujumbe au *kiteto*. Mzee aliyetumwa hapo awali hukaribishwa na kuombwa kujieleza lengo la kuitembelea familia ile. Mzee anaposimama huwafahamisha wote waliohuduria ya kwamba alikuja kuomba moto au kuomba uposo. Mvulana huwaonyesha wazazi wake msichana aliyemposa katika boma hilo. Hata hivyo sio lazima mvulana kuanza kutambulisha lakini pia msichana anaweza kufanya hivyo. Utaratibu huu hutegemea mipangilio ya familia husika. Kimsingi, huwa na mazungumzo mafupi ambayo huwa ni ya kupanga harusi.

### **2.2.3. Sherehe ya Kutahiriwa / *Ngasu ya Kitabhani/ Kuingija Mmbora Kingasu***

Zamani wasichana wa kike waliweza kutahiriwa wakiwa na umri mkubwa hata wengine wakiwa tayari wamebaleghe hasa katika koo za Kiruttu lakini koo za kimmene na Kizirai walitahiri wasichana wao wakiwa na umri mdogo. Gharama zote zilizohusiana na utaratibu wa kumtahiri msichana ziligharimiwa na mvulana aliyemposa. Kwa mfano kujenga kibanda au *iyanda la kitabhani* vazi rasmi la kutahiriwa au *suke ya mmbora ya kingasu*, nachupa iliyojaa samli ya ng'ombe yaani *samuli au ngorino ya kukandia papa*. Mafuta haya yalichanganywa na ndizi iliyopondwa pondwa na waliyatumbia katika kupakia vazi lile lake la kutahiriwa.

Mvulana huchinja ng'ombe na hupeleka mguu wa nyuma wa ng'ombe kwa familia ya msichana ili aweze kutengenezewa supu. Malengo makuu huwa ni kumrudishia msichana afya iliyopungua katika kipindi cha matayarisho na baada ya kutahiriwa. Baada ya kutahiriwa msichana hukaa ndani ya nyumba kwa muda wa mwezi mmoja. Akiwa ndani hujishughulisha na utunzaji wa nywele zake za kichwani yaani *anasigha nyui kwa kutumia isiji na mafuta*. Nywele hizi hukatwa au *huenjwa* siku ambayo

hutoka nje baada ya kupona. Siku hiyo vazi alilokuwa akilitunza kwa kulipaka mafuta na ambalo alilitumia katika kujistiri hulitoa na kumpatia mamake. Vijana walilazimika kutahiriwa kwa sababu kulikuwa na dhana kuwa msichana asipotahiriwa atakufa na asingeweza kuolewa. Aliweza kudharauliwa kwa kupewa majina kama mjinga au *lulturwai*.

#### **2.2.4. *Ngasu ya Ludabhano/Mafunzo ya Makungwi***

Sherehe hii huandaliwa na mamake msichana. Huwa ni sherehe ya kumpa mtoto wake wa kike mawaidha ya kukabiliana na maisha katika ndoa. Mamake msichana huvuna ndizi na kutengeneza pombe ambayo hutumiwa na makungwi. Msichana hupewa mafunzo ya utu uzima hususan jinsi ambavyo angeweza kuishi na kumtunza mume wake,wazazi wa mume,na jamii nzima ya mume.Shughuli hii hufanyika mahali maalum kwenye kibanda yaani *ngondi*. Taarifa kwamba msichana amevunja ungo humfikia mama mzazi kupitia kwa nyanyake msichana, shangaziye, mke mwenza wa mama au wifi ambaye ameolewa katika boma hilo. Msichana anapoipita ngazi hii ya mafunzo ya makungwi huitwa *isiri* yaani anafaa kuolewa. Siku hizi wasichana hupewa mafunzo na wazazi na wachungaji wao ama makanisani au misikitini.

#### **2.2.5. *Ngasu ya Kutaha Mawa / Kumtambulisha Mvulana***

Mvulana hutengeneza pombe ambayo hupelekwa kwa msichana. Wazazi wa mvulana huandamana na baadhi ya watu wa familia yao kwenda kwa wazazi wa msichana. Siku hiyo msichana huwekwa ndani ya nyumba na hutolewa nje wakati wa shughuli ya kujitambulisha. Msichana hutolewa nje na msimamizi wake yaani *mkara*. Msichana akitoka nje huchukua kijiko cha kienyeji yaani *ngwaru* kisha huchota pombe ambayo huwa ndani ya chungu na kumpa mchumba wake. Hii ni ishara kwamba binti huyo amekubali kijana amwoe. Siku kama hii huwa muhimu sana kwa sababu msichana akikataa kuteka pombe na kumpa mchumba wake,basi hakuna sherehe yoyote ya ngasu itakayofanyika. Hii ni dalili kwamba msichana amemkataa mvulana huyo. Baada ya zoezi hili hufanya hivyo na kumpelekea babake mzazi huku akiongozwa na msimamizi wake. Anapompatia babake pombe humwambia ya kwamba *papa uu niye mmbwange wangu namkunda* yaani baba huyu ndiye mchumba wangu ambaye nimempenda.

Baba anapoipokea pombe hiyo hupiga funda moja kisha humuuliza msichana wake *mwanangu iki nikala kijo ngwa kari unenitahisha?* yaani nikila chakula hiki utakuja kumkataa kijana huyu? Msichana hujibu hapana baba, kula bila woga. Kisha humwendea babake mdogo na taratibu kama zile za mwanzo hurudiwa. Baadaye humwendea babake mvulana na anapoipokea huwa ni dhihirisho la kwamba msichana amempenda kijana wake. Babake mvulana husema *asante mama*. Kisha humpelekea mamake mzazi na mamake mdogo. Utaratibu kama ule uliofuatwa wakati baba akikabidhiwa pombe hufuatwa. Shughuli za siku hiyo hukamilika baada tu ya msichana kumtambulisha mchumba wake. Wazazi wa mvulana huleta *mbuta nne* yaani madebe manne ya pombe ya kienyeji. Madebe hayo manne hutumiwa kama ifuatavyo: madebe mawili hutumiwa kama sehemu ya kuuliza dhamira ya mkao, debe la tatu huwa ni la kuwaruhusu kuondoka na lile la mwisho hutumiwa baada tu ya wageni kuondoka.

#### **2.2.6. *Maria / Hatua Zinazofuatwa Kabla ya Harusi***

Kimsingi huwa kuna *maria manne* au hatua nne ambazo huzingatiwa kabla msichana hajawekwa ndani kudhihirisha mwanzo wa matayarisho ya kuolewa. Hatua hizo ni pamoja na kuwakaribisha wazazi wa msichana kuona mji anakotoka mvulana na maombi na majibu ya kumruhusu mvulana kumweka ndani mchumba wake.

#### **2.3.0. *Kuitangija / Kuwakaribisha Wazazi wa Msichana Kuona Mji Anakokaa Mvulana***

Hatua ya kwanza pamoja na ile ya pili au *iria la kubhoka* na *la keri* huwa ni ya kuwaonyesha wazazi wa msichana mahali na jamii ambayo mtoto wao atajiunga nayo. Sherehe hii huwakusanya watu wa familia hizi mbili pamoja na kuweza kujuana. Hatua ya kwanza huwahuusu watu wachache tu ambaa huwa watu wa karibu sana na babake msichana. Hatua ya pili watu wengi hualikwa kwani mtoto katika tamaduni za Wataveta huwa ni wa jamii. Hatua hii huwa na sehemu mbili muhimu ambazo pia sharti zizingatiwe. Sherehe ya kwanza hufanyika nje ya nyumba na baba mkwe hangeingia ndani ya nyumba hata kama kungetokea tatizo la muhimu kiasi gani. Sherehe ya pili hufanyika ili kumwingiza baba mkwe ndani ya nyumba. Katika kutambulisha ya kwamba mvulana alitekeleza wajibu wake wa kumwingiza baba mkwe ndani ya nyumba, baba hubadilisha jinsi ya kuwasiliana na kumwita mtoto wake kutoka *bhakuo* hadi kwa *mukwea*. Baba mkwe hangeweza kuwasiliana na

mkaza mwana wake moja kwa moja. Walisalimiana na kuwasiliana kana kwamba kulikuwa na mtu aliyejkuwa akipitisha ujumbe baina yao wawili. Mara kwa mara ungewasikia wakisema mwambie huyo baba au mama kwamba nimemsalimia. Mkaza mwana hangeweza kuzungumza na baba mkwe uso kwa uso bali alizungumza naye akiangalia chini.

Siku hiyo huwa kuna madebe manne ya pombe inayotengenezwa kwa ndizi yaani *nalu* na debe moja la pombe inayotengenezwa kwa asali yaani *mawa ma nzoke* ambayo huwa katika banda la faragha au *ngilibhata*. Hapa ndipo mahali ambapo mambo kuhusu mahari huzungumziwa. Huwa ni hatua muhimu sana katika jamii kwani huwa ni kipindi ambacho watu hutangaziwa kwamba msichana anafaa kuolewa. Kwa hiyo familia waliruhusiwa kula chochote kutoka kwa familia ya mvulana. Siku hiyo huwa kuna vibanda au *ngondi* tatu. Kimoja cha wanaume na cha pili cha kina mama na cha tatu ni cha kufanya mazungumzo ya faragha au *ngilibhata*.

Ng'ombe huchinjwa ambapo hutolewa vijisehemu au *bhianda* ambapo huwa ni vya muhimu sana katika kila hatua. Sehemu hizi za nyama zinapokosekana au kutolewa vibaya huweza kumlazimu baba mkwe kutoa ng'ombe mwingine. Katika banda la wanaume huwa na vyakula ambavyo ni vya lazima vипатикане. Miongoni mwa vyakula hivyo ni nyama ya ulimi wa ng'ombe yaani *lumi*, Mapafu au *mabhorı* ambayo huliwa na baba mkwe pekee, nyama inayotolewa sehemu ya mgongoni yaani fwai, nyama inayotolewa sehemu ya paja ikiandamana na fupa lake yaani *lorishe na* hutolewa pia sehemu ya nyama ambayo hupatiwa ndugu wa kike wa msichana ambayo hujulikana kama *ibhindi la sakame*. Vyakula ambavyo huliwa siku hiyo huwa ni ndizi za mshale ambazo hazipondwi pondwi, ugali kutokana na unga wa ndizi yaani *makafi* na mboga za majani yaani *lufuriani*. Katika banda la kina mama hutandazwa ngozi ya ng'ombe ambayo huitumia kukalia.

Mamake mvulana hukaa pamoja na kivyere wake na sehemu ya *fwai* ambayo huwa ni sehemu ambayo hupatiwa mamake msichana inapoletwa huikata kwanza kisha humkabidhi mwenzake ambapo naye huwakatia wanawake wale wengine. Kuna sehemu inayompasa ndugu wa kike wa msichana yaani *ibhindi la sakame*. Vyakula huwa ni sahani nne za ugali wa makopa yaani *bhitangu bhinne bhyia bhughai bhwa makafi*, ndizi au madio, na kimanga. Mboga za ugali haziungwi, huwekwa mafuta na chumvi tu na nyama huwa ni utumbo. Ndizi huwa ni za mishale ambazo hazipasuliwi.

Katika banda la tatu, hukusanyika wanaume na wanawake kwa pamoja lakini huwa ni la watu wachache. Vyakula huwa kama vibanda vile vingine.Pombe ya asali debe moja huwa ndio ya kuanzia mazungumzo.Hatua ya tatu huwa ni ya kuomba ruhusa ya kumueka msichana ndani yaani *kuaika mwai*. Baada ya kula na kunywa, wazazi wa msichana humjibu babake mvulana ya kwamba wameyasikia maombi yao lakini hawangeweza kuwajibu kwa wakati huo. Wangeenda kisha wangewajibu siku nyingine ambayo huwa ni hatua ya nne. Utaratibu wa kumwonyesha mkwe mahali anapotoka mvulana bado unazingatiwa hadi hivi sasa.Huwa ni kipindi muhimu mno kwani ndio siku ambayo mahari hujadiliwa na idhini ya kufunga ndoa pia hutolewa katika hatua hii.Hata hivyo ikumbukwe ya kwamba ruhusa ya kufanya harusi haiwezi kutolewa mpaka kiasi fulani cha mahari kilipwe.

### **2.3.1. *Kuaika Mwai / Kuomba Kumweka Mwana Mwali Ndani***

Katika hatua ya tatu au *iria la katatu* huwa ni ya kuomba idhini ili kuruhusiwa kumweka mwanamwali ndani. Utaratibu wa maandalizi haya hulingana na ule wa hatua ya kwanza na ya pili.Baada ya kula na kunywa mzee ambaye ni mshenga huelezwa ya kwamba ombi lake la kumweka mwanamwali ndani lingejibiwa siku nyingine. Hivyo basi huondoka na hujitayarisha kurudi tena katika hatua ya nne. Hatua ya nne au *irika la kanne* hufanyika ili kumpa kijana jibu la kumruhusu kuweza kumweka mchumba wake ndani yaani *kumwaika mwai*. Baada ya kula na kunywa, kijana huambiwa ya kwamba kabla ya kumweka msichana ndani ajenge nyumba ya aina ya mviringo yaani *mkolosai*; nyumba hii ilijengwa kwa kutumia nyasi kuanzia chini hadi juu yaani *madafwa kufuma wanga mpaka sii*. Ndani ya nyumba hii kuna mahali pa kupikia, mahali pa kufugia kuku, mahali pa kulishia ng'ombe, mahali pa kulalia na mahali pa kufugia mbuzi na kondoo. Sehemu ya ng'ombe na ile ya jiko hutengwa kwa kujengwa uzio unaowatenganisha ng'ombe na jiko yaanindarari kiasi kwamba hata ng'ombe wanapolishwa wasiweze kurusha nyasi na kusababisha moto.

### **2.3.2 *Kuaika / Kumweka Mwanamwali Ndani***

Utaratibu wa kuoa huanza rasmi kwa sherehe ya kumweka msichana ndani, shughuli inayojulikana kama *kuaika mwai*. Kipindi cha kumweka mwanamwali ndani hutofautiana na hutegemea na jamii au hususan uwezo na mapato ya jamii husika.Baadhi ya jamii huweza kuwaweka wasichana wao ndani kwa mwaka mmoja na wengine hata miaka miwili. Shughuli ya kumweka mwanamwali ndani hufanywa

usiku. Msichana hufungiwa ndani huku mlango ukiwa umekomelewa kwa magogo. Vijana walioandamana na bwana harusi hung'ang'ana mpaka waweze kufaulu kuuvunja mlango.

Vijana hawa huwa wamejihami kwa fimbo mkononi kama tahadhari kwamba endapo pangetokea vurugu au vita baina ya vijana wa kijiji ambacho msichana hutokea na wale walioandamana na bwana harusi kwamba wangeweza kukabiliana nao vilivyo. Kama tulivyotaja hapo awali wasichana waling'ang'aniwa kwa sababu walikuwa wachache wakilinganishwa na idadi ya wavulana. Wasichana ambaa hukaa ndani wakati mlango unapovunjwa hufanya kila jitihada kuwazuia vijana kutoka upande ule wa bwana harusi kuingia ndani. Wakati mwingine hutokea vurugu hata watu kuweza kutobolewa macho. Harakati hizi hufaa kukamilika kabla ya jogoo la kwanza kuwika kwani awikapo jogoo, shughuli hiyo haingeruhusiwa kuendelea kulingana na tamaduni za jamii hii. Kwa maana hiyo basi vijana wanaposhindwa kuuvunja mlango wa nyumba na babake msichana kugundua kwamba kungeweza kupambazuka kabla mlango haujavunjwa huweza kuwasihhi wasichana wanaomkinga bibi harusi kuwaruhusu vijana kuingia ndani.

Pindi tu vijana wanapofaulu kuingia ndani ya nyumba, dadake mvulana humpaka msichana mafuta. Mafuta haya huwekwa ndani ya chombo maalum kilicho julikana kama *muko* yaani kijiko cha asili. Mafuta yanayotumiwa huwa ni ya ng'ombe yaani *ngorino* na msichana hupakwa katika kipaji chake cha uso huku akiambiwa ya kwamba hata akikaa kwao miaka mingapi atabaki kuwa mke wa ndugu yake. Msichana hulia anapokuwa katika zoezi la kupakwa mafuta. Msichana anapokuwa ndani haruhusiwi kusalimiana au kuwa na mawasiliano na watu wa upande wa bwana harusi isipokuwa tu wale ambaa hawajatahiriwa. Fauka ya hayo, msichana akiwa ndani haruhusiwi kuoga kwa maji bali hujichubua kwa kutumia ndizi yaani *papa* ambayo huwa ni aina fulani ya ndizi iliyojulikana kama *indiji au itendera* iliyopondwa pondwa kwa mafuta ya ng'ombe yaani *ngorino*.

Baada ya zoezi la kumpaka mwanamwali mafuta kukamilika basi vijana walioandamana na bwana harusi huanza kuimba wimbo uitwao *mwerimweri* huku wakielekea nyumbani. Katika safari ya kuelekea nyumbani kwa bwana harusi vijana hawa hufikia mahali wakasimama kisha wakaunda duara wakaimba katika hali ya kusherehekeea. Ifahamike ya kwamba chochote watakachopata katika eneo hilo hata

kama ni mimea hukanyagwa kanyagwa na mwenyewe hangedai chochote. Vijana huwa wamepandwa na hasira yaani *kuilang'a*. Vijana hutoka hapo mbio wakiwa na furaha ya kwamba mwenzao amepata mke. Wakifika nyumbani huwakuta wazee wa kiume na wakike wakiwangojea na hulakiwa kwa wimbo ufuatao:

**MWERIMWEERI**

**Mweri mweeri x2**

**Hiyooo**

**Mwai weetu**

**Hiyoo**

**Twamwaiika**

**Hiyooo**

**Na ng'ombe jeetu**

**Hiyooo**

**Na mbuji jeetu x2**

**Hiyooo**

**Tughambe mweri mweeri**

**Hiyoo**

**Mwai weetu**

**Hiyooo**

**Twamreera**

**Hiyooo**

**Nazinya jeetu**

**Hiyooo**

**Na madio meetu**

**Hiyooo**

**PAMBIO**

**Yehoye hoo x2**

**Iyehoye hoo x2**

**Lanye mweri mweeri**

**Hiyooo**

**Mwai weetu**

**Hiyooo**  
**Twamgera kiaama**  
**Hiyooo**  
**Na mbuji jeetu**  
**Hiyooo**  
**Na zoke jeetu**  
**Hiyooo**

### **TAFSIRI KWA KISWAHILI**

**Msichana wetu**  
**Hiyooo**  
**Bibi harusi wetu**  
**Hiyooo**  
**Tuliyemfunza**  
**Hiyooo**  
**Na ng'ombe wetu**  
**Hiyooo**  
**Na mbuzi wetu**  
**Hiyooo**  
**Tuseme msichana wetu**  
**Hiyoo**  
**Bibi harusi wetu**  
**Hiyooo**  
**Tuliyemlea**  
  
**Hiyooo**  
**Na uwezo wetu**  
**Hiyooo**  
**Na ndizi zetu**  
**Hiyoo**

Ubeti wa kwanza katika wimbo *mwerimweri* huimbwa na wale vijana wa kike na wa kiume walioandamana na bwana harusi wakishangilia kufaulu kwao kumweka bibi harusi ndani. Wanaelezea ya kwamba katika kipindi chote bibi harusi atatunzwa kwa kutumia rasilimali zitokanazo kwa ng'ombe na mbuzi. Katika ubeti wa pili vijana

wanashangilia kumpata bibi harusi ambaye watamtunza akiwa kwao kutokana na bidii zao. Ikumbukwe ya kwamba kabla ya kipindi cha kumweka mwanamwali ndani mvulana alipaswa kusaidia katika kazi mbalimbali nyumbani mwa msichana.Kwa mfano; kurina asali, kujenga nyumba na kulisha mifugo. Mvulana alipaswa kuyafanya hayo yote kama njia mojawapo ya taratibu za kuoa.Katika ubeti wa tatu wasichana kutoka upande mwanamwali anakotoka nao hufurahia ya kwamba bibi harusi alipitia mikononi mwa kungwi kwa kutumia rasilimali zao kama vile mbuzi, asali na pombe.

### **2.3.3. *Kutika Ngunga / Kupeleka Vazi***

Kupeleka vazi au *kutika ngungani* shughuli ambayo hufanywa na vijana pamoja na mamake mvulana nyumbani kwa wazazi wa msichana. Shughuli hii hufanyika siku ya pili baada ya msichana kuwekwa ndani.Kabla ya mamake mvulana hajawasili msichana hujificha porini ili atafutwe. Ikitokea ya kwamba bibi harusi hakupatikana basi watu wa nyumbani kwao humwomba atoe sauti ili waliokuwa wakimtafuta waweze kumwona. Mamake mvulana na wanawake alioandamana nao humlazimisha mwanamwali kuingia ndani ya nyumba baada ya kupatikana alikojificha. Mwanamwali akiwa ameketi mamake mvulana huja na kumbandika nguo mgongoni. Vazi hili hujulikana kama *iseto* na ndilo ambalo huletwa na mamake mvulana.Bibi harusi hulitumia vazi hili katika kujisitri na kujificha uso ili asionekane ovyo na watu amba o hawapaswi kumwona.

### **2.3.4. *Kudidingishwa/ Kumpeleka Bibi Harusi Nyumbani kwa Mume***

Baada ya msichana kuwekwa ndani kwa kipindi ambacho huzingatiwa na uwezo wa familia; usiku wa kuamkia siku ya kwenda kwa bwana harusi wimbo *mala magheri marefika* huimbiwa msichana akiwa na wenzake amba o hukaa chumbani au sebuleni mwa nyumba ambayo huishi. Zamani kulikuwa hamna viti na wasichana waliweza kukalia ngozi ya ng'ombe iliyowambwa au kwenye vitanda viliviyotengenezwa kwa miwale yaani *mabhale* au kukalia kwenye migomba ya ndizi iliyokatwa. Kimsingi, wasichana hawa huimba wimbo wa huzuni ukiwa umejaa ghadhabu wakiwasuta wazazi wa mwanamwali kwa kukubali kupokea posa ya mvulana ambaye hata hawajamchunguza hulka zake. Kwa sababu ya uchungu wa ujumbe uliobebwa katika wimbo huo amba o huwa umejaa vijembe yaani *Kubigha masoma* wazazi wa msichana na hata ndugu zake hukaa mbali na nyumba walimokaa wasichana ili kuepuka kujazwa na jazba.

Babake msichana aliweza kuwaamuru wasichana wanaoimba pamoja na mtoto wake wanyamaze na msichana aende kwake yaani akaolewe ili naye akajijenge. Hata hivyo kwa sababu ya utangamano na makabila mengine na madhara ambayo yaliweza kusababishwa na uimbaji wa wimbo huu siku hizi hauimbwi tena. Asubuhi ya kuamkia siku ya harusi kakake msichana ambaye humfuata katika uzawa ndiye humtoa dadake kwa mume wake yaani *kumdidingsha mwai*. Mvulana anayemtoa au kumkabidhi mwanamwali kwa bwana harusi hupewa mbuzi mmoja jike na mshale mmoja wa upinde ambao una sumu. Ndoa inapovunjika vitu hivi hurudishwa kwa mume.

### **MALA MAGHERI MAREFIKA**

**Mala magheri ee iyo maringana**  
**Kutonga natonga ee iyo kureyoa**  
**Kureyoa wikuji ee too na wikenya**

**Hala wikikua yoo niwotoka**  
**Mama nakushigha mwenye eetoe**  
**Natonga lanye etoe kureyowa**  
**Bhaa mndwetu eetoe natonga**

**Bhaa mndwetu natonga yoo kureyowa**  
**Bhala bharela ng'ombe ngwa**  
**Bhachike kinugu eeh saa ighembe**  
**Ighembe lishonwa yoo**

**Ighembe lishonwa eto ni mshana**  
**Mshana mangeri eetoo arufure**  
**Aachiku kinugu etoo sa ighembe**  
**Mala magheri ee iyo marefika**

**Iya na papa eetoo twaaghana**  
**Iya wangu etoo twaaghana**  
**Ekubaiya lukwi etoo ni ani**

**Iya wangu eto nakushigha**  
**Ekutongia ngondeni eto ni wakweani**  
**Hee iya wangu eto nakushigha**  
**Ekuetie idio etoo ni wakweani**

**Nafika kichini eto kureyowa**  
**Nirepimiwa kijo eto na madio**  
**Hee, nitara etoo bwasi bwangu**  
**Hee, niketeze bhome bwasi bwangu**

**Ekuwura tauni eto papa ni wakweani**  
**Hee natonga kichini eto kureyoa**  
**Reguree ngoo eto ikubhure tauni eto ee**  
**Hee iya wangu eto twaaghana**

**Ekuhaghia iyanda eto niwakweani ee**  
**Nashigha hetu heteka ee hee**  
**Natonga kurekija hengi iya ee hee**  
**Natikwa kichini etoo kureyowa**

**Papa wangu etoo twaaghana**  
**Hee ekukezia etoo ni wakweani**  
**Kana ekubighia kibulu eto ni wakweani**  
**Natikwa kichini etoo kureyowa**

**Eee mala magheri etoo marefika**  
**Hee irika letu etoo twaaghana**  
**Nineseka na ani etoo wasiwi bwangu**  
**Hee natikwa kichini etoo kureyowa**

**Jila ndamwena chetu ee chatera**  
**Nashighwa mkibha etoo bhwasi bhwangu**  
**Mwikae nenzo ee kiboheni**  
**Hee, natikwa kichini etoo kureyowa**

## **TAFSIRI KWA KISWAHILI**

**Ile siku jamani imefika**

**Kwenda naenda jamani kuangalia**

**Kuangalia iliyokomaa na mabichi**

**Ili isiyokomaa niweze kurudi**

**Ndugu zangu nimeenda**

**Ndugu zangu nimeenda leo kutazama**

**Wale waliokula ng'ombe wa watu**

**Wakatike katikati kama mpini wa jembe**

**Siku jamani imefika**

**Mama na baba jamani twaagana**

**Mama yangu jamani twaagana**

**Atakayekuvunjia kuni jamani ni nani**

**Mamangu jamani nakuacha**

**Atakayekwendea shambani jamani ni nani**

**Hee mama yangu jamani nakuacha**

**Atakae kuletea ndizi jamani ni nani**

**Naenda ubayani jamani kutazama**

**Nitapimiwa chakula jamani tabu zangu**

**Hee nitahesabiwa jamani hata na ndizi**

**Hee nifanye nini tabu zangu**

**Atakaye kwambia pole ukitoka kusaga ni nani**

**Hee naenda ubayani jamani kuangalia**

**Ukashike tumbiri akuambie pole jamani**

**Hee, mama yangu jamani twaagana**

**Atakaye kufagilia nyumba ni nani**

**Naacha kwetu kukipotea jamani ee**

**Naenda kujenga kwingine jamani ee hee**

**Napelekwa kubaya jamani kuangalia**

**Baba yangu jamani twaagana**  
**Yule atakayekukusalimia ni nani**  
**Ama atakayekukutengenezea uji ni nani**  
**Hee nimepelekwa ubayani jamani kuangalia**

**Ehee kumbe ile siku jamani imefika**  
**Hee rika letu jamani tunaagana**  
**Nitacheza na nani jamani tabu zangu**  
**Hee nimepelekwa ubayani jamani kutazama**

**Napelekwa ubayani jamani kuangalia**  
**Ille michezo yetu sasa imehairishwa**  
**Nimeachwa masikini jamani tabu zangu**  
**Mkae na amani kwaherini**

Katika ubeti wa kwanza msichana anawalamikia wazazi wake kwa kumtoa kwa mwanamume. Mwanamwali anasema hajazoea *wikuji na wikenya* yaani hajazoea mboo ndefu na hata ile fupi, kwa hiyo anaogopa kwenda kwa huyo mume. Hata hivyo inapotokea ya kwamba mwanamume ana mkia mrefu kupita kawaida yaani *isimo* hupewa kipimo cha kumwingilia mwanamke. Wakati mwingine mkia wa mwanamume hubidi kuvalishwa *kishongo* au kikuba ili anapomwingilia mwanamke asipitishe sehemu inayotakikana. Hata hivyo, wakati mwingine mwanamke hushindwa kuvumilia na hubidi kurudi kwao.

Msichana anawalamikia wazazi wake kwa kupokea zawadi za mvulana hata kabla hawajamfahamu tabia zake. Anasema *warela ng'ombe ngwa wachike kinugu* yaani waliokula mali za watu wakatike viuno. Analalamika kwamba hata akifa mikononi mwa mumewe wazazi wake wasilalamike kwa sababu walimuuzza kwa kula mali ya watu huku wakimtangaza kuwa ni mke wa watu. Anasema *kureyoa wikuji na wikenya* yaani anaenda kuteswa lakini atafanya nini na wazazi wake tayari wameshamuuza kwa mwanamume.

Sherehe ya kumzawadi msichana huongozwa na wazazi wake ambao humshauri ya kwamba vyombo atakavyopewa asivisahau kwani ndivyo atakavyovitumia nyumbani kwa mumewe. Msichana hupewa nasaha na wazazi wake ya kwamba akienda kwa

mumewe amheshimu na watu wote wa jamii ya bwana bila kuwabagua; ampatie bwanake chakula kila anapohitaji, asiwe mchoyo, azingatie kilimo na aendeleze uzao katika familia ya bwana. Baada ya shughuli ya kumzawadi msichana kukamilika watu walioandamana na bwana harusi hurudi na mwanamwali mpaka nyumbani. Jioni hiyo majira ambayo ng'ombe hurudi kutoka malishoni hufanywa utaratibu wa kumtoa mume vitu mwilini. Mwanamume hatolewi viatu vivi hivi tu bali hujaribu kukataa kataa lakini mwishoni humruhusu kumtoa yaani *kumuhamba mmbwange*. Vitu vinavyotolewa huwa ni viatu, kisu, na mkuki alivyokuwa amevaa au ameshikilia. Malengo ya shughuli hii ni kuwafahamisha watu jinsi atakavyopatia mume wake heshima, atakavyomtunza, atakavyokuwa mnyenyeketu mbele ya mume wake na kwamba mume atakuwa kichwa katika nyumba.

Siku hizi, wiki moja au mbili kabla ya harusi, mvulana hupeleka zawadi kama vile debe moja la pombe ya asali kwa wazazi wa msichana ili kupata baraka yaani *kutufiwa mate*. Usiku wa kuamkia siku ya harusi wazazi wa mvulana hupeleka mguu mmoja wa mbele wa dume la ng'ombe na pombe debe mbili. Siku ya kwenda kwa bwana, msichana hupelekwa usiku na vijana wa kiume wa rika lake pamoja na mume wake. Wakati mwingine msichana anaweza kujitia hamnazo kwamba hataenda na akifanya hivyo hupelekwa kwa nguvu.

Jioni hiyo msichana hubebwa mgongoni na ndugu yake wa kiume kuanzia mlangoni huku wakizunguka nyumba yao mara nne. Wanapozunguka huimba wimbo *Mwari Gheenda* huku wakienda mbele na kurudi nyuma. Baada ya mizunguko minne dadake mvulana anayeoa huingia katikati yao na kumnyakua msichana mikononi mwa kakake. Maana ya mizunguko minne huwa ni kielelezo cha kuwa akienda kwa mumewe aketie kiti cha miguu minne yaani ajishughulishe na kujenga familia yake. Hata hivyo msichana huwa hajachilii hivi hivi tu kwani hujaribu kurusha rusha miguu yake yote hewani yaani *kutabhatabha* ili asichukuliwe kwa urahisi.

## **MWARI GHEENDA**

**Heee mwari gheenda**

**Heee mwari hunduuka**

**Heehe waibhaa shaaghi**

**Heee waibhaa mutiiko**

**Heehe waibhaa luuko**

**Hehe waibhwa nyuungu**

**Hehe waibhaa kideende**

**Hehe waibhaa luungo**

**Hehe waibhaa mwanje**

**Hehe waibhaa ngiingo**

**Hehe waibhaa mkaazi**

**Hehe waibhaa ngwaru**

**Hehe waibhaa ighembe**

### **TAFSIRI KWA KISWAHILI**

**Heeee mwanamwali nenda**

**Heeee mwanamwali rudi**

**Heehe umesahau maksai**

**Hee umesahau mwiko**

**Heehe umesahau kijiko**

**Hehe umesahau chungu**

**Heehe umesahau kijichungu**

**Hehe umesahau uteo**

**Hehe umesahau sinia**

**Hehe umesahau ushang'a**

Baada tu ya mvulana kupokonywa dadake aliyembeba mgongoni safari ya kuelekea nyumbani kwa bwana harusi huanza rasmi ambapo wimbo wa *hale kisamo* huimbwa. Mwanamwali hubebwa mgongoni na dada zake mvulana huku wakipokezana hadi wafike nyumbani. Wanapokosekana watu wa jamii ya mvulana wa kumbeba mwanamwali basi watu wa karibu sana naye ndio pekee huruhusiwa kumbeba. Lengo la kutowaruhusu watu ambao sio wa karibu au hawana unasaba na mvulana kumbeba msichana ni kwamba waliogopa watu wengine waliokuwa na jicho la nje ambao wangeweza kuharibu matiti ya mwanamwali kiasi kwamba asingeweza kupata maziwa wakati wa kunyonyesha au hata kuharibiwa kizazi kiasi cha kutopata mtoto.

## **HALEE-E HALE KISAMO**

**Halee-e hale kisamo**

**Halee-e hale kisamo**

**Hoolele holele kisamo**

**Heee haleee hale kisamo.**

**Funga Mburi wededewa kisamo, heee**

**Hoyehoo, hale kisamo.**

**Makurukuru Masinde kisamo, hee**

**Hoyehoo, hale kisamo.**

**Mfurunganje ruruma kisamo,hee**

**Hoyehoo, hale kisamo.**

**Mwari wetu etonga ededwa kisamo,hee**

**Hoyehoo, hale kisamo.**

**Mtongorito shombeni kisamo, hee**

**Hoyehoo, hale kisamo**

**Kwanyika wandu kwarighia kisamo,hee**

**Hoyehoo, hale kisamo.**

**Endamara, wededwa kisamo,hee**

**Hoyehoo, hale kisamo.**

**Irika langu natonga kisamo,hee**

**Hoyehoo, hale kisamo.**

**Wakora nyungu, shidongu kisamo,hee**

**Hoyehoo, hale kisamo.**

**Funga mburi walia kisamo,hee**

**Hoo hoyehoo, hale kisamo.**

**Hake Metinyoki ni rungu ya chuma,hee  
Hoyeo, hale kisamo.**

**Hake Lesareyo ni rungu ya mwingo,hee  
Hoyeo, hale kisamo.**

### **TAFSIRI**

#### **HALEE-E HALE KISAMO**

**Hoyee-e hoye burudani  
Hoyee-e hoye burudani  
Hooye hoyeho burudani  
Heeee hayee ndio burudani**

**Ukifunga mbuzi unasengenywa burudani, hee  
Hooheyo ndio burudani**

**Kukurukakara furahia burudani, hee  
Hooheyo ndio burudani**

**Mvule nguruma burudani, hee  
Hooheyo ndio burudani**

**Bibi harusi wetu anatembea akisengenywa burudani, hee  
Hooheyo ndio burudani**

**Bwana harusi ugenini burudani, hee  
Hooheyo ndio burudani**

**Watu wametawala burudani, hee  
Hooheyo ndio burudani**

**Unapika huku wasengenywa burudani, hee  
Hooheyo ndio burudani**

**Rika langu limekwenda burudani, hee**

**Hooheyo ndio burudani**

**Wasafisha chungu, watukanwa burudani, hee**

**Hooheyo ndio burudani**

**Unafunga mbuzi ukilia burudani, hee**

**Hooheyo ndio burudani**

**Kwa Metinyoki ni rungu la chuma, hee**

**Hooheyo ndio burudani**

**Kwa Lesareyo ni rungu la mti wa mpingo, hee**

**Hooheyo ndio burudani**

Wimbo huu zamani uliimbwa hata wakati wa kuwatawaza machifu. Maneno ya kishairi yaliyotumiwa hubadilika kuambatana na tukio lakini mahadhi hayabadiliki huwa yale yale. Kimsingi, wimbo huu hutukuzwa mno na huimbwa katika kila sherehe muhimu na huchukuliwa kama wimbo wa taifa la Kenya. Huimbwa watu wakiwa katika makundi mawili. Kundi la kwanza ni lile la bwana harusi na lile la pili huwahusisha watu upande wa bibi harusi. Kila upande hujaribu kuonyesha ubingwa wao katika kughani au *kungola reweta*.

Kila baada ya hatua kadhaa katika safari ya kuelekea nyumbani kwa bwana harusi msichana aliyembeba mwanamwali anapochoka kumbeba mgongoni *huterewa* kwa kusema *hiinde lanye* yaani hutoa ishara ya kwamba anaomba msaada kwa dadake mwingine ili amsaidie kumbeba mwanamwali. Watu husimama wakabadilishana kumbeba bibi harusi huku wakiendelea kuimba. Wanapofika nyumbani kwa bwana harusi wasichana walioandamana na bibi harusi hukaa pale kwa siku nne. Shughuli hii hujulikana kama *kuyaiya msenge* au kumlinda mwanamwali kutoonana na mume wake kabla ya siku iliyoamriwa. Mwanamwali pamoja na wasichana wanaokaa pamoja naye hawali chakula kutoka kwa bwana harusi kwa kipindi cha siku nne. Siku ya kwanza hula chakula ambacho huletwa na mamake msichana na wanawake alioandamana nao. Siku ya pili hula chakula kilicholetwa na wasichana ambaa waliandamana na bibi harusi. Siku ya tatu hula chakula kitakacholetwa na mjomba

wake. Siku ya nne wasichana waliokuwa wakilala na bibiharusi hupakwa mafuta kichwani yaani *ilongo*.

Vijana waliokwenda kumchukuwa bibi harusi wanapofika nyumbani kwa bwana harusi huchinjiwa mbuzi ambaye hujulikana kama *mbuji ya irika* au mbuzi wa kujiunga katika kundi la waliooa na debe moja la pombe. Asubuhi ya kuamkia siku ambayo msichana huingia katika boma la mumewe, bwana huvishwa pete yaani *kishongo*. Watu wakiwa katika kibanda yaani *ngondini* mbuzi dume huletwa kisha ngozi iliyo katika sehemu ya mbele ya uso hukatwa na sehemu fulani hutumiwa kutengenezea pete ambayo huvishwa msichana. Ikibainika ya kwamba msichana aliyeolewa alikuwa na mimba basi sehemu ya mguu wa mbele wa mbuzi aliyechinjwa hupelekwa kwa wazazi wa msichana. Ikiwa hana mimba hupelekwa sehemu ya mgongo.

Msichana anapoingia katika boma la jamii ya bwana, babake mvulana akiandamana na wazee wengine wa rika lake humvisha kamba shingoni yaani *ngoi* ambayo hutumiwa katika shughuli za kurina asali. Mamake mvulana naye humpaka mafuta kwenye kipaji chake cha uso kuonyesha ishara ya kwamba amekubalika katika jamii hiyo. Msichana akiwa ameolewa bila wazazi wake kutambua yaani *kuingilia*, siku ya kwenda kwao bwana harusi huenda na beberu moja la mbuzi. Watu wanapofika karibu na nyumbani husimama. Mamake bibi harusi pamoja na bibi harusi wakiwa hawaangaliani wanaletwa pamoja kisha lile beberu huchunwa ngozi kidogo sehemu ya uso kisha mama na msichana wake huvalishwa pete. Baada ya zoezi hili msichana huondoa nguo aliyojifunika usoni kisha wanaonana na mamake ambaye humshika mkono na kumwingiza ndani ya nyumba.

### **2.3.5 Hitimisho**

Katika sura hii tumeangalia utaratibu wa ndoa mionganini mwa jamii ya Wataveta. Jamii ya Wataveta wana taratibu zao za kuoza wasichana wao. Taratibu hizi huandamana na sherehe ambazo hutawaliwa na ulaji wa vyakula pamoja na unywaji wa pombe. Katika jamii ya Wataveta utaratibu wa kuoa hutekelezwa kwa makubaliano baina ya familia mbili zinazohusika. Mtoto wa kike huwa ni mali ya jamii na sehemu kubwa ya mali inayotolewa huliwa na wanajamii.

Kila utaratibu wa kuoa mionganini mwa jamii ya Wataveta huandamana na nyimbo ambazo huimbwa kwa minajili ya kuwafunza maharusi na kutoa changamoto kwa wale ambao hawajaoa. Hata hivyo ikumbukwe ya kwamba katika utaratibu wa kuoa uimbaji huanza mara tu baada ya kumweka mwanamwali ndani. Sehemu yote ya awali huwa ni mazungumzo yakiongozwa na ulaji wa vyakula vya aina mbalimbali. Unywaji wa pombe hasa ile inayotengenezwa kuitia kwa asali ilithaminiwa sana. Ifahamike ya kwamba msingi na utaratibu wa kuoa katika jamii ya Wataveta haukuiongozwa na dini bali mila na tamaduni za jamii hii.

## **SURA YA TATU**

### **TARATIBU ZA KUOA NA NYIMBO ZINAZOHUSIKA KATIKA UTARATIBU WA KUOA KATIKA JAMII YA WASWAHILI**

#### **3.0 Utangulizi**

Katika sura ya pili tuliangazia maswala kuhusu taratibu za kuoa na nyimbo zinazohusika miongoni mwa jamii ya Wataveta. Katika sura ya tatu tumeshughulikia taratibu za kuoa na nyimbo zinazohusika katika jamii ya Waswahili.

#### **3.1.0. Taratibu za Kuoa Katika Jamii ya Waswahili**

Jamii ya Waswahili waliwaoza wasichana wao wakiwa wamebaleghe kinyume na jamii ya Wataveta ambao utaratibu wao wa kuwaoza wasichana ungeweza kuanza hata mama akiwa mjamzito. Katika jamii ya Waswahili huwa kuna ndoa ambazo hupangwa ambazo huwa na utaratibu uliopangwa kuanzia uchumba hadi ndoa. Sherehe ya harusi katika jamii ya Waswahili huwa ni ghali mno na huchukua muda mrefu kuipanga lakini ni yenyekupendeza na kuburudisha sana. Hata hivyo ukweli ni kwamba ndoa katika jamii ya Waswahili yaweza kuwa fupi na yenyekharama ya chini mno ikiwa ni nikaha ikafanywa katika misingi ya dini ya Kiislamu na kuhusisha mila na tamaduni za Waswahili. Mila na tamaduni ni muhimu sana hasa kwa wanandoa ambao ndio mwanzo wameoana tu.

#### **3.1.1. Maana ya Harusi**

Kulingana na wazee wa Kiswahili waliohojiwa, harusi yaweza kuwa na maana mbili. Ya kwanza ni ile ya kuoa na nyingine ni ile ya kutahiriwa. Mvulana alipaswa kutahiriwa kabla hajaoa. Wasichana katika jamii hii hawakutahiriwa. Jamii ya Waswahili walithamini sana sherehe na hususan ile ya harusi. Kama anavyosema Harding (2003:66) anasema kwamba:

Katika jamii za Kiafrika sherehe huchukua nafasi kubwa mno  
katika maisha ya mwanadamu na kwamba sherehe huleta watu  
pamoja ili kusheherekeea jambo muhimu katika jamii. (tafsiri  
yetu)

### **3.1.2. Umri wa Kuoa Na Muda wa Maandalizi ya Harusi**

Jamii ya Waswahili hawakuwa na umri maalum wa wavulana wao kuoa. Wavulana waliruhusiwa kuoa baada na mara tu ya kubaleghe. Wavulana walibaleghe kuanzia umri wa miaka kumi na minne (14) na kuendelea. Hata hivyo, siku hizi wavulana huoa wakiwa na umri wa miaka ishirini na kuendelea kwa sababu wengi wamejiingiza katika harakati za kuendeleza masomo na vile vile kupanda kwa gharama ya maisha kwenda juu na kuwafanya kutaka kuepuka majukumu ya kifamilia. Ifahamike ya kwamba mwanamke katika jamii hii hangeruhusiwa kuolewa mara ya pili kabla ya idhini ya talaka haijatolewa na mume wake. Ikumbukwe ya kwamba mila, tamaduni na dini ya Waswahili huzingatiwa hasa katika maswala ya ndoa. Mume anaweza hata kuoa wake wanne akitimiza uadilifu ambapo uadilifu hapa ukiwa kwa maana ya utaratibu wa dini ya Kiislamu na uwezo wake wa kifedha. Lakini, mwanamke anaweza kuolewa na kuachwa na mwanamume mara tatu na wanaume mbalimbali.

Hata hivyo, ni muhimu ifahamike ya kwamba talaka kwa mwanamke iko chini ya idhini ya mume. Mke hawesi kumwacha mume lakini anaweza “kujifusai” yaani kuomba talaka kwa kadhi ili kuachwa. Mke akiachwa talaka tatu haifai kurudiwa na mumewe au mtalaka wake mpaka aolewe na mume mwengine na aachwe. Muda ambao hutumiwa katika maandalizi ya harusi hutegemea na uwezo wa kifedha wa familia. Shughuli ya kuoa huchukua siku tano (5) au hata miezi minne (4). Hata hivyo, kwa sababu ya kupanda kwa gharama ya maisha, watu wengine huamua kuandaa harusi ambayo huweza kuchukua hata siku moja.

### **3.1.3. Kuchagua Mchumba**

Swala la kuchagua mchumba liliongozwa na wazazi wa mvulana na ambao humtafutia mwana wao mchumba kutoka kwa familia iliyokuwa ama na maadili mema au ya kutajika. Hata hivyo, kulingana na mabadiliko ya kimaisha yanayotokana na utandawazi, elimu wanayoipata vijana pamoja na uhuru wa maingiliano baina ya wasichana na wavulana swala la kuwachagulia wachumba limeendelea kufifia. Hata hivyo, bado kuna baadhi ya wazazi ambao wanaendelea kuwachagulia vijana wao wa kiume na hata wa kike wachumba. Zamani wavulana wakitafutiwa wachumba na kuchumbiwa mapema hata wakiwa na umri mdogo kati ya miaka minane (8) hadi kumi (10).

Katika jamii ya Waswahili mvulana huchaguliwa mchumba na watu wa nasaba yake wakiwemo; mamake, shangaziye na dada zake ambao tayari wameolewa. Ifahamike ya kwamba wasichana hawakuruhusiwa kuonekana na watu ambao hawakuwa na uhusiano wa karibu na familia yao. Kwa hiyo, muda mwingi wasichana katika jamii hii walikuwa wakijificha. Kwa maana hiyo basi, mienendo ya kitabia ya wasichana waliochumbiwa ilijulikana kuitia habari ambazo zilikusanywa kutoka kwa watu ambao walikuwa karibu sana na msichana. Wakati mwingine picha zilitumwa kisiri na shangazi au dadake msichana ili kuweza kumwona msichana aliyemtaka. Vile vile wasichana kadhaa huweza kualikwa ambao mionganoni mwao huwa yule msichana aliyetarajiwa kuolewa. Pia, majirani zake hutumika katika kumsaidia mvulana kumwalikia binti aliyekusudiwa kuposwa.

Mvulana aliyetaka kuoa huonyeshwa wasichana kadhaa ambao hukusanywa kwa pamoja. Hata hivyo wasichana wenyewe huwa hawajui lengo la kuwakusanya. Mvulana huchagua msichana mmoja mionganoni mwa wasichana kadhaa alioonyeshwa. Kulingana na wazee wa jamii ya Waswahili waliohojiwa na mtafiti, jamii ya Waswahili iliruhusu ndoa za ukoo. Kwa mfano, unaweza kumpata mvulana akimuoa hata binamu yake na jamii ikiwa haina pingamizi na ndoa hiyo. Takribani jamii nzima ya Waswahili ni wafuasi wa dini ya Kiislamu ambao huzingatia imani yao kutoka katika kitabu kitakatifu cha Korani na kwamba huwaoza mabinti zao kuambatana na imani ya dini yao.

Mwanamke wa Uswahilini hakuruhusiwa kuolewa na mwanamume ambaye hakuwa mwislamu lakini mwanamume aliruhusiwa kumuoia mwanamke ambaye hakuwa mwislamu ilimradi mwanamke huyo asilimishwe. Kulingana na wazee wa Kiswahili waliohojiwa akiwemo mzee Abdala Mmbwana, mwanamume angweza kuoa kutoka katika nyumba ya watu maskini lakini mwanamke alitarajiwa kuolewa na mwanamume ambaye alikuwa na uwezo wa kifedha. Hata hivyo ifahamike ya kwamba jambo hili halizingatiwi na jamii nzima. Kwa maana hiyo basi, kuona mtu mzima kuoa msichana wa umri mdogo lilikuwa jambo la kawaida katika jamii ya Waswahili. Kulingana na kitabu kitakatifu cha Korani, Mtume alipinga swala la kupeleka posa mahali ambapo tayari pameshaposwa kwani kufanya hivyo kungeleta chuki mionganoni mwa wanajamii. Ila si makosa kuposa mahali palipoposwa.

### **3.1.4. Utaratibu wa Kulipa Mahari**

Mahari hupewa nafasi kubwa sana katika mila ya Kiislamu ambayo kwamba ndio desturi ya Waswahili ambao imani yao hujengwa. Kulingana na wazee waliohojiwa na mtafiti, wazazi wa msichana wakiwa ni waaumini wa dini ya Kiislamu hutaka kupata idhini ya kukubali kuolewa kwa hiari mtoto wao kabla ya swala la mahari halijazungumziwa. Hata hivyo, kulingana na desturi na mila za Waswahili wazazi ndio wenye kuamua au kutoa maamuzi ya mchumba wa msichana au mvulana na hata mahari yatakayotolewa na wala hakuna aliyeweza kupinga.

Baada ya idhini kutolewa basi swala la mahari huafikiwa na wazazi wa pande zote.Kwa mfano: wajomba, mashangazi, babu, nyanya,baba na mama wa mtoto. Mahari ni lazima na ni maelewao baina na mume na mke na hupewa mke na hii ndiyo mila ya Kiislamu. Kama tulivyoeleza hapo awali kuhusiana na mahari basi watu tuliowataja ndio huhusika katika kutaja kima cha mahari na ndio wenye kupokea mahari na hakuna mwenye kupinga. Sana sana mahari inayotolewa huhusisha vitu kama vifuatavyo: kiasi cha pesa walichoridhia wazazi, vitu vyenye thamani, fanicha, mavazi na vitu vya urembo, dhahabu au fedha. Ikumbukwe ya kwamba mvulana hatoi vitu hivyo vyote bali huchagua baadhi au kimoja

Mahari yaweza kuwa fanicha kama vile; kitanda, sofa seti na meza. Gharama ya vitu hivi yaweza takriban kukadiriwa kuwa kama laki mbili hivi (200,000) kwa maisha ya hivi sasa. Mahari yaweza kulipwa kwa njia ya pesa ambayo hukadiriwa kuwa kiasi cha laki moja (100,000) hadi laki moja na nusu (150,000) au vitu vya dhahabu vyenye thamani ya laki moja (100,000) hadi laki moja na nusu(150,000).Mahari vile vile inaweza kulipwa kufuatia utaratibu wa sheria za Kiislamu kwa kuzingatia kitabu kitakatifu cha Korani ambapo msichana aliweza kupewa kiasi cha kima cha shilingi mia moja na ishirini na tano (125) kama ilivyoamriwa na Mtume.

Vile vile, msichana anaweza kuamua ya kwamba mahari yake yatakuwa kitabu kitakatifu cha Korani na Mswala. Kwa maana hiyo basi mahari katika jamii ya Waswahili huwa ni swala la makubaliano na hutegemea nafasi ya familia na uwezo wao wa kifedha. Zamani mahari hayakuwa na kima bali ilikuwa ni chochote mtu alichopewa kwani waliamini ya kwamba kumwekea msichana kiwango cha mahari ni kama kuumuza mtoto.

### **3.1.5. Kuchumbia**

Katika mila na desturi za Waswahili uchumba ndio hutangulia katika harusi iliyopangwa.Kama tulivyoeleza hapo awali wazazi wa mvulana pamoja na wana familia wa karibu na marafiki ndio huhusika sana katika harakati za kumtafutia mvulana mchumba. Mambo yanayowapendeza wazee katika kumtakia kijana wao mke ni pamoja na kuangalia familia ikiwa ni ya watu wenyewe maadili mema na waaumini wa dini ya Kiislamu, wenyewe uhusiano mzuri wa kifamilia, mke mzuri wa kupendeza, mlango wenyewe kuheshimika. Baada ya kukusanya taarifa kamili kuhusiana na familia husika basi familia ya mvulana hutuma ujumbe wa kuchumbia kwa wazazi wa msichana. Ni nadra sana watu kupewa jibu la uchumba siku hiyo.Hata kama familia ina sifa na hadhi ya aina gani si aghalabu kujibiwa hapo hapo hata kama jawabu la uchumba litakuwa limekubalika.

Familia ya mke huchelewesha jawabu ili kutaka kujua hulka na sifa za familia ya mume, uhusiano wao, mali na dini.Katika utaratibu wa harusi zilizopangwa wazazi wa mvulana huwa na habari za msichana ambaye wanamchumbia. Wakati mwingine wazazi wa mvulana hutaka kutambua namna msichana alivyoumbika.Kwa mfano wanetaka kutambua maumbo yake, urefu na hata uzito wake. Baada ya zoezi hili wazazi wa msichana humtaka awape wageni chai na vitafunio. Zoezi hili hufanywa kwa makusudi ili kuwafanya wazazi wa mvulana kuweza kumwona na kumkagua msichana.Baada ya chai, wazazi wa mvulana huweza kuondoka wakiahidi kurudi mapema huku wakiacha nyuma picha ya mvulana aliyekusudia kuo.

Mwanamume aliweza kuoa kutoka kwa familia ya watu maskini lakini mwanamke mara nyingi hupendelea kuolewa na mtu ambaye ana uwezo. Lengo lilikuwa ni kulinda ndoa isiharibike kwa urahisi. Zamani mvulana na msichana waliweza kuchumbiwa hata kwa kutazama picha ambayo huonyeshwa kila mmoja wao. Hali hii ilichangiwa sana na umbali wa wasichana na kwamba wote wawili hawakuruhusiwa kuonana mpaka ile siku ambayo iliamriwa kwao kuonana. Siku hizi haya mambo hayapo tena kwani wavulana huweza kujichagulia wasichana wanaowapenda.

Wanaume walitumwa kwa wazazi wa msichana hupewa tarehe ya kurudi ili kupewa ripoti ya maombi ya uposo kuwa yamekubaliwa au yamekataliwa. Katika kipindi hiki chote jamii ya msichana huweza kufanya vikao mbalimbali kuchunguza endapo familia husika ni ya watu wenyewe vichwa vigumu, aidha ni watu wenyewe magonjwa ya

kuambukiza, uwezo wao wa kulipa mahari, kufanya maandalizi ya harusi au kupanga kukataa posa. Jibu la kukubaliwa au kukataliwa kwa posa linaweza kutolewa kwa mtu yeyote anayeheshimika katika jamii au mwakilishi wa familia. Posa inaweza kukataliwa kwa kutoa maelezo ya kutokukubaliwa au kutotoa maelezo kabisa. Posa yaweza kukataliwa kwa sababu ya umri mdogo wa msichana, hajajua maisha ya kuolewa, anasoma au ameposwa mapema au ameshalengewa au posa imeshapokelewa.

### **3.1.6. Uposo**

Posa ni makaribisho ya uchumba uliokubaliwa.Uchumba ukishakubalika ndipo uposo hupelekwa. Familia ya mvulana hupeleka uposo kwa familia ya msichana kwa wakati maalumu uliopangwa na wazazi wote wa pande mbili. Makaribisho ya mapokezi huandaliwa na watu wa mke kwa vinywaji vya kuburudisha ambavyo huitwa “maji ya mzinga”yakiwa ni pamoja na aina mbalimbali za vinywaji vya matunda. Kwa mfano: avokado, machungwa na vitu vya kuburudisha roho kama vile; kastadi, podini, faluda na vitafunio kama vile keki, kababu, sambusa na donati.

Kama ilivyo desturi ya Waswahili kitafunio cha halua na kahawa huwa havikosekani katika maandalizi hayo ambayo hugharamiwa na watu wa familia ya upande wa mke.Mvulana anayeo a kwa ushirikiano na wazazi wake hujianaa kutoa mahari kwa wazazi wa mke. Baada ya kukamilika kwa zoezi hili basi posa husemekana ya kwamba imekubalika. Mahari yalikuwa yakikadiriwa na wazee kwa mila na desturi za Waswahili, ingawa Uislamu humpa fursa mke kutaja mahari yake mwenyewe.

Wanaohudhuria hafla ya kupeleka na kupokea posa ni wakwe na mashemeji wa baba pamoja na ndugu wa karibu wa mama.Naye mume hufuatana na wazazi wake, shangazi na wajomba. Marafiki wa karibu wa pande zote mbili hualikwa. Wazazi wa mvulana wanapofika nyumbani kwa msichana hutangaza rasmi lengo la kuwatemeblea. “Tumeju na jambo la kheri kutaka jiko,” jiko hapa kwa maana ya msichana. Siku hiyo hufanyika sherehe kidogo ambapo chakula huandaliwa lakini watu waliohudhuria hawajihuishi na uimbaji na uchezaji.

Baada ya karamu hiyo ndogo ya posa wazee wa mume hutaja tarehe ya kuoa na kuafikiana na watu wa mke kwa jambo hilo. Wazazi wa pande zote hushauriana katika mipangilio kamili ya harusi.Hapo ndipo posa hutimu na wachumba hupewa nafasi ya kusalimiana. Wazazi huagana kwa vigelegele na shangwe na nderemo na

kuomba dua kwa mola wao.Hivyo basi, posa inapokubaliwa msichana huwa mchumba wa mvulana.

### **3.1.7. Kupeleka Begi**

Siku hizi wazazi wa mume hupeleka begi kama kipengele kimojawapo cha makubaliano ya mahari. Begi hupelekwa na wazazi wa mume pamoja na watu wa familia mpaka nyumbani kwa wazazi wa mke huku likisindikizwa kwa ngoma na nyimbo. Begi hilo linapofikishwa nyumbani kwa msichana hypokelewa kwa shangwe na nderemo na watu wa upande wa mke. Kabla ya begi kufunguliwa hutanguliwa na dua za kukinga macho ya mahasidi na shari zao.

Begi hufunguliwa huku kila kilichokuwa ndani ya begi kikionyeshwa watu waliohuduria wakishuhudishwa na wakishangilia kwa vigelegele. Ndipo kwa mzaha mwanamke wa upande wa mume hupanda juu ya meza na kulifungua begi na kunadi vitu vilivyomo ndani ya begi hilo. Mtangazaji huanza kwa kusema ni kitu gani huvaliwa wapi na kimenunuliwa wapi? Huonyesha kimoja kimoja kuanzia mavazi, leso, viatu hata vitu vya ndani vya siri kama vile; ushanga wa dhahabu, chupi au koro, buibui, sidiria na virinda. Mwanamke huyu alifanya shughuli hii kwa madaha na sifa akivionyesha vitu vyote hadharani na huku akiigiza kuvivaa kwa kujirembesha kana kwamba ye ye ndiye aliyekuwa bibi harusi.

Mwanamke huyo hunusisha watu manukato yaliyomo ndani ya begi hilo ili wapate harufu za haludi, udi wa mawaridi, na mafuta mazuri na kuwaambia kuwa watatamani tu harufu kwani yao ni kushuhudia tu kwa vile vitu hivyo viliandaliwa bibi harusi. Wakati huo huo jamii iliyohuduria ya mke na mume humtuza na kumshangilia mwanamke anayenadi begi hilo kwa vigelegele anapokuwa akiimba na kucheza wakati wa sherehe hiyo. Nyimbo za sifa na mafumbo na pongezi hushuhudiwa kwa furaha kubwa mno wakati wa maonyesho hayo.

Pesa zilizokusudiwa kulipwa kwa ajili ya mahari pia huweza kupelekwa pamoja na begi na kuhesabiwa hadharani huku zoezi hili likishuhudiwa na watu wa jamii za pande zote mbili. Watu wa mke huandaa vyakula na mapochopochi kwa wageni wa upande wa mume.Kimsingi, desturi ni kuwa mahari hypokelewa baada ya kupeleka posa.Hata hivyo kuonyeshwa kwa mahari hadharani wakati wa kupeleka begi huwa ni mojawapo wa mila na tamaduni za Waswahili.

Mambo haya hufanyika muda mfupi baada ya posa kufanyika nyumbani kwa akina bibi harusi. Sherehe hii hufanywa na kuhudhuriwa na wanawake walioolewa pekee wa rika zote. Sherehe hii hutambulisha ya kuwa harusi inakaribia na ni furaha kwa familia ya upande wa mume. Begi pia huandamana na mahari ambayo hutolewa kwa viwango mbalimbali kulingana na uwezo wa familia ya bwana harusi. Familia nyingi hutumia pesa hizi kununulia fanicha ambazo hupewa msichana anapokwenda kwa mume. Kwa bahati mbaya ndoa inapovunjika na wanandoa kuachana msichana hurudi na fanicha hizi nyumbani kwao.

Begi hutolewa kama zawadi kwa msichana. Talaka ikishinikizwa au ikianzishwa na mke basi mahari hurudishiwa mwanamume. Hata hivyo, taratibu za kuoa zimegeuka sana siku hizi kwa sababu nyingi zikiwemo, mabadiliko ya utandawazi, wasichana kupata elimu zaidi kuliko wanaume na wanawake wengi kutambua haki zao za kimsingi na kuepuka tabia za kuchaguliwa wachumba na wazazi wao. Swala la wanawake kupata elimu ya juu kuwazidi wanaume limewafanya wanawake wengi kuwa na uwezo mkubwa kuliko wanaume. Pete huwa ni zawadi ya mume kwa mke na hupelekwa katika safari ya kwanza ya kuwatemebelea wazazi wa msichana.

Kama tulivyoelezea hapo awali utoaji wa mahari katika jamii ya Waswahili uliweza kufanywa kulingana na imani ya dini ya Kiislamu na kwamba mwanamwali angeweza kupendekeza mahari. Kulingana na wazee wa Waswahili waliohojiwa wanakubaliana ya kwamba maziwa ya mama huwa ni shukurani ambayo hupewa mama kwa malezi bora ya mwanamwali. Sehemu hii huwa ni kiasi cha elfu thelathini hadi hamsini. Maziwa ya mama hugawanyiwa akina mama wa familia kama vile shangazi na wakaza wajomba. Kilemba cha baba ambacho pia ni shukrani kwa baba kwa kumlea msichana ambapo huwa ni elfu thelathini hadi hamsini. Begi huwa na gharama ya laki moja hadi laki moja na nusu. Siku ya harusi hupangwa na hupewa kati ya miezi mitatu au minne ili kuwapatia familia zote fursa ya matayarisho ya harusi.

### **3.1.8. Kufuga Ukuti**

Kufuga ukuti ni kipindi cha majuma au muda ambao mwanamwali huwekwa ndani na haruhusiwi kutoka nje kwa kipindi chote cha matayarisho ya harusi. Muda wote wa kipindi hiki mwanamwali hufundishwa maadili ya unyumba na vile vile kutayarishwa kwa harusi. Inapokaribia majuma mawili kabla ya harusi, mchumba ambaye huwa ni bibi harusi hangeruhusiwa yaani ilikuwa ni mwiko kutoka nje peke yake ila kwa dharura na huambatanishwa na mtu mzima wa upande wake. Zamani bibi harusi alirembeshwa na kungwi ambaye alikuwa mtu mwenye sifa maalum wake kwa namna mbalimbali ya kushauri. Kungwi alikuwa mtalaamu wa masuala ya unyumba kati ya mume na mke na alikuwa ni mama mzee. Humfundisha kuhusu usafi wa mwili, unadhifu na jinsi ya kumstarehesha mume kimpenzi.

Mbali na Kungwi huwa kuna somo ambaye huchaguliwa kutoka kwa baadhi ya wanafamilia au hata wakati mwingine kutoka kwa mtalaamu wa maswala ya Elimu Asilia ya Waswahili na Ndoa. Katika kipindi cha kufuga ukuti Somo humsinga bibi harusi kwa kumpaka mafuta katika ngozi yake na hata kumtoa nywele za malaika katika mwili wake na kumfuta uso ili kuifanya uwe ukimeremeta kama lulu na kumrembesha mwili ili kuifanya ngozi yake iwe laini. Hata nywele zake hutiwa mafuta zikashughulikiwa mpaka zilainike na kuvutia kwa harufu inayovutia na kupendeza.

### **3.1.9. Kueka Goma au Kutia Utı**

Goma huwekwa katikati ya lango la kuingilia nyumba ya bibi harusi na linaweza kuwekwa miezi mitatu kabla ya nikaha. Wanawake ambao hualikwa kuja kuandaa sherehe hii hufanya shughuli mbalimbali kama vile kupura pamba au kutia mito sufi. Watu huja kuimba na kusaidia wenzao kwa shughuli mbalimbali za matayarisho ya harusi. Watu wengi siku hizi hutumia magodoro ya dukani badala ya sufi. Isitoshe, kwa sababu ya gharama ya maisha kwenda juu na wanawake wengi kuajiriwa kufanya kazi za ofisini wengi hawana muda wa kufanya mambo haya. Kwa maana hiyo basi, sherehe hizi hazina uzito mkubwa kama vile zamani.

Zamani goma liliwekwa na “wamiji” yaani kiongozi wa kike katika miji kumi na miwili. Hata hivyo siku hizi goma huwekwa na makungwi endapo mwanamwali mlengwa alipelekwa kwa makungwi au mamake msichana anaweza kuwa na marafiki ambao ni makungwi (Timammy 2002). Kazi yao kubwa ni kumpatia msichana

mafunzo kuhusu mambo yote ya kujamiana na vilevile mbinu za kuishi na mumewe. Siku hizi mambo haya hayafanyiki tena na wachumba hushauriwa aidha na wazazi wao au kiongozi wa dini. Utaratibu wa kualika watu kuhudhuria sherehe ya kupiga goma huanza pale ambapo siku ya kwanza watu wanaoalikwa huwa ni wa upande wa mke ambapo huwa ni nyumba kumi zinazokuwa upande wa Kibla. Siku ya pili watu upande wa mume na ule upande wa mke huungana na kujigawanya ili kupendekeza nyumba ambazo wangezitembelea.

Kuna sababu kadhaa ambazo huchangia katika upigaji wa goma. Goma hupigwa ili kufahamisha watu ya kwamba kuna harusi na watu wote wanaotembelea nyumba hiyo wajue kuwa kuna harusi. Mtu yejote atakayeingia katika nyumba hiyo ni sharti apige goma na asipofanya hivyo huonekana kana kwamba hakuwa na furaha na harusi hiyo alikuwa na 'luhi' yaani choyo cha ndani au alikuwa na wivu.

Goma vile vile hupigwa kuashiria kuanza kwa matambiko na kusoma dua kutoka kwa kitabu kitakatifu cha Korani. Siku ya sherehe goma hubebwa na akina mama huku wakiimba mpaka kwenye langa la nyumba ambapo hulifunga goma kwa kamba ndani ya nyumba. Sadaka za aina mbalimbali kwa mfano, michele, nazi au pesa hutolewa. Kila anayepiga goma hutia pesa. Mtu ambaye hajaolewa au ameachwa na mumewe haruhusiwi kupiga goma.

Kuna utaratibu ambao hufuatwa watu wanapopiga goma. Goma halipigi tu hivi hivi bali sharti lipigwe kwa utaratibu fulani ambao pia hutoa mlio tofauti tofauti ikiashiria jumbe mbalimbali. Kuna watu maalumu ambao hutakiwa kuanza kupiga goma ili wale wengine wafuate. Vile vile kuna nyimbo maalum ambazo huimbwa wakati wa kuliweka goma. Siku hizi wazee ndio hupiga goma. Mtu huweza kutofautisha ujumbe uliobebwa kwenye goma kulingana na mbinu mbalimbali za upigaji na ujumbe uliobebwa katika nyimbo. Kwa mfano:

**Harusi kuanzishwa**

**Tunayo harusi**

**Tunayo**

**Harusi tunaanzisha**

**Tunapiga mbiu kwa wote walitangulia**

**Harusi twaitia udi, ubani na uvumba**

**Mungu ututangulie.**

**Mungu muumba tunakuomba  
Utimize tunayokuomba  
Harusi yetu ifane ili wana tuwaoze  
Wapate na mibaraka kutoka kwako.**

**Pingamizi zisivunje harusi  
Harusi iwe ya heri ili yote yatimie  
Kuanzia mwanzo hadi mwisho  
Goma twalicheza kutangaza harusi**

### **3.2.0. Nikaha ya Siri / Kuozwa kwa Siri**

Watu wengi hawafahamishwi ili kuhudhuria sherehe ila tu watu wa karibu sana na ambao wana uhusiano na familia ya msichana. Wakati mwingine nikaha ya siri hufanyika kwa sababu wasichana wengine hawapendi kuolewa kwa kuogopa macho ya watu. Isitoshe wakati mwingine ndoa ziliweza kuzuiliwa kwa kutumia mazingaombwe hata kutiwa chuki na majirani ili kuvuruga ndoa hivyo basi kutoa mchango wa kufanyika kwa nikaha ya siri. Lengo la nikaha ya siri huwa ni kuwatangazia watu kwamba mvulana ameoa.

### **3.2.1. Nikaha ya Dhahiri / Kuozwa Dhahiri**

Nikaha ya dhahiri au kuozwa dhahiri ni sherehe ambayo hufanywa kwa uwazi na watu wengi hualikwa ili waweze kuhudhuria. Sehemu hii ni muhimu mno kwani ndiyo siku ambayo bibi harusi huozwa kwa mume. Shughuli hii yaweza kufanyika msikitini, ukumbini au hata nyumbani kwa wazazi wa mvulana. Nikaha ya kuozwa husomwa kwa kutoa hotuba kuhusu maadili mema hususani kwa maharusi. Kimsingi, huwa ni tukio la kufungisha ndoa. Qasida huimbwa huku aya mbalimbali kutoka Quran tukufu zikisomwa. Baada ya tukio hili hufuatia gwaride la kumpeleka bwana harusi nyumbani kwake.

### **3.2.2. Gwaride**

Kimsingi,gwaride huwa ni la bwana harusi na hufanywa baada tu kufungwa nikaha. Bwana harusi hupelekwa nje kwa gwaride kwa sherehe kutoka nyumbani au pale mahali palipofungwa nikaha hadi kwa akina bibi harusi ili kutoa mkono wa hongera kwa bibi harusi. Huwa mke ashapambwa. Kipindi hiki mume huwa ashaozwa na hupelekwa kutokea mahali alipoozwa hadi nyumbani kwa mke. Katika safari ya kuelekea kwa bibi harusi wanawake wote huimba na kucheza ngoma. Mume anaenda nyumbani kwa mkewe kuingia nyumbani. Kwa maana ya kwamba kupewa mke. Msichana hutayarishiwa chumba ambacho hukutana na mume wake.Bwana harusi hutoa mkono kwa mke wake huwa ni njia kumzawadia mke kwa vitu kama vile: pesa, mkufu wa dhahabu, pete ya dhahabu au kitu kingine chochote.

Baada ya mwanamume kutoa mkono huandaliwa kombe la bwana harusi. Zoezi hili hufanyika kwa mapishi ya vyakula vya aina ainati ambavyo huandaliwa watu wa mume na marafiki na jamaa zake lakini nyumbani mwa mke. Watu waliohudhuria huimba kwa shangwe na vigelegele. Kwa mfano, wimbo ufuatao huimbwa;

**Bwana harusi asemaje**

**Ataka leo leo**

**Nanyinyi mwasemaje**

**Twataka leo leo**

**Huyoo bwana harusi anaingia**

**Laalaa lalala**

**Anaingia**

**Leo ni leoo hoo×2**

**Sijauona mpambano**

**Kweli si uongo**

### **3.2.3 Limatul - Harus (Chakula cha Mchana)**

Sherehe ya kula chakula cha mchana ambayo hufanyika nyumbani kwa mvulana ambapo wanajamii na marafiki hujumuika pamoja kwa chakula cha mchana. Hufanywa baada ya nikaha na hufanywa na mwanamume akishirikiana na watu wa familia yake. Huweza kufanyika katika sehemu mbalimbali zikiwemo; kwenye ukumbi au kiwanjani. Lengo huwa ni kutimiza suna ya Mtume kwa kutoa sadaka ya

kukirimisha harusi. Watu kutoka katika upande wa mke na mume huhudhria. Huwa si lazima kufanyika ila hutegemea uwezo wa familia

### **3.2.4 Fungate ya Harusi na Kuosha Moo**

Zamani fungate ya harusi ilifanyika baada ya nikaha. Baada ya harusi na wakati wa kipindi cha fungate familia ya upande wa bibi harusi humwandalia bwana harusi sherehe ya kuosha moo yaani kuoshwa miguu. Kuosha moo ni sherehe ambayo hufanyika nyumbani katika familia ya bibi harusi. Siku hiyo bwana harusi huandamana na marafike zake mpaka nyumbani kwa bibi harusi. Wanapofika hukaribishwa chumbani kulikowekwa pazia na nyuma ya pazia hiyo ndipo hukaa bibi harusi pamoja na marafiki zake tayari kwa sherehe ya kuosha moo. Bwana harusi pamoja na marafiki zake hupandisha nguo sehemu ya miguu mpaka kwenye magoti na hupenyeza miguu yao chini ya pazia.

Baada ya zoezi hili marafiki wa bibi harusi nao huwaosha miguu marafiki walioandamana na bwana harusi. Marafiki wa bibi harusi huwafanyia sherehe marafiki wa bwana harusi kwa kuwafinya na kuwavuta vuta miguu pengine kwa lengo la kuwatekerenya. Bwana harusi na marafiki zake hutakiwa kulipa kiasi fulani cha pesa kwa ajili ya zoezi la kuosha moo marafiki zake bwana harusi. Pesa hizo hutolewa kabla ya watu hawa hawajatoka katika chumba hicho. Marafiki wa bibi harusi nao huchukua maji yaliyotiwa mafuta mazuri, kitambaa na sabuni na kuanza kusafisha miguu ya marafiki zake bwana harusi. Ngoma na mayowe ya sherehe hiyo hukithiri pindi bwana harusi anapoingia na wenziwe chumbani mwa kuoshewa moo. Makusudio ya kuoshwa moo ni kumkaribisha bwana harusi katika kundi la waliooa na kumtakia kila la heri katika ndoa.

### **3.3.0 Hitimisho**

Kila utaratibu wa kuoa mionganoni mwa jamii ya Waswahili huandamana na nyimbo ambazo huimbwa kwa minajili ya kuwafunza maharusi na kutoa changamoto kwa wale ambao hawajaoa. Hata hivyo, ikumbukwe ya kwamba katika utaratibu wa kuoa uchezaji huanza mara tu baada ya kumweka mwanamwali ndani. Sehemu yote ya awali huwa ni mazungumzo yakiongozwa na ulaji wa vyakula vya aina mbalimbali. Ifahamike ya kwamba msingi na utaratibu wa kuoa katika jamii ya Waswahili uliongozwa na dini pamoja na mila na tamaduni za jamii hii. Jamii ya Waswahili ni tofauti kidogo na jamii ya Wataveta. Posa inapokubalika na kuanza mikakati ya

harusi, mambo yote huongozwa na nyimbo huku zikiandamana na uchezaji. Wanawake ndio huchangamka sana katika maandalizi ya harusi na hususan katika uchezaji. Wanaume kwa muda mrefu wamehusika katika utoaji wa pesa na hawahusiki katika uchezaji. Kwani uchezaji hufanywa na wanawake pekee.

**SURA YA NNE**  
**ULINGANISHAJI WA FANI ZA KIUTENDI KATIKA NYIMBO ZA HARUSI**  
**MIONGONI MWA JAMII YA WASWAHILI NA WATAVETA**

**4.0 Utangulizi**

Katika sura ya tatu, tulishughulikia suala la utaratibu wa kuo mionganoni mwa jamii ya Waswahili. Katika sura hii, tunashughulikia ulinganishaji wa fani mbalimbali za kiutendi zinazohusishwa na nyimbo za harusi mionganoni mwa jamii ya Waswahili na Wataveta.

**4.1.0 Utendaji**

Katika kuelezea masuala yanayohusiana na fani za kiutendi katika nyimbo za harusi mionganoni mwa jamii ya Wataveta na Waswahili tumejaribu kuzingatia baadhi ya maswali yaliyoulizwa na Finnegan (1992:53-57) kama alivyonukuliwa na Olali (2004). Maswali haya tumeyatumia ili kutuwezesha kuelezea dhana ya utendaji katika nyimbo za harusi mionganoni mwa jamii ya Wataveta na Waswahili. Maswali haya ni: Nani? Lini? Wapi? Nini na Njia gani? Nani mtendaji katika nyimbo za harusi na ni kina nani husikiliza? Shughuli mbalimbali za utendaji za nyimbo za harusi hufanyiwa wapi na ni wakati gani utendaji hutekelezwa? Je, nyimbo inayozungumziwa imewasilishwa kwa njia gani? Nyimbo iliyoteuliwa hutendwa namna gani? Kwa hivyo, ili fani za kiutendi ziweze kukamilika ni lazima ziweze kuruhusu watu wote kujumuika katika utendaji na vile vile watendaji waweze kuitambua hadhira yao. Hivyo basi, mutribu anatakiwa awe na ujuzi wa ubunifu wa hali ya juu anapoongoza wimbo mbele ya hadhira.

Kipengele muhimu cha utendaji ni hadhira. Hadhira kwa kiwango kikubwa hufanikisha utendaji. Anayewasilisha ujumbe hutarajia hadhira kuupokea ujumbe na wakati mwingine hadhira inaweza kubainisha matokea ya ujumbe husika. Kulingana na Finnegan (1977), Okpewho (1992), Alembi (2002) na Miruka (1994) wanakubaliana ya kwamba hadhira mara nyingi katika fasihi simulizi ya Kiafrika huwa hadhira shiriki na sio hadhira tuli katika utendaji.

Uhusiano na mwingiliano kati ya mwasilishaji au msanii na hadhira ndio wanautendaji wanaouita mfanyakiko wa kimawasiliano. Akisisitiza umuhimu wa hadhira katika utendaji hasa katika fani za kiutendi, Kipury (1983: 12) anasema:

Hadhira huwa na umuhimu mkubwa.Hadhira huwa shiriki au isiyoshiriki.Tabia za hadhira hutegemea aina ya utendaji, namna ya uwasilishaji na uhusiano uliopo baina ya msanii na hadhira. (Tafsiri yetu)

Utendaji mwingi hasa wa nyimbo katika jamii za kiafrika ulijumuisha msanii na hadhira. Hadhira katika jamii ya Wataveta na ile ya Waswahili hasa wakati wa nyimbo za harusi ilikuwa ni shiriki au tendi. Licha ya hadhira kuupokea ujumbe na kupata burudani pia ilishiriki katika kufanikisha utendaji huo kwa kuitikia, kupiga vigelegele, kupuliza ala za muziki au miondoko ya ngoma pamoja na mikonyezo, ishara za nyuso, kupiga makofii, kucheka au kubadilisha sauti. Hivyo basi, katika uimbaji wa nyimbo za harusi katika awamu mbalimbali hadhira na utendaji ni vipengele ambavyo havingeweza kutengana. Hadhira ilikuwa utendaji na utendaji ulikuwa hadhira. Hadhira ilijiunga na msanii katika kuimba nyimbo, kuitikia, kucheka, kulia na hata kushangilia, kulingana na ujumbe na hisia zinazojitokeza kutohana na wimbo husika.

Msanii au mtendaji ni kiungo muhimu sana katika utendaji. Wasanii ndio huongoza hadhira katika utendaji wa kisanii katika jamii nyingi za Kiafrika. Hadhira na msanii hawangeweza kutenganishwa katika utendaji.Hoja hii inashadidiwa na Mbogo (1984) katika Matti (1997:55) kuwa:

Katika hatua za mwanzo za maendeleo ya binadamu, hadhira na mtendaji hazingetengeka.Hadhira ilikuwa watendaji na watendaji wakawa hadhira.Hadhira na watendaji walikuwa ukoo mzima au jamii nzima.  
(tafsiri yetu)

Katika utendaji wa nyimbo za harusi katika jamii ya Waswahili na Wataveta wasanii walikuwa waimbaji wenye ubunifu, ujuzi na maarifa kuhusu jamii. Utendaji simulizi ni mbinu ya uwasilishaji wa fani za kiutendi za fasihi simulizi kwa matendo kama minenguo, uso-ishara, vigelegele na kutumia maleba. Kwa mujibu wa Baumann (1977) anaeleza ya kuwa utendaji ni namna ya uzungumzaji. Kimani (2004) anaeleza kuwa mtendaji au fanani huwajibika kwa hadhira kwa kuonyesha umahiri wake wa kimawasiliano katika kuwasilisha maudhui ya wimbo. Utendaji hauwezi kukamilika bila hadhira.Kimani (2004:102) ana maoni yafuatayo:

Iwapo utendaji umetungwa akilini matini simulizi hubakia hazijatekelezwa hadi ziwasilishwe.Ni kupitia kwa utendaji mbele ya hadhira ndipo matini simulizi huweza kuwa na maana.

Nyimbo za harusi mionganoni mwa jamii ya Waswahili na Wataveta haziwezi kuleta maana bila kuwasilishwa mbele ya hadhira hasa katika muktadha unaohusu sherehe ya harusi. Kulingana na Okpewho (1992) anasema ya kwamba pamoja na wasanii wenyewe, hali ya utendaji, ustadi wa msanii, hali na mapokezi ya hadhira hutegemea muktadha wa utendaji na dhima ya utendaji. Vipengele hivi hutekeleza wajibu muhimu katika kufasiri maana katika matini simulizi. Utendaji hauwezi kukamilika bila kuwepo na mahali pa tukio la utendaji. Utendaji wa fasihi simulizi katika jamii za Kiafrika hauweza kutendeka mahali popote bali hutendeka katika sehemu na kwa malengo husika. Hata hivyo, utendaji uliofungamanishwa na harusi kama vile wimbo wa harusi ultendeka mahali sherehe hiyo ilipofanyika. Utendaji wa nyimbo za harusi katika jamii za Waswahili na Wataveta ulifanyika ama jioni au wakati mwininge usiku mahali wazi nyumbani kwa bwana au bibi harusi. Siku ya harusi utendaji ulifanyika katika eneo la harusi yaani nyumbani kwa msichana au mvulana au hata wakati mwininge njiani wakielekea nyumbani. Hivyo basi katika suala zima la mahali pa utendaji wa nyimbo za harusi ni bayana kuwa utendaji ultendeka mahali popote katika awamu mbalimbali za sherehe ya harusi.

Utendaji katika nyimbo za harusi katika jamii ya Waswahili na Wataveta hufanikishwa zaidi na matumizi ya maleba. Maleba yakiwa ni mavazi yanayotumiwa na msanii katika utendaji akiyatuma katika hali na sura yake ya kawaida. Mifano ya maleba ni kama vile kuvaajaa njuga, kujipaka rangi mwilini. Were na Wandibba (1988:85) wanaelezea kwamba maleba hutumiwa hivi:

Wanaume hufunga njuga na hubeba ngao na mikuki. Wanaume na wanawake hujifunga manyugi (vibwaya) viunoni ambazo ni sketi za kuchezea zilizotengenezwa kwa majani ya mukindu au murugunyu. (tafsiri yangu)

Fasihi simulizi ya Kiafrika hujitegemea na ujumbe wake hutegemea jamii ili kuweza kufaulu. Kwa maana hiyo basi, hamna utafiti wowote wa nyimbo za harusi katika jamii ya Kiafrika utakaofaulu kwa kutumia matini iliyoandikwa pekee bali pia sharti ujumuushe tajiriba ya mutribu ambaye ndiye huwasilisha nyimbo kwa hadhira. Lakini,

ni lazima uzingativu wa aina ya hadhira, ujumbe unaotakiwa kuwasilishwa, ujuzi wa mutribu na mambo yote ya kimsingi yanayohusishwa na utendaji wenyewe yazingatiwe.

Harusi huwa ni mojawapo ya nafasi muhimu ambazo jamii huzitumia ili kuweza kukutana, kujuliana hali za kimaisha na kimaendeleo na vile vile kusherehekeea kuoza au kuoza kwa wana wao. Hivyo basi harusi ni kigezo muhimu cha kujenga umoja na ushirikiano mionganoni mwa jamii. Wakati mwingine sherehe za harusi hutoa fursa au kujenga mazingira ambayo baadhi ya watu huweza kujipatia marafiki au hata wachumba. Kulingana na Finnegan (1977) anasema ya kwamba,

“kila kipengele katika fasihi simulizi hakiwezi kufikia katika upeo wake wa maana pasipo uzingativu wa ufaafu wa fani za kiutendi.” (tafsiri yetu)

Ikumbukwe ya kwamba tunapozungumzia masuala kuhusu nyimbo za harusi tuelewe ya kwamba kuna ushahidi wa kutosha ya kwamba upo uhusiano mkubwa kati ya fani za kiutendi na tafsiri ya maana ya ujumbe wenyewe amba o huandamana na nyimbo husika hususan zile za harusi. Fani za kiutendi zikiwemo ishara za macho, mikono na vidole, minenguo ya mwili na kimya vyote ni viango mahususi vya mawasiliano. Kimsingi, fani za kiutendi hizi ni vigezo muhimu vya kuelezea dhana ya nyimbo ambavyo humpa fursa mtendaji ili kuweza kuifikia hadhira na huwa ni njia mahususi ya mawasiliano katika nyimbo za harusi. Fani za kiutendi mionganoni mwa jamii ya Waswahili na Wataveta huwa ni mbinu mahususi ambazo hutumiwa na jamii hizi zikiambatana na nyimbo sana sana zile hasa zinazomlenga bibi harusi. Lengo kuu la matumizi ya fani za kiutendi ni pamoja na kupitisha ujumbe kwa hadhira, kuburudisha, kumpa mwanamwali ushauri nasaha kuhusu majukumu ya kuwa mke na akumbuke ya kwamba kipindi hicho chote atakuwa amevuka kutoka katika upande wa ujanani na kujiunga na upande ule mwingine wa utu uzima.

Kulingana na Miruka Okumba(2003) anaeleza ya kwamba

“utendaji ni mbinu ambayo hutumiwa katika uimbaji ili kupitisha ujumbe kutoka kwa mutribu hadi kwa hadhira kwa kutumia mbinu ya uchezaji” (tafsiri yetu)

Kimsingi, uasilishaji huu unaandamana na minenguo ya mwili na ishara za uso kwa wote waliohudhuria. Mtendaji katika harakati za uimbaji anaweza kuonyesha thamani yake kubwa katika uchezaji kwa kutingisha kichwa chake, kuinua mkono wake juu au kuuzungusha pande mbili huku akiwa amesimama. Hadhira hata kama itakuwa na wachezaji na watazamaji wanaoshiriki kwa pamoja katika uimbaji lakini pia ni sharti wakati wote wawe katika njia ya kuhusishwa kikamilifu kwa njia ya moja kwa moja ili kuweza kufikia kiwango kinachostahili cha nyimbo na kuwasilisha ujumbe ufaao wa utendaji kwa hadhira.

Nyimbo hutumia fani za kiutendi na ndio maana huthaminiwa sana katika sherehe za harusi mionganoni mwa jamii ya Wataveta na ya Waswahili kwa jumla. Katika jamii ya Wataveta sherehe nyingi hutumia fani za kiutendi. Kwa mfano, katika sherehe ya kutahiri watoto,kuomba mvua,kusherehekeea harusi,ushindi katika vita na hata katika kuwatawaza machifu nyimbo mbalimbali zikihusishwa na fani za kiutendi ziliimbwa ili kupatia tukio hilo hadhi inayotarajiwa.Ikumbukwe ya kwamba katika tamaduni mbalimbali za Kiafrika,nyimbo huchukua nafasi kubwa mno katika sherehe zote katika uhai wa maisha ya binadamu. Kwa maana hiyo basi, nyimbo katika sherehe yoyote ile huwa na jukumu la kuleta watu pamoja na kuwapatia fursa ya kusherehekeea mambo muhimu katika maisha yao ya kila siku.

Kulingana na Kabira na Karega, (1988)

Ikiwa hadhira ina uhai katika utendaji wake na watu wote wahusike katika utendaji basi wanaweza kumpatia mutribu changamoto ili aweze kuwa mbunifu zaidi katika kutekeleza wajibu wake katika wimbaji. Hata hivyo, kwa upande mwingine endapo hadhira ni tuli na sio ile ya kutoa changamoto za kutukuza basi mutribu hawezu kuwa mbunifu wa kutegemewa na mara nyingine huweza kukatiza uasilishaji(tafsiri yetu)

Kwa maana hiyo basi, ni muhimu mutribu ajitahidi kuwa na uwezo wa ubunifu wa hali ya juu sana ili kuweza kutambua hali halisi ya hadhira yake, hamu yao na kwamba wataweza kufurahia uasilishaji wake au kuukataa. Mutribu katika fasihi simulizi ni nguzo muhimu mno,mara nyingi huonekana kama mpokeaji na wakati mwingine akafanya kazi ambayo ni ya ubunifu katika utunzi wa nyimbo ambazo huongoza.Hata hivyo jukumu lake muhimu huwa ni kukumbuka na kuwasilisha

maswala muhimu na kuyaweka katika uimbaji na vile vile maswala ibuka kwa hadhira.

Hata hivyo, swala la kumbukizi katika uimbaji wa nyimbo katika fasihi simulizi limekuwa na mjadala mkubwa sana.Kulingana na Massamba (2002) anatoa sababu zake za kukosoa jambo hili kama ifutavyo: (a) hali ya ati ati kuhusu masimulizi ya utendaji na vile vile jinsi fasihi simulizi ilivyo ya muda mrefu (b) ukuaji wa uhamasishaji wa umuhimu wa utendaji na madhara ya hadhira na utunzi wa utungaji na mbinu za uwasilishaji ambao umetanda kwingi hasa katika matumizi ya video (c) utafiti ambao tayari umeshafanywa kuhusu masuala muhimu ya fasihi simulizi.Hata hivyo, ni swala linalozingatiwa na wengi kwamba mutribu katika fasihi simulizi anaweza kutatizwa na hadhira au tukio linalohusika katika utendaji wake.Isitoshe,hali na makubaliano mionganoni mwa hadhira inaweza kutatizwa na urefu wa kile kilichoandaliwa.

Mutribu katika fasihi simulizi huonekana kama mpokeaji tu ambapo jukumu lake kuu ni kukumbuka mambo yote muhimu katika utendaji wake na kuwasilisha maswala ibuka kwa hadhira. Kwa hiyo inaonekana ya kwamba mwimbaji au mtunzi anayeimba bila utata sharti awe ameiradidi kazi husika kutoka kwa kumbukizi zake za awali ili aweze kuwasilisha kazi asilia.Ni kweli kwamba nyimbo nyingi huwa tayari zimeshatungwa hapo awali na watu ambao hata hawajulikani.

Kwa hiyo kazi kubwa ya mutribu huwa ni kuongoza katika uimbaji na utendaji na mambo haya hupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Mutribu katika nyimbo za harusi ana vitu vingi ambavyo viko karibu naye ambavyo huweza kuvitumia katika hali ya kuendeleza kazi yake kwa hadhira. Kwa hiyo kazi anayofanya mutribu hukaribiana sana na kazi ya hadhira.Kukaribiana huku katika utendaji kunaipatia hadhira na mutribu nafasi ya kuwa karibu ili kuendeleza hali ya kufaulu na wakati mwingine kubaini ujumbe uliobebwa ndani ya maneno yaliyotumiwa katika uimbaji.

Miongoni mwa jamii mbalimbali za Kiafrika watu wakiwa katika shughuli za uimbaji hususan katika sherehe mbalimbali huweza kusitisha shughuli zao zote za kawaida kwa kuziweka kando na kila tukio hupewa nafasi yake inayostahili. Hivyo basi nyimbo za harusi zaweza kuchukuliwa kama njia mojawapo ya kukumbuka tamaduni zao, matambiko, historia ya jamii na chanzo cha jamii husika. Mambo haya yote

yanaweza kubainishwa kupitia kwa nyimbo mbalimbali. Kimsingi, nyimbo zinaweza kuwa kiunzi muhimu cha kuitambulisha jamii na utamaduni wake.

Watu wengi wa rika na jinsia mbalimbali hujumuika katika kusherehekeea harusi hivyo basi kuonyesha namna wanavyopenda kujihusisha na sherehe za kuoa.Kama anavyosema Ruth Finnegan (1992:28)

ili fasihi simulizi ambayo inayohusu uimbaji kufikia  
katika kilele chake ni lazima fani za kiutendi ziweze  
kutumika. Maandishi ya nyimbo pekee hayawesi  
kukidhi mahitaji ya nyimbo katika hadhira.(tafsiri  
yetu).

Kwa maana hiyo basi, ni sharti aina ya utendaji na hadhira inayohusika iweze kuzingatiwa. Tukumbuke ya kwamba utaratibu wa kuwasilisha nyimbo za harusi waweza kuwa katika viwango viwili ambapo huwa ama katika hali ambayo imepangwa au ile ambayo haijapangwa ambayo pia huhusisha kujumuika kwa hadhira.

Kulingana na wazee wa Kitaveta waliohojiwa na mtafiti wanaeleza ya kwamba kuna dhana potovu kuwa tamaduni za Wataveta hasa katika fani za kiutendi zinafanana na zile za jamii ya Wamasai. Jamii mbalimbali zinapokaribiana katika shughuli zao mbalimbali za kimaisha hukopeshana mambo mbalimbali mionganini mwao ikiwa ni mila, tamaduni, mavazi na kadhalika.Kwa maana hiyo basi, Wataveta ambao wanapakana na kabile la Wakakhe wakakopa baadhi ya mila zao. Wakakhe nao vile vile wakakopa baadhi ya mila na tamaduni za Wataveta. Wakakhe ni mionganini mwa jamii zinazopatikana mpakani mwa nchi ya Kenya na Tanzania katika mkoa wa Kilimanjaro nchini Tanzania.

Kabila hili ambalo pia tamaduni zao zinafanana kwa kiwango fulani na zile za Wamasai wameishi na Wataveta kwa miaka mingi kiasi kwamba waliweza kuingiliana katika mambo mengi ikiwemo tamaduni zao. Hivyo basi, kwa sababu ya kufanana kwa tamaduni za Wamasai na Wakakhe na kwamba Wakakhe na Wataveta waliishi katika maeneo ambayo yanakaribiana, baadhi ya watu wakachukulia ya kwamba Wataveta walikopa tamaduni zao kutoka kwa jamii ya Wamasai.

Kwa mfano,Wakakhe na Wataveta kuvalia vazi lenye rangi ya damu ya mzee au maruni katika uchezaji wa nyimbo zao za harusi.Hata hivyo fani za kiutendi za Wakakhe ni tofauti na zile za Wataveta. Kwa mfano, katika jamii ya Wakakhe wanaume na wala sio wanawake ndio pekee huruka wakati wa kuimba na huruka wakiwa wamenyooka twaa kama mshale. Ilihali jamii ya Wataveta huwashirikisha wanaume pamoja na wanawake katika uchezaji ambapo wanaume huruka wakiwa wameikunja miguu yao hasa sehemu ya nyuma na kifua kukiinamisha kidogo kwa mbele sehemu ya vifua vyao wanaporuka.

Kama tulivyotangulia kusema hapo awali, katika jamii ya Wataveta watu huanza kusherehekeea na kushangilia harusi siku ambayo msichana anawekwa ndani ya nyumba kwa kipindi ambacho huamuliwa na watu wa jamii ya bwana harusi. Baada tu ya kufaulu kuuvunja mlango na kumpaka msichana mafuta kwenye paji lake la uso, vijana walioandamana na bwana harusi huanza safari ya kurudi nyumbani huku wakishangilia kwa shangwe hoihoi na vigelegele. Katika jamii ya Waswahili shughuli rasmi ya kusherehekeea harusi huanza mara tu baada ya uposo kukubaliwa na jamii ya msichana.

#### **4.1.1. Ishara za Uso**

Ishara za uso kama mojawapo ya fani za kiutendi za fasihi simulizi hujitokeza kwa njia mbalimbali wakati wa uimbaji. Kwa mfano, kulegeza au kuangaza macho, kuonyesha tabasamu, kukunja uso, na hata kukenua meno ni mionganoni mwa fani za kiutendi ambazo hutumiwa wakati nyimbo za harusi zinapoimbwa. Ujumbe muhimu ambao hubebwa na takriban ishara zote za uso wakati nyimbo za harusi zinapoimbwa ni furaha.

Hata hivyo, katika jamii ya Wataveta, hali ya hasira huweza kujitokeza hususan katika mojawapo ya taratibu za kusherehekeea harusi. Hali hii hujitokeza hasa wakati ambapo jamii ya bwana harusi hufika nyumbani kwa familia ya bibi harusi katika harakati za kumpeleka bibi harusi nyumbani kwa bwana harusi. Baadhi ya aila ya msichana hujawa na jazba wanapomwona mmoja wao akiwaacha. Wachezaji waliweza kuonyesha hisia za hasira usoni kwa kukunja uso na kuufanya matuta ili kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa. Mikunjo usoni huwa ni dalili ya hasira na hata kukerwa na jambo fulani katika mchakato wa uimbaji au hata shughuli nzima kwa ujumla. Ishara za uso hubadilika mara kwa mara wakati wa uimbaji na hufuutiliwa sana na

wapokeaji. Kuna ushahidi wa kutosha ya kwamba maana inayobebwa ndani ya ishara hizi yaweza kuafiki malengo ya uimbaji hasa kuambatana na fafanuzi za jamii na tamaduni mbalimbali.Kulingana na Bukenya, et.al (2010)

“Kila fani ya kiutendi ambayo ina uhusiano na ishara za uso na kwa kila fani ya kiutendi ambayo mtendi hufanya hutoa mchango kwa kufikia kiwango chake kwa kutoa mchango kwa watazamaji na husaidia kila mtazamaji kuelewa mambo yanayotendeka”(tafsiri yetu)

Kwa mfano, kuwa na jazba, mshtuko au mhemuko katika uimbaji kuonyesha hisia za uhalisia wa wahusika katika uimbaji. Kwa mfano katika wimbo wa *Halee-e hale kisamo* kuna fani ya kiutendi ya ishara ya uso hasa waimbaji wanapofikia katika sehemu *funga mburi wededwa kisamo* ambapo waimbaji hukunja nyuso zao ni kuzifanya matuta kuonyesha jazba,humtayarisha bibi harusi ya kuwa atakuwa akisengenywa hata kama akifanya jambo lolote zuri.

**Halee-e hale kisamo**

**Hoolele holele kisamo**

**Heee hale kisamo**

**Funga mburi wededwa kisamo,hee**

**TAFSIRI**

**Hoyehoo, hale kisamo.**

**Hoyee-e hoye burudani**

**Hoyee-e hoye burudani**

**Hooye hoyeho burudani**

**Heee hayee ndio burudani**

**Ukifunga mbuzi unasengenywa burudani,hee**

**Hooheyo ndio burudani**

Ikumbukwe ya kwamba mbali na kuonyesha fani ya kiutendi ya uso ishara kuna vile vile fani ya kiutendi inayoonyesha hali ya furaha. Kwa mfano waimbaji na hata hadhira wanaweza kuonyesha nyuso zenye furaha kwa kuonyesha tabasamu. Hali hii inaweza kujitokeza hasa siku ambayo mwanamwali hufikishwa nyumbani kwa bwana

harusi. Wanajamii na wale wote walioandamana na mwanamwali wanapomfikisha bibi harusi nyumbani kwa bwana harusi hulakiwa kwa vifijo, vigelegele, shangwe na hoihoi. Kwa mfano katika wimbo huu

**Mwai wetu eohiyoo tumuenda tummbhone**  
**Mwai wetu eohiyoo tumuenda tummbhone**  
**Ambiere tumubhokeje tumuenda tummbhone**  
**Mwai wetu eohiyoo tumuenda tummbhone**  
**Akuundae akundae**  
**Akuunda akuundae**

### **TAFSIRI**

**Bibi harusi wetu yuko wapi tunataka tumuone**  
**Kivyere tumshangilie tunataka tumuone**  
**Bibi harusi wetu yuko wapi tunataka tumuone**  
**Amependa amependa**  
**Amependa amependa**

Kuna fani ya kiutendi ya ishara ya uso hasa pale waimbaji wanapofikia katika sehemu ya *akuundae akuunda* ambapo waimbaji huimba kwa shangwe, vifijo na nderemo. Hii ilikuwa ni ishara tosha ya kuwa mwanamwali anayeolewa alikubaliwa katika boma na kwamba idadi ya watu katika familia ile iliongezeka.

**Halee ee hale kisamo**  
**Holele holele kisamo hee**  
**Halee kisamo**  
**Mwari wetu lienda lidedwa kisamo hee**  
**Hale kisamo**

Katika jamii ya Wataveta pia kuna fani ya kiutendi katika wimbo wa *hale ee hale kisamo* hasa wachezaji wanapofikia katika sehemu ya *Mwari wetu lidedwa kisamo* waimbaji huimba wakiwa katika mistari miwili ambapo mmoja huwa ni wa wanaume na mwingine huwa ni wa wanawake. Katika harakati za kucheza mwanamume huweza kutoa ishara ya jicho kwa mwanamke ambaye amependezewa na uchezaji wake kisha akamwendea na akimfikia karibu hupiga mguu mmoja chini kwa kishindo. Mwanamume amfikiapo mwanamke hufanya ishara ya kulegeza macho

yake na huonekana kufanya ishara ya kukunja shingo yake kidogo upande mmoja kisha wote huanza kuruka juu sawia kwa pamoja.

Baada ya kuruka mara mbili au tatu hivi wote husimama na mwanaume humwegemea mwanamke kwa kumwekea kichwa begani kwa sekunde chache tu kama njia ya kuonyesha madido katika uchezaji.Kimsingi,fani ya kiutendi ya kumfungia jicho mtu huwa haitoeki tu hivi hivi tu bali hutokea ama kwa mtu ambaye umependezewa na uchezaji wake,au Mara nyingine hutokea kwamba wanaoruka kwa pamoja huwa wana usuhuba wa kimapenzi au hata wakati mwingine hutokea ya kwamba mmoja kati yao amependezwa na uimbaji wa mwimbaji mwingine.

Katika jamii ya Waswahili kama ilivyo katika jamii ya Wataveta, kuna fani za kiutendi ambazo hutokana na mabadiliko ya ishara za uso.Kwa mfano, kuna fani za kiutendi katika wimbo “paka mapepe”

**Fanya ufanyakayo fanya**

**Umweke umwekavyo**

**Nilikwisha kukanya**

**Huyo si wa kuridhisha**

Waimbaji wanapofikia katika sehemu hii “fanya ufanyakayo fanya” waimbaji hutoa ishara ya kutoa macho pima na kuyapesapesa kulia na kushoto na kufanya waonekane kama watu wenye majivuno na ambao hawajali vitendo vya walengwa.Katika wimbo“ maso maso” kuna fani ya kiutendi ya uso-ishara pale ambapo wanawake hutoa ishara kama kuonyesha tendo la kuwaita wanawake hasa wanapogusa macho yao kwa vidole na kutoa ishara za kuwaita wanawake waje ili waweze kucheza kwa pamoja.Kinyume na jamii ya Wataveta ambao hawatumii vidole vyao katika harakati za kuonyesha fani za kiutendi za ishara za uso.

**Somo yake bibi harusi aje tumfunze mwari  
asiende kufedheheka**

**Ukiitwa na mumeo mama ni wajibu kuitika**

**Wewe bibi umwitike bwana labeka**

**Umridhie mumeo kwa kila analolitaka**

**Aati aje hapa tuhangaike naye**

**Ati aje hapa**

**Tuhangaike naye**

Kwa maana hiyo basi ikumbukwe ya kwamba jamii hizi mbili hutumia fani ya kiutendi ya ishara za uso katika mbinu za kudhihirisha utendaji katika nyimbo zao za harusi.Hata hivyo ujumbe unaopitishwa katika ishara hii hutofautiana.

#### **4.1.2 Kunyamaza Kimya**

Kunyamaza kimya katika nyimbo ni mbinu ya makusudi ambayo hutumiwa na wachezaji wa nyimbo za harusi.Lengo hasa ni kupidisha jumbe mbalimbali ili ziweze kuwafikia walengwa au hadhira katika kuonyesha ya kwamba kulikuwa na jambo muhimu lililobebwa katika wimbo husika.Kunyamaza kimya kwa muda katika nyimbo za harusi huleta matarajio au kuipatia hadhira nafasi ya kutafakari yote yaliyojiri kabla ya kuendelea na uimbaji wa wimbo. Huwa ni mbinu mahususi ambayo hufanywa kwa makusudi ili kuweza kuifanya hadhira kuwa na usikivu na kuteka nyara hisia zao kuanzia mwanzo wa nyimbo hadi mwisho.

Wamitila, K.W.(2002:90) Katika kushughulikia kimya katika Uhakiki wa Tamthilia anasema kuwa

tuisomapo tamthilia hatuwezi kuutambua uzito wa kisanaa  
pamoja na athari inayotolewa na matumizi ya kimya.Kimya  
huweza kutumiwa kusisitiza kiwango cha athari ya kisanaa  
na maneno fulani.Pia husisitiza na kulifanya jambo  
maalumu litokeze mbele ya mengine na kuweza kuwazia  
kwa makini.

Kuambatana na maelezo haya tutakubaliana ya kwamba nafasi inayopatiwa mutribu wakati wa uimbaji wa nyimbo sharti iwe katika hali ya utendaji unaofaa ili kuifanya kazi yake iweze kufana na kuweza kunasa fikra au mvuto wa nyimbo kwa hadhira.Hata hivyo aina hizi za nyimbo lazima pia zitegemee tajiriba ya mutribu katika kuzipitisha mbele ya hadhira. Mutribu na waimbaji wenye haiba ya hali ya juu katika majukumu yao ya uimbaji huweza kutekeleza fani ya kiutendi ya kunyamaza kimya katika uimbaji kwa njia rahisi mno kuliko yule ambaye hana sifa za aina hiyo.

Katika jamii ya Wataveta kuna fani ya kiutendi katika wimbo katika kiwango cha kunyamaza kimya hasa waimbaji wanapofikia katika kibwagizo *akuunda ee akuunda*. Watendaji hasa wanawake hunyamaza kwa muda kukawa na ukimya wa muda kisha wakaendelea kuimba. Kitendo cha kunyamaza kimya katika sehemu hii kinasisitiza ya kwamba msichana anayezungumziwa alikubali kuolewa.

**Atoonga mbwanyeni atoonga**  
**Atoonga ee atoonga**  
**Akuunda ee akuunda**  
**Akuunda ee akuunda**

### **TAFSIRI**

**Ameenda jamani ameenda**  
**Ameenda ameenda**  
**Ameenda ameenda**  
**Ameependa amependa**

Katika jamii ya Waswahili kuna fani ya kiutendi ya ukimya katika wimbo “Paka mapepe huyo” hasa waimbaji wanapofikia sehemu hii “Habibu mimi niko.”

**Akipenda msukume x2**  
**Tena sikusalimu**  
**Mkomeshe akukome**  
**Atabaki alalame**

**Habibu mimi niko**  
**Siku zote mi ni wako**  
**Sitoe mtu kwako**

Kwa sababu ya mabadiliko ya kimaisha na athari zinazotokana na matumizi ya utandawazi, mbinu za uimbaji hususan katika kipengele cha ukimya, utendaji wenyewe na maudhui katika nyimbo za harusi yamebadilika. Waswahili wanafahamika sana katika matumizi ya ishara za vidole katika nyimbo zao za harusi huku zikifua tifa na ukimya, ili hali jamii ya Wataveta huonyesha ishara za ukimya kwa kuinua na kupiga mguu mmoja chini na kisha kuendelea na uchezaji ama kunyamaza katikati ya nyimbo au katika kiti.

#### **4.1.3 Kiitikio**

Kulingana na Akivaga na Odaga (1982:13) wanasema:

“kiitikio katika fasihi simulizi huweza kuchukua mikondo mbalimbali. Kwa mfano, kiitikio chaweza kuwa katika kiwango cha wazo moja, matukio au kadhia ambazo hurudiwa rudiwa katika nyimbo kwa kutumia maneno mbalimbali. Wakati mwingine waweza kupata maneno, aya au hata sentensi zikirudiwa rudiwa mara kwa mara katika nyimbo.” (tafsiri yetu)

Kwa hiyo kiitikio katika nyimbo za harusi chaweza kuwa katika hali ya neno ambalo hurudiwa rudiwa, aya, sentensi au hata nyimbo kwa ujumla ambayo hurudiwa rudiwa. Kiitikio sharti kiweze kujisimamia chenyewe na kutosheleza malengo au majukumu ya nyimbo. Kwa hiyo, kiitikio sio lazima kiwe katika hali ya neno ambalo hurudiwa rudiwa lakini kinaweza kuchukuwa maumbo mbalimbali. Hutokea kwamba muundo wa nyimbo huweza kubadilisha neno lakini mahadhi yakasalia kutobadilika. Mbinu iliyo bora katika uwasilishaji wa nyimbo za harusi katika sehemu ya kiitikio hutawaliwa na ujuzi alionao mutribu ukifuatiwa na marudio ya kiitikio chenyewe. Kiitikio hutumika katika kusositiza ujumbe katika nyimbo na kujenga dhana ya kuwahusisha watu wote katika uimbaji na vile vile kuikumbusha hadhira kuhusu yale mambo muhimu katika wimbo.

Kulingana na Kimani, N (2004:117) anasema,

“jukumu la hadhira katika kiwango cha mawasilisho ya Nyimbo hutawaliwa zaidi na namna ambavyo fani za kiutendi zitakavyojibiwa na mutribu. Hivyo basi, kutoa mchango mkubwa wa kuwasaidia washirika kukumbuka yale yote yaliyosemwa au kuimbwa. Kiitikio huonekana kama njia mahususi ya kipumuo ambacho huwapatia watendaji muda wa kufikiri na kupanga mambo ambayo yangefuata. Hivyo basi kiitikio kinaelezea haja ya kuwa na hadhira sikuvi katika utendaji. Kimsingi, kiitikio huwa kama pumziko ambapo huwapatia wachezaji muda wa kufikiri na kupanga yatakayojiri”. (Tafsiri yetu)

Kwa hiyo kiitikio chaweza kuleta mabadiliko yanayoweza kuipa hadhira hamu ya kutaka kuendelea kusikiza wimbo. Baada ya watu kuimba mstari mmoja au miwili hivi, mstari ule wa mwisho hurudiwa. Kwa mfano katika jamii ya Wataveta kuna fani

ya kiutendi ya kiiitikio katika wimbo *eshenenete sa mshamba wa igonji*. Waimbaji hurudia sehemu hii *saa mshamba wa igonji* kila mara baada ya mwisho wa ubeti. Hali hii huonyesha ya kwamba wasichana wote wamemeremeta kama mkia wa kondoo. Kiitikio kama mojawapo ya fani za kiutendi katika nyimbo za harusi mionganoni mwa jamii ya Wataveta kimetumiwa katika hali ya kusisitizia jambo fulani katika uimbaji.

**Bhaiya bhoze bheshenenete**

**Saa mshamba wa igonji**

**Saa mshamba wa igonji**

**Woowi bheshenenete**

**Saa mshamba wa igonji**

**Bhabora bhoze bheshenenete**

**Bhabora bhoze bheshenenete**

**Saa mshamba wa igonji**

**Saa mshamba wa igonji**

## **TAFSIRI**

**Kina mama wote wanameremeta**

**Kama mkia wa kondoo**

**Kama mkia wa kondoo**

**Jama wanameremeta**

**Kama mkia wa Kondoo**

**Wasichana wote wanameremeta**

**Wasichana wote wanameremeta**

**Kama mkia wa kondoo**

**Kama mkia wa Kondoo**

Katika jamii ya Waswahili kiiitikio hutumiwa katika kusisitizia ujumbe ambao huweza kuwa katika njia ya kusifu, kusuta, kukomoa au kuelimisha. Kwa mfano, kuna fani ya kiutendi katika wimbo “Harusi Howa Chooni ” ambapo wachezaji hurudia sehemu hii “harusi chooni Howa” kila baada ya mwisho wa ubeti. Matumizi ya kiiitikio hapa ni kusisitiza ujumbe ambao umekusudiwa katika wimbo.

**Huo wiya wa mwana**

**Huo wiya wa mwana**

**Wiya wa mwana umetenda nganu na mpunga  
Hai kanga wangu ndokose ye pweke naindoni  
Mwana kanga ndokose ye pweke maindoni  
Harusi chooni Howa**

Vile vile katika wimbo “maso maso”kuna fani ya kiutendi pale waimbaji hurudia baadhi ya sentensi katika ubeti.Kwa mfano katika sehemu hii “maso maso ee mwanangu asimwone.”

**Ayee maso maso ee mwanangu asimwone  
Maso maso ee mwanangu asimwone  
Maso maso ee mwanangu asimwone  
Jicho la hasidi ee mwenetu asimwone  
Jicho la hasidi ee mwenetu asimwone**

#### **4.1.4. Ishara za Mikono na Vidole**

Ishara za mikono hutumiwa kulitilia mkazo wazo au mawazo, dhana au ujumbe uliobebwa katika nyimbo. Washiriki hufungua na kufinyanga viganja vyao vyaa mkono kuonyesha umuhimu wa waimbaji kuongeza mwendo au kasi ya utendaji. Matumizi ya vidole huchukua sehemu kubwa sana katika kupidisha ujumbe kwa hadhira mionganini mwa jamii ya Waswahili na Wataveta. Katika jamii ya Waswahili hasa katika wimbo wa“tabanana hapa hapa” kuna fani ya kiutendi ya matumizi ya vidole pale ambapo waimbaji wanapofikia katika sehemu ya “ lala naye siku mbili na kwangu alale siku mbili.” Waimbaji huonyesha ishara ya mbili kwa vidole viwili.

**Mapenzi huipati raha nazijulia  
Penzi nampa lote yeye anafurahia  
Wewe hujui chochote  
Mimi ninavyosikia  
Na kupika si yako wazi  
Kibichi wampikia  
Ndio maana siku zote huja kwangu kujilia x2  
Tutabanana hapa hapa sote wa mume mmoja  
Lala naye siku mbili na kwangu alale mbili x2  
Siku moja Kizidisha cha moto utakiona x2**

Waimbaji hutoa ishara na kuangazia katika mtu wa kufikiria kwa kuinua kidole cha shahada juu kuonyesha nambari moja huku wakikitingisha na kutoa tahadhari ya kwamba akizidisha siku moja ataona cha moto. Kimsingi, mwimbaji anapitisha ujumbe kwa hadhira ya kwamba yejote atakayejaribu kuyaingilia mapenzi yake na mumewe basi atabaki kujilaumu mwenyewe baadae. Matumizi ya kidole cha kati mionganoni mwa wanawake wa Kiswahili ni jambo ambalo limethaminiwa sana. Kwa mfano kwa kutumia viganja vyao vya mkono waimbaji huweza kutoa ishara kwa kuviweka viganja vyao kifuanini na wafikapo sehemu hii “Habibu mimi niko”katika wimbo“paka mapepe”waimbaji hunyamaza kidogo kabla ya kuendelea na uimbaji. Hali hii hutoa msisitizo kwamba amemweka mume wake moyoni na hana nafasi ya mtu mwingine.

**Habibi mimi niko**

**Siku zote mi ni wako**

**Sitoe mtu kwako**

Katika wimbo “paka mapepe huyo” pia kuna fani ya kiutendi ya ishara ya vidole hasa waimbaji wanapofikia sehemu ya “tena kisha atapenya na baba atamtaka”. Waimbaji hutumia vidole vyao vya mkono wa kulia kuonyesha ishara ya jinsi msichana angewachanganya na hata namna angepenyeza kwa kufanya ishara za zigizagi au kombokombo kuonyesha kwenda kufanya mapenzi na baba.

**Nilikwisha kukanya**

**Huyo si wa kuridhisha**

**Leo atawachanganya**

**Mwana wa shangazi na paka**

**Tena kisha atapenya**

**Na baba atamtaka**

Matumizi ya kidole cha kati mionganoni mwa wanawake wa Uswahilini ni jambo ambalo haliwezi kupuuzwa. Kimsingi, matumizi haya yanatoa mwelekeo wa mambo yaliyofichwa. Kidole hiki hutumika katika kusuta au pale wanawake wanaposutana. Nyimbo hii huimbwa kuwasuta wanawake ambao hutoka nje ya ndoa zao na kufanya mapenzi kinyume na ndoa.

Katika jamii ya Wataveta kuna fani za kiutendi zinazohusiana na matumizi ya mikono karibu katika kila nyimbo ya harusi.Kwa mfano, katika wimbo wa ‘*hale kisamo*’kuna fani ya kiutendi pale wachezaji wanapotumia viganja vyao vya mikono kugusa sehemu zao za mapaja wakiviteremsha vidole vyao chini na kuvipandisha juu kwenye mapaja yao karibu na sehemu zao za siri huku wakipeleka vifua vyao mbele na nyuma hasa wakifikia katika sehemu hii “*hoyehoo,hale kisamo*”.

**Halee-e hale kisamo**  
**Halee-e hale kisamo**  
**Hoolele holele kisamo**  
**Heeee haleee hale kisamo.**  
**Funga Mburi wededewa kisamo, heee**  
**Hoyehoo, hale kisamo.**

### **TAFSIRI**

**Hoyee-e hoye burudani**  
**Hoyee-e hoye burudani**  
**Hooye hoyeho burudani**  
**Heeee hayee ndio burudani**  
**Ukifunga mbuzi unasengenywa burudani,hee**  
**Hooheyo ndio burudani**

Wachezaji wanakumbusha hadhira ya kwamba mbali na mambo mazuri yaliyofanywa na bibi harusi kama kukata nyasi lakini bado wanajamii hukaa kando na kumsengenya kwamba hajui kufanya vizuri.Ishara za mikono hutumiwa pia pale ambapo bibi harusi anapoingia langoni mwa nyumba ya bwana harusi ambapo hurushiwa mchele mweupe. Urushaji wa mchele mweupe hasa kwa bibi harusi na wale wote walioandamana naye wanapoingia langoni mwa nyumba ya bwana harusi huchukuliwa kama mbinu ya kuondoa mikosi na kuleta baraka katika nyumba. Kimsingi, wanajamii huamini ya kwamba kwa kufanya hivyo nyumba ingeweza kuwa na mali na amani kama vile mchele ulivyo mweupe.

#### **4.1.5. Minenguo ya Mwili**

Minenguo ya mwili huhuishwa na uchezaji pamoja na ishara ambazo hutendwa na wachezaji na watazamaji wakati wa utendaji. Fani ya kiutendi ya minenguo ya mwili ni njia mojawapo ambapo mchezaji wa nyimbo huweza kuwasilisha nia au hata hisia zake kupidia kwa maungo yake ya mwili au hata kimojawapo cha viungo vyake vikiwemo: makalio, kiuno, kichwa, mikono, na hata miguu. Viungo hivi huweza kusaidia katika kubainisha hali ya mtu ikiwa ana uchovu,aibu, kufishwa moyo, kutosheka, majigambo, mateso au kufanikiwa.

Lengo kuu la minenguo ya mwili kama fani ya kiutendi katika jamii ya Wataveta na Waswahili ni kuwasilisha nia au hata hisia kupidia kwa mojawapo ya viungo vyake vya mwili.Katika jamii ya Wataveta kuna fani ya kiutendi ya minenguo ya mwili katika wimbo “*Mwai Wetu Eohiyoo.*”

**Mwai wetu eohiyoo tumuenda tummbhone x2**  
**Mwai wetu eohiyoo tumuenda tummbhone x2**  
**Ambiere tummbhokeje tumuenda tummbhone**  
**Mawi wetu eohiyoo tumuenda tummbhone**  
**Na Bhammcheku tumbhokeje tumuenda tummbhone**  
**Mwai wetu eohiyoo tumuenda tummbhone**  
**Bha rumburie tummbhokeje tumuenda tummbhone**  
**Mwai wetu eohiyoo tumuenda tummbhone.**  
**Lubegho lwa mwana luwaaja x2**  
**Ahee luwaja x2**  
**Luwaja kamwe luheme x2**  
**Ahee luwaja x2**  
**Luwaja kangi ugure kikudiee**  
**Ahee luwaja**  
**Lubegho lwa mwana luwaja x2**  
**Ahee luwaja x2**  
**Luja kangi ugure ndenie x2**  
**Ahee luwaja x2**  
**Luwaja kangi usome sakaro**  
**Ahee luwaja**  
**Lubegho lwa mwana luwaja**

**Ahee luwaja**

**Luwaja kamwe luheme**

**Ahee luwaja**

**Wee luwaja kangi ugure muutwi**

**Ahee luwaja**

### **TAFSIRI**

**Bibi harusi wetu yuko wapi tunataka tumuone x2**

**Bibi harusi wetu yuko wapi tunataka tumuone x2**

**Kivyiire tumngoje tunataka tumuone**

**Bibi harusi wetu yuko wapi tunataka tumuone**

**Na kina mama tuwangoje tunataka tumuone**

**Bibi harusi wetu yuko wapi tunataka tumuone**

**Na ndugu zake tuwangoje tunataka tumuone**

**Bibi harusi wetu yuko wapi tunataka tumuone**

Huu ni wimbo ambao ulitoka kwa kabilia la Wapare kutoka Tanzania. Kama tulivyosema hapo awali ya kwamba kuna Wapare wengi ambao huishi Taveta kwa hiyo baadhi ya nyimbo kutoka Taveta utazipata Upareni na nyimbo kutoka Upareni ukazipata Taveta. Kila sherehe ya harusi mionganini mwa jamii ya Wataveta utaipata nyimbo hii ikiimbwa. Wanawake kutoka upande wa bwana harusi wanapofika nyumbani kwa mwanamwali hupokelewa na wenzao kwa nyimbo ambazo huimbwa kwa kusutana, kukomoana na baadae shughuli nzima kujaa shangwe na nderemo. Wanawake huweza kusukumana kwa mikono na kutumia sehemu zao za makalio kuwazuia wasichana upande wa bwanaharusi kutoingia ndani. Wakati mwingine sanduku huweza kupasuliwa na hata watu kuumizana. Kuna fani ya kiutendi ya minenguo ya mwili hasa katika wimbo *mwai wetu* ambao huimbwa na wasichana kutoka upande wa bibi harusi hasa wanapofikia katika sehemu *egura mutwi, egura ndeni*. Waimbaji wakifikia sehemu hii hushika kichwa kuonyesha uchungu unatokana na shughuli ya kujifungua mtoto. Katika wimbo wa *mwai wetu* kila ubeti unaoishia na “...*mauwa*” wanawake husukumana kwa kutumia makalio yao.

**Mwai wetu ee**

**Mwai wetu mauwa**

**Mwai wetu ee**

**Mwai wetu motomoto**

**Mwai wetu mauwa**

**Kiratu chake ee**

**Kiratu chake mauwa**

**Kiratu chake ee**

**Kiratu chake motomoto**

**Kiratu chake mauwa**

**Bibi harusi wetu ee**

**Bibi harusi wetu mauwa**

**Bibi harusi wetu ee**

**Bibi harusi wetu motomoto**

**Bibi harusi wetu mauwa**

**Kiatu chake ee**

**Kiatu chake mauwa**

**Kiatu chake motomoto**

**Kiatu chake mauwa**

Katika wimbo huu wanawake huweza kukabiliana na kuzozana kiasi cha kwamba huweza kuchaniana nguo. Harakati hizi huweza kuwa mbaya kiasi kwamba vazi la bibi harusi huweza kuraruliwa na wakati mwingine kusababisha kuhairisha kwa shughuli ya harusi.

Katika jamii ya Waswahili kuna fani ya kiutendi ya minenguo ya mwili hasa katika wimbo “maso maso mwanangu” ambapo wanawake huchezesha mabega na kunengua viuno huku wakiimba kwa mviringo. Katika mchezo huu wanawake wanapofikia katika sehemu hii ya “asema yuwapi ee mama harusi aje hapa tuhangaike naye” wanajaribu kuuliza mahali mama harusi alienda ili aje wahangaike naye katika harusi.

**Hongera mwanangu ee hongera x2**

**Nami ni mamaye hongera x2**

**Asema nami ni mamaye hongera x2**

**Sisi ni wazazi ee hongera**

**Asema hongera mwanangu ee hongera**

**Na mimi mamaye hongera**  
**Mwana wa uchungu wangu ee hongera**  
**Asema nami ni mamaye hongera**  
**Asema yuapi ee mama harusi**  
**Aje hapa tuhangaike naye.**

Kuna fani ya minenguo ya mwili katika wimbo wa Waswahili “Naupiga papapa Naupiga lololo”. Wimbo huu ni maarufu sana katika jamii hii na huimbwa katika hafla ya harusi katika jamii. Wimbo huu pia ulitumiwa na Timammy (2002) wakati akishughulikia nyimbo za harusi katika jamii ya Waswahili. Katika wimbo huu waimbaji huimba na kucheza huku wakielekeza vidole vyao katika sehemu ya mbele na nyuma ya miili yao. Kuna fani ya kiutendi ya minenguo ya mwili hasa waimbaji wanapofikia katika sehemu hii “Naupiga papapa naupiga lololo” ambapo huelekeza vidole vyao vya shahada katika sehemu zao za mbele na nyuma. Ishara hii huonyesha jinsi ambavyo mwanamke humridhisha mwanamume katika ngono.

**Naupiga papapa**  
**Naupiga lololo**  
**Ukitaka mumeo asitoke**  
**Akilala mguu mpachike**

#### **4.1.6 Maleba**

Kulingana na Mwenda Mbatia, (2001:41) anasema ya kwamba

maleba ni mavazi maalum yanayotumiwa na waimbaji  
kubunia taswira ya watu wanaowaimbia. Kwa mfano,  
waimbaji katika nyimbo za harusi kuvalia sare ili  
kuwatambulisha na wale watu wengine waliohudhuria.

Kwa hiyo tutambue ya kwamba kuna tofauti muhimu kati ya mavazi ya maisha ya kila siku na maleba katika utendaji wa nyimbo za harusi. Maleba huwasilisha ujumbe sawa na ule wa mavazi ya kawaida kwa kuzingatia jinsia, nafasi na jukumu. Kabla ya matumizi ya nguo kutoka katika mataifa ya Kimagharibi jamii ya Wataveta ilikuwa ikitumia ngozi iliyoshonwa vizuri na ilitumiwa kama vazi na hata katika harusi vazi hili hupambwa na kuwa la kufana sana kulingana na sherehe husika.

Wamitila, K.W. (2011) anasema ya kwamba maleba ni mojawapo ya vipengele muhimu vya mandhari. Maleba yanayotumiwa na wahusika wa kazi za kifasihi yana mchango mkubwa kwenye athari ya tamthilia nzima. Maleba haya huweza kuakisi kipindi cha kihistoria pamoja na hali iliyokizunguka kipindi hicho.Uteuzi wa maleba hudhibitiwa na nia ya kutaka kuzua athari fulani. Maleba pamoja na mafigu au vinyago vya wahusika huweza kutumiwa kuwapa wahusika sifa ambazo sio za kibinadamu hivyo basi kufanikisha utendaji.

Wilson (1998:387) anasema kuwa kwa sababu maleba yanavaliwa kiuhalisia na waigizaji, maleba ndicho kipengele cha kipekee cha vitu vionekanavyo katika jukwaa.Vile vile maleba yana thamani ya kipekee. Huongeza kipima rangi, umbo msokotano na uashiriaji kwa athari nzima. Maleba yana uhusiano wa karibu na vifuasi kama vile vipodozi, mapambo ya mwili kama vile mikufu na bangili, mitindo ya nywele, mafigu na nywele bandia. Maleba yana uwezo wa kuwasilisha ujumbe mzito kwa hadhira fauka ya kupendeza. Kwa mujibu wa Aston na Savona (1991) maleba hubainisha picha halisi ya mhusika na kuashiria kufanana au kutofanana. Maleba pia hutofautisha kati ya wahusika wa kike na wa kiume.

Mavazi ni mojawapo ya fani za kiutendi ambazo hutumiwa zaidi katika uimbaji wa nyimbo za harusi na katika sherehe mbalimbali za kitamaduni. Kwa mfano, katika jamii ya Wataveta maleba hutumiwa na wanawake na wanaume ambao huvalaa vazi ambalo lina rangi ya kufanana yaani *marikano* hasa katika uchezaji wa *Urwasi* ambao hufanywa karibu katika kila sherehe. Katika jamii ya Waswahili wanawake na wanaume hutofautiana katika matumizi ya maleba kwa sababu uchezaji wa nyimbo za harusi humiliwa na wanawake. Hadhi au uwezo wa mtu waweza kubainishwa na aina ya mavazi ambayo mtu huvalia. Isitoshe mavazi pia yaweza kubainisha tamaduni, kiwango cha imani na hata jinsia ya mtu.

Katika jamii ya Waswahili matumizi ya leso yalitumika karibu katika kila hafla ya sherehe. Leso hufungwa kiunoni hasa sehemu za makalio hasa wakati wanawake wanapoimba na kucheza. Leso inapofungwa kiunoni husaidia katika kuonyesha bayana jinsi makalio yanavyocheza na kutibwirika. Ikumbukwe ya kwamba kuna wanawake ambao huimba wakiwa wameketi huku wakipiga makofi na wengine wakiwa wamesimama huku wakiimba kwa kuzunguka katika mviringo mbele ya hadhira. Wanawake ambao wamesimama hufunga viuno vyao kwa leso ambazo

huonyesha jinsi makalio yao yanavyochezeshwa kufuatia mdundo wa nyimbo.Kwa mfano kuna fani ya kiutendi ya maleba katika wimbo “Naupiga papapa naupiga lololo”ambapo wachezaji wanapofikia sehemu hii hunenguwa viuno vyao kuonyesha jinsi ambavyo wangeweza kuwafurahisha waume wao katika kujamiana.

Katika jamii ya Wataveta kuna fani ya kiutendi ya maleba katika uimbaji wa nyimbo zote za harusi. Wanaume na wanawake hujifunga shuka zenyе rangi ya babu mzee. Wanawake hujifunga kuanzia sehemu ya kifuani ilihali wanaume hujifunga kuanzia sehemu za mabegani.

Wachezaji hasa wanawake wanapofikia katika sehemu hii *waibhaa ngwaru* vazi hili husaidia katika kuchezesha sehemu ya mbele ya kifua. Zamani vazi leusi ndilo lililotumiwa sana na liliweza kulainishwa ili kuwa laini kwa kutumia mafuta ya ng’ombe yaliyojulikana kama *ngorino* ili kulifanya vazi hili liweze kumeremeta.Kwa sababu ya mwingiliano na makabila mengine hasa Wakakhe vazi hili limegeuka kutoka vazi la rangi nyeusi hadi kuwa vazi la rangi ya damu ya mzee yaani maruni.

#### **4.1.7 Vigelegele**

Katika jamii ya Waswahili na Wataveta fani ya kiutendi ya vigelegele huchukuwa nafasi kubwa mno katika nyimbo za harusi. Katika utaratibu wote wa kuo katika jamii ya Waswahili na Wataveta vigelegele hupigwa na lengo kuu huwa ni kuonyesha furaha ya kwamba shughuli fulani iliyokusudiwa imekubalika na mvulana ameweza kupata mwanamke ambaye angeendeleza familia yao.

Katika jamii ya Wataveta fani ya kiutendi ya vigelegele hutumiwa katika hali ya kuonyesha furaha vile vile hutumiwa katika kufahamisha watu ya kwamba jambo fulani lilokuwa likiendelea liliweza kukamilika.Kwa mfano, kuna fani ya kiutendi katika wimbo *lishenenete saa mshamba wa igonji* hasa waimbaji wanapofikia sehemu hii *saa mshamba wa igonji*. Wachezaji hupiga vigelegele vya kuonyesha furaha yao kwa kumpata bibi harusi ambaye ni mrembo.

**Bhangasu bhoze bheshenenete x2**  
**Saa mshamba wa igonji**  
**Lanye bhome bheshenenete**  
**Saa mshamba wa igonji**

**Bhakara bhave bheshenenete x2**

**Saa mshamba wa igonji x2**

**Lanye namsema bheshenenete**

**Saa mshamba wa igonji**

Katika jamii ya Waswahili vigelegele pia huchukua sehemu kubwa kuonyesha furaha katika mchakato mzima wa taratibu za harusi. Karibu nyimbo zote za harusi huandamana na fani za kiutendi ya vigelegele. Kwa mfano, katika wimbo “maso maso” kuna fani ya kiutendi ambapo waimbaji wanapofikia katika sehemu hii “aje hapa”waimbaji hupiga vigelegele kufurahia harusi na kufurahi na mamake biharusi na pia kuzidisha furaha na shamrashamra za harusi.

**Mwana wa uchungu wangu ee hongera**

**Asema nami ni mamaye hongera**

**Asema yuapi ee mama harusi**

**Aje hapa tuhangaike naye**

**Yuwapi ee yuwapi mama harusi aje tuhangaike naye**

**Asema jamani ee yuwapi bibi harusi tuhangaike naye**

**Aje hapa**

**Tuhangaike naye**

**Ohoo aje hapa**

Fani ya kiutendi ya vigelegele katika jamii ya Waswahili hupigwa hususan kwa kufurahia kupokea kwa uposo, katika sherehe ya kupokea begi, wakati wa kupiga goma, wakati wa nikaha ikisha fungishwa na wakati ambao wanajamii wanapofurahia jambo muhimu katika jamii.Fani ya kiutendi ya upigaji wa vigelegele ina umuhimu uliolingana katika jamii ya Waswahili na Wataveta .Vigelegele katika jamii hizi mbili hupigwa kwa njia ambayo inafanana na yote hupitisha jumbe za furaha.

#### **4.2.0. Hitimisho**

Dhana ya fani za kiutendi katika nyimbo za harusi mionganoni mwa jamii ya Waswahili na Wataveta ni kigezo muhimu cha kupitisha ujumbe kwa hadhira. Mara kwa mara kauli tendi hizi hubeba ujumbe fiche na wakati mwingine mambo ambayo yasingeweza kutamkwa kwa mazungumzo basi njia mujarabu inayotumiwa ni fani za kiutendi.

Hata hivyo ishara za vidole na minenguo ya mwili ndiyo hutawala kauli tendi katika jamii ya Waswahili kwa jumla. Hata hivyo jamii ya Wataveta wanazo kauli tendi ambazo ni pamoja na minenguo, matumizi ya mikono na vidole. Fani za kiutendi kama vile maleba, uso-ishara, minenguo ya mwili, vigelegele, kimya na mtuo na kiti kati nyimbo za harusi mionganoni mwa jamii ya Waswahili na Wataveta ni nyenzo muhimu sana katika kuleta hali ya utendaji na ufaafu katika nyimbo.

## **SURA YA TANO**

### **MUHTASARI WA UTAFITI, CHANGAMOTO NA MAPENDEKEZO**

#### **5.0 Utangulizi**

Katika utafiti huu, tulikuwa na malengo ya kulinganisha fani za kiutendi katika nyimbo za harusi mionganoni mwa jamii za Wataveta na Waswahili. Dhamira yetu katika sura hii ni kutoa majumuisho juu ya mchakato wa zoezi zima la utafiti liliivoendeshwa. Tumeweza kujadili nadharia tete zetu pamoja na kuangazia matatizo ya utafiti wetu. Pia tumetoa muhtasari, hitimisho na mapendekezo ambayo yatasaidia watafiti wengine katika kufanya tafiti zao.

#### **5.1.0 Muhtasari wa Utafiti**

Kusudi kuu la utafiti wetu lilihusu ulinganishaji wa fani za kiutendi katika nyimbo za harusi za Waswahili na Wataveta. Kimsingi, utafiti huu umefanikiwa kujibu nadharia tete zilizoorodheshwa. Ingawa utanze wa nyimbo umeshughulikiwa na wasomi wengi swala la ulinganishaji wa fani za kiutendi katika nyimbo za harusi za Waswahili na Wataveta halijashughulikiwa.

Sura ya kwanza ya utafiti ilishughulikia utangulizi, tatizo, malengo, sababu, nadharia tete, upeo na mipaka, misingi ya nadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada, wanaozungumzia nyimbo kwa ujumla, yaliyoandikwa kuhusu utendaji, njia za utafiti na uchanganuzi wa data. Sura hii ilikuwa uti wa mgongo wa kazi yetu.

Katika sura ya pili na ya tatu tumeshughulikia utaratibu wa kuo na nyimbo zinazohusika katika jamii ya Wataveta na Waswahili. Nyimbo tulizozikusanya kwa ajili ya utafiti huu ni za kiasili tano (5) za Waswahili na tano (5) za Wataveta. Utaratibu huu ni sehemu muhimu mno katika jamii na hutoa taswira ya utamaduni husika. Hivyo basi tukiutumia utaratibu huu tunaweza kusawiri mila, miiko na utamaduni wa jamii katika ujumla wake. Utaratibu huu unaweza kutumiwa katika kuitambulisha jamii, kuhifadhi mila na tamaduni za jamii. Katika sura ya nne tulilinganisha fani za kiutendi katika nyimbo mionganoni mwa jamii za Waswahili na Wataveta. Tumegundua ya kwamba kuna fani za kiutendi katika nyimbo za harusi za Wataveta na Waswahili zilizolingana. Pia tumegundua ya kwamba kuna fani za kiutendi ambazo hazifanani.

Nadharia tete zetu zilikuwa mbili. Nadharia tete ya kwanza ilihusu kauli kwamba fani za kiutendi ni za aina mbalimbali katika jamii ya Wataveta na ile ya Waswahili. Hili limebainika ni kweli kwamba fani za kiutendi ni za aina mbalimbali. Nadharia tete ya pili ni kwamba fani za kiutendi zina uhusiano kati ya jamii ya Wataveta na ile ya Waswahili. Kulingana na utafiti tuliofanya hili limedhihirika kuwa na ukweli kwamba kuna uhusiano unaojitokeza katika fani za kiutendi katika nyimbo za jamii hizi mbili zina ulingano kama vile vigelegele, minenguo ya mwili, kiiitikio, kunyamza kimya na ishara za uso isipokuwa kuna fani za kiutendi ambazo zinatofautiana kama vile maleba na matumizi ya vidole na mikono katika jamii hizi.

### **5.1.1. Changamoto Tulizokumbana Nazo Katika Utafiti Wetu**

Utafiti huu ulifanywa maktabani na nyanjani. Sampuli yetu ilikuwa sampuli lengwa. Ukosefu wa fedha za kuwezesha usafiri hadi sehemu ambayo ni chimbuko la data lilikuwa tatizo. Iilitubidi kutembelea maeneo mbalimbali katika kaunti ndogo ya Taveta na Kaunti ya Mombasa. Sherehe za harusi katika tamaduni za Waswahili haziruhusu wanaume kuhudhuria hali ambayo ilikuwa ngumu kwetu kupata data tulizokusudia. Hivyo basi kupelekea kupata changamoto kubwa katika uchanganuzi wa fani za kiutendi katika nyimbo za harusi. Nyimbo tulizozikusanya zilikuwa nyingi na za aina mbalimbali. Iilitulazimu kuzichuja ili kupata zile zilizotufaa katika utafiti wetu.

Katika eneo la Kimorigo wahojiwa walidhani ya kwamba mtafiti alikuwa anakusanya aina za nyimbo tu ili aweze kufanya biashara na kujitajirisha. Wakati mwingine mtafiti ilibidi kutumia pesa nyingi sana ili kuweza kuwashawishi baadhi ya walengwa kuhojiwa.

Mtafiti alikuwa na tatizo la kutafsiri nyimbo kutoka kwa lugha ya Kitaveta hadi ya Kiswahili. Kila alipofanya hivyo maana za nyimbo zilibadilika jambo ambalo lilipelekea nyimbo husika kutoimbika kwa kutumia mahadhi ya Kitaveta. Changamoto ambazo tumezitaja ni baadhi tu ya changamoto tulizokumbana nazo katika utafiti. Licha ya changamoto hizo tuliweza kukusanya data iliyotufaa katika utafiti wetu.

### **5.1.2 Mapendekezo**

Malengo ya utafiti wowote ni kutambua mwanya ambao unahitajika kuzibwa na watafiti wa baadaye. Matokeo ya utafiti huu yalihusu jamii ya Wataveta na jamii ya Waswahili wa Mombasa. Tungependekeza ya kwamba utafiti ufanywe katika sehemu nyingine ya jamii hizi kama vile Waswahili wa Lamu au Wataveta wa Challal. Tungependekeza vile vile kwamba utafiti huu uwachochee wasomi wa fasihi simulizi hasa kutoka jamii ya Wataveta na Waswahili kufanya utafiti wa fani na muundo wa vipengee vya fasihi simulizi ili kuhakikisha kwamba fasihi simulizi ya Wataveta na Waswahili haifi na kusahaulika.

## MAREJELEO

- Abercrombie, D. (1968) *Paralangue. Journal of Disorders of communications.* British.
- Akivaga, S.K.& Odaga, A.B. (1982) *Oral Literature. A School Certificate Course.* EAEP. Nairobi.
- Alembi, E. (2002) *The Construction of the Abanyole Perceptions in Death Through Oral Funeral Poetry.* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Heisinki.
- Balisidya, M.L.(1987) *Tanzu za fasihi simulizi,Temu,C.W na Mbogo,* E. MULIKA NO.19 TUKI.
- Bauman, R (1992) *Performance katika Folklore, Cultural Performance and Popular Entertainments.* Oxford University Press, New York
- Beeman, W. (1997) *Performance Theoryinan Anthropology Program.* Katika <<http://www.brown.edu/Departments/Anthropology/Publications>.
- Beja, S.K. (2000) *Giriama Funeral Songs a Functional Aesthetic Study.* Tasnifu ya PhD Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa).
- Brown, P. NA Levinson, S. (1978) *Pragmatics:* Cambridge University Press. London.
- Bukenya, A. (1990) *Oral Literature for Schools.A Senior Course.* Longhorn Publishers, Nairobi.
- Bukenya, A.S. et.al (2010) *Oral Literature.* Longhorn Publishers (K) Ltd, Nairobi.

- Fine, E. (1984) *The Folklore Text: From Performance to Print.* University Press, Bloomington. Indiana.
- Finnegan, R. (1977) *Oral Literature in Africa.* Oxford University Press. London.
- Finnegan, R. (1977) *Oral Poetry: Its Nature, Significance and Context.* Cambridge University Press. London
- \_\_\_\_\_ (1992) *Oral Poetry. Its nature, Significance and Social Contex.* University Press, Bloomington. Indiana.
- Foley, J. (1995) *The Singer of the Tales Performance.* University Press, Bloomington, Indiana.
- Greenville.F (1970) *African Language Studies A note on the Hamziyya Deciphered in.* VOL XII. London.
- Hardings,F (2003) *African Aspects in Carnival.The Art of Carnival.*Xpress and Arts Council of England.London
- Kabira, Wanjiku and Karega Mutahi (1988). *Gikuyu Oral Literature.* Heineman Nairobi.
- Kavuga, F.S. (1997) *Desturi na Mila za Wapare.*Vuga Press Soni.
- Kipury, N. (1983) *Oral Literature of the Maasai.* Heinmann, Nairobi.
- Kitsao, J. (1975) *A Stylistic Approach Adopted for the Study of Swahili Prose Texts.* Unpublished M.A. Thesis, University of Nairobi.

- Levison, C. Stephen. (1965) *Pragmatics*. Cambridge. Cambridge University Press. London.
- Malinowski.B. (1944) A Scientific Theory of Culture. Chapel Hill. University of North Carolina Press.
- Masebo J.A na Nyangwine, N (2007) *Nadharia ya Lugha ya Kiswahili*. Nyambari Nyangwine Publishers. Dar es Salaam.
- Massamba, D.P.B (2002) *Utunzi wa Ushairi wa Kiswahili katika makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili*. Fasihi ya Uchunguzi wa Kiswahili. Dar es Salaam.
- \_\_\_\_\_ et.al (1999) *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu*. Sekondari na Vyuo. TUKI. Dar es Salaam.
- Matti, N (1997) *Sanaa za Maonyesho za Kiafrika za Jadi*. *Mfano wa Tohara za Watharaka*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret.
- Mbatia, M. (2001) *Kamusi ya fasihi*. Standard Textbooks Graphics and Publishing Limited. Nairobi.
- Mbiti.J. (1991) *Introduction to African Religion*. East African Publishers, Nairobi.
- Mbogo, E.(1996) *Vipuli vyaya Figo*. East African Educational Publishers, Nairobi.
- \_\_\_\_\_ (1984) *Sundiata*. Lake Publishers & Enterprises. Kisumu.

- Mghanga J.D. (1984) *Fasihi Simulizi katika jamii ya Kidawida.* Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Miruka, O. (1994) *Encounter with Oral Literature.* East African Educational Publishers.Nairobi.
- \_\_\_\_\_ (2003) *Studying Oral Literature.* Acacia Publishers, Kenya. Nairobi.
- Mjomba, D.(2012) *Nyimbo za harusi mionganii mwa jamii ya Wadawida.* Tasnifu ya Shahada ya Uzamili Chuo Kikuu Cha Nairobi (Haujachapishwa)
- Momanyi.C. (2015) Historia Na Utamaduni wa Wataveta. CUEA.
- Mubima, O. (1997) *The Traditional African Poets of Oracy.* A paper presented at the 5<sup>th</sup> International Workshop on Orature. Nairobi.
- Mulokozi, M.M.(1989), *Fasihi ya Kiswahili.* Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania. Dar es salaam.
- \_\_\_\_\_ (1996) *Fasihi Simulizi Nyimbo za Kumbi.* TUKI. Dar es Salaam.
- \_\_\_\_\_ 2011) *Fasihi Simulizi, Nyimbo za Kumbi.* Tuki. Dar es salaam.
- Mwakasaka, C.S. (1977) *The Oral Literature of Banyakyusa.* University of Dar es Salaam.
- Nandwa, J. na Bukenya,A.(1990) *African Oral Literature for Schools.* Longman. Nairobi.
- Ngara, E(1985). Stylistic Criticism and the African Novel. Heinemann. London.

- Ngure.A. (2003) *Fasihi Simulizi kwa Shule za Sekondari.* Phoenix Publishers Limited. Nairobi.
- Njogu Kimani (2004). *Rearing Poetry As Dialogue.* The Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi.
- Njogu,K. & Rocha. C.(1999). Ufundishaji wa Fasihi.Nadharia na Mbinu. Jomo Kenyatta Foundation. Nairobi.
- Nkwera,F.R.(1998) *Tamrini za Fasihi Simulizi,Sekondari na Vyuo.* Business Printers Limited, Dar es salaam.
- \_\_\_\_\_ 1998), *Tamrini za Fasihi Simulizi.*Katika Makala ya Semina za Kitaifa ya Waandishi wa Kiswahili Fasihi,Chuo Kikuu TUKI.
- Okpewho, I. (1992) *African Literature. Backgrounds, Character and Continuity.* Bloomington, University Press. Indiana.
- Omar, C.K. and Mvungi,M.(1988) *Urithi wa Utamaduni Wetu.* Tanzania Publishing House, Dar-es-Salaam.
- Radcliffe, A.R. (1957) *A Natural Science of Society.* Glencoe, IL. Free Press
- Schechner, R. (1988) *Performance Theory.*Routledge.London.
- Senkoro, F.E.M.K. (1989) *Fasihi Andishi,* Kauttu Ltd. Dar es Salaam
- Sunkuli,L. &Miruka,A.(1990) *A Dictionary of Oral Literature.* EAEP, Nairobi.
- Syambo,K& A.Mazrui (1992) *Uchambuzi wa Fasihi.* East African Educational Publishers Nairobi.

- Timammy, R. (2002) *Swahili Women's Wedding Songs; A Stylistic Analysis*. Tasnifu ya PhD Chuo Kikuu Cha Nairobi.
- Tuki (2000) *English-Swahili Dictionary 1st edition*; Institute of Kiswahili Research. Dar-esalaam.
- Wamitila,K.W. (2004). *Kichocheo cha fasihi simulizi Na Andishi*. Focus Books. Nairobi.
- Were, G & Wandiba,S (1988) *Meru District Social-Cultural Profile*. Nairobi.
- Yule, G (1999). *Pragmatics*, Oxford University Press. London.

## **VIAMBATANISHO**

### **(i) NYIMBO ZA HARUSI ZA WATAVETA**

#### **1. MWAI WETU EOHIYOO**

**Mwai wetu eohiyoo tumuenda tummbhone x2**

**Mwai wetu eohiyoo tumuenda tummbhone x2**

**Ambiere tummbhokeje tumuenda tummbhone**

**Mwai wetu eohiyoo tumuenda tummbhone**

**Na bha Mcheku tummbhokeje tumuenda tummbhone**

**Mwai wetu eohiyoo tumuenda tummbhone**

**Na bhache nabho tummbhokeje tumuenda tummbhone**

**Mwai wetu eohiyoo tumuenda tummbhone**

**Wee bhana bhakundana sigheni bhauhane**

**Mwai wetu eohiyoo tumuenda tummbhone**

**Bha ii sanga bhehiyoo izooni tushahiree**

**Mwai wetu eohiyoo tumuenda tummbhone**

**Akuundae akuunda**

**Akundae akuunda**

**Ni weetu ee ni wetu**

**Ni wetu ee ni wetu**

**Atoonga mbwanyeni atoonga**

**Atoonga ee atoonga**

**Akuunda ee akuunda**

**Akuunda ee akuunda**

**Ni wetu ee harika ni wetu harika**

**Ni wetu ee ni wetu**

**Atonga hee atonga**

**Atonga hee atonga**

**Lubegho lwa mwana luwaaja x2**

**Ahee luwaja x2**

**Luwaja kamwe luheme x2**

**Ahee luwaja x2**

**Luwaja kangi ugure kikudiee**

**Ahee luwaja**

**Lubegho lwa mwana luwaja x2**

**Ahee luwaja x2**

**Luja kangi ugure ndenie x2**

**Ahee luwaja x2**

**Luwaja kangi usome sakaro**

**Ahee luwaja**

**Lubegho lwa mwana luwaja**

**Ahee luwaja**

**Luwaja kamwe luheme**

**Ahee luwaja**

**Wee luwaja kangi ugure muutwi**

**Ahee luwaja**

**Ngoma mbiri nyika ni mundu na mlamuye,**

**Eee bhae abha mfinanga**

**Ni wetu ee ni wetu x2**

**Akuunda ee akunda**

**Akuunda ee akunda**

**Atonga ee atonga**

**Atongae mbwanyeni atonga**

**Atonga ee atonga**

**Mwai wetu eohiyoo tumuenda tummbhone**

**Mwa wetu eohiyoo tumuenda tummbhone**

**Bha ambiere moohiho izoni mshaire**

**Mwai wetu eohiyoo tumuenda tummbhone**

**Bha mcheku moohiyoo izooni mshaire**  
**Mwai wetu eohiyoo tumuenda tummbhone**  
**Bha rumburia moohiyoo izooni mshaire**  
**Mwai wetu eohiyoo tumuenda tummbhone**  
**Wedi sa ndembe ja manna ee tumuenda tummbhone**  
**Mwai wetu eohiyoo tumuenda tummbhone**  
**Kangi ni mjewa sa ipapayu tumuenda tummbhone**  
**Mwai wetu eohiyoo tumuenda tummbhone**

**Akuunda ee akunda**  
**Akunda ee akunda**  
**Ni weetu ee ni weetu**  
**Ni weetu ee ni wetu**

**Atoonga harika atonga haya wee**  
**Atoonga ee atoonga**  
**Akuunda ee akuunda**  
**Akuunda ee akunda**

### **TAFSIRI YA KISWAHILI**

**Bibi harusi wetu yuko wapi tunataka tumwone**  
**Bibi harusi wetu yuko wapi tunataka tumwone**  
**Kivyere tumngojee tunataka tumwone**  
**Bibi harusi yuko wapi tunataka tumwone**

**Na kina mama tumngojee tunataka tumwone**  
**Bibi harusi wetu yuko wapi tunataka tumwone**  
**Na wanawake nao tuwangojee tunataka tumwone**  
**Bibi harusi wetu yuko wapi tunataka tumwone**

**Jamani watoto wamependana acheni waoane**  
**Bibi harusi wetu yuko wapi tunataka tumwone**  
**Na jamii iko wapi njooni tunataka tumwone**  
**Bibi harusi wetu yuko wapi tunataka tumwone**

**Amependa amependa**  
**Ni wetu ndio ni wetu**  
**Ni wetu ndio ni wetu**  
**Ameenda jamani ameenda**  
**Ameenda ameenda**  
**Amependa amependa**  
**Amependa amependa**

**Ni wetu jama ni wetu jama**  
**Ni wetu ndio ni wetu**  
**Ameenda ameenda**  
**Uchungu wa kujifungua huuma**  
**Ndio huuma**  
**Huuma mara moja utulie**  
**Ndio huuma**

**Huuma hata ushike kiuno**  
**Kweli huuma**  
**Uchungu wa kujifunguwa huuma**  
**Ndio huuma**  
**Huuma mpaka ushike tumbo**  
**Ndio huuma**  
**Huuma hata uweze kushika chini**  
**Ndio huuma**  
**Uchungu wa kujifunguwa huuma**  
**Ndio huuma**  
**Huuma mara moja utulie**  
**Ndio huuma**  
**Jamani huuma mpaka mtu ashike kichwa**  
**Ndio huuma**

**Watu wawili porini ni mtu na shemejiye**  
**Ndio hivyo eti Mfinanga**  
**Ni wetu kweli ni wetu**

**Amependa amependa**  
**Amependa amependa**  
**Ameenda ameenda**  
**Ameenda jamani ameenda**  
**Ameenda kweli ameenda**  
**Bibi harusi yuko wapi tunataka tumuone**  
**Bibi harusi yuko wapi tunataka tumuone**  
**Kina vivyere mko wapi mshangilie**  
**Bibi harusi yuko wapi tunataka tumuone**  
**Kina mama wako wapi waje washangilie**  
**Bibi harusi yuko wapi tunataka tumuone**  
**Ndugu zake wako wapi njooni tumshangilie**  
**Bibi harusi yuko wapi tunataka tumuone**  
**Bibi harusi ni mzuri kama tembe ya mzabibu**  
**Bibi harusi yuko wapi tunataka tumuone**  
**Hata mweupe kama papai tunataka tumuone**  
**Bibi harusi yuko wapi tunataka tumuone**

**Amependa ee amependa**  
**Ni wetu ni wetu**  
**Ni wetu ni wetu**  
**Ameenda jama ameenda ameenda haya wee**  
**Ameenda ee ameenda**  
**Amependa ee amependa**

## **2. MWAI ESHENENETE**

**Isanga loosee,lisheneneete x2**  
**Isanga loosee,lisheneneete x2**  
**Lanye bhome,lishenenete**  
**Saa mshamba wa igonji**  
  
**Bhangasu bhome bheshenenete x2**  
**Saa mshamba wa igonji**  
**Lanye bhome bheshenenete**  
**Saa mshamba wa igonji**

**Bhakara bhoze bheshenenete x2**

**Saa mshamba wa igonji x2**

**Lanye namsema bheshenenete**

**Saa mshamba wa igonji**

**Bhaiya bhoze bheshenenete x2**

**Saa mshamba wa igonji x2**

**Woowi bheshenenete**

**Saa mshamba wa igonji**

**Bhabora bhoze bheshenenete x2**

**Saa mshamba wa igonji x2**

**Lanye bhome bheshenenete**

**Saa mshamba wa igonji**

**Bharisha bhoze bheshenenete**

**Saa mshamba wa igonji**

**Ni kididi bheshenenete**

**Saa mshamba waigonji**

**Bhaghosi bhoze bheshenenete**

**Saa mshamba wa igonji**

**Lanye bhome bheshenenete**

**Saa mshamba wa igonji**

**Bhamanyi bhoze bheshenenete**

**Saa mshamba wa igonji**

**Lanye bhome bheshenenete**

**Saa mshamba wa igonji.**

**Teri yetu ishenenete**

**Saa mshamba wa igonji**

**Wuui ishenenete**

**Saa mshamba wa igonji**

## **TAFSIRI YA KISWAHILI**

**Jamii yote inameremeta**

**Jamii yote inameremeta**

**Jameni jama inameremeta**

**Kama mkia wa kondoo**

**Wanawali wote wanameremeta wote wanameremeta**

**Kama mkia wa kondoo**

**Jamani jama wanameremeta**

**Kama mkia wa kondoo**

**Wasimamizi wote wa harusi wanameremeta**

**Kama mkia wa kondoo**

**Jamani naomba wanameremeta**

**Kama mkia wa kondoo**

**Kina mama wote wanameremeta**

**Kama mkia wa kondoo**

**Jama wanameremeta**

**Kama mkia wa kondoo**

**Wasichana wote wanameremeta**

**Kama mkia wa kondoo**

**Jamani jama Wanameremeta**

**Kama mkia wa kondoo**

**Wachungaji wote wanameremeta**

**Kama mkia wa kondoo**

**Ni kweli wanameremeta**

**Kama mkia wa kondoo**

**Wa Mnene wana meremeta**

**Kama mkia wa kondoo**

**Jamani jama wanameremeta**

**Kama mkia wa kondoo**

**Ardhi yetu inameremeta**  
**Kama mkia wa kondoo**  
**Jamani wote wanameremeta**  
**Kama mkia wa kondoo**

### **3. MALA MAGHERI MAREFIKA**

**Mala magheri ee iyo maringana**  
**Kutonga natonga ee iyo kureyoa**  
**Kureyoa wikuji ee too na wikenya**  
**Hala wikikua yoo niwotoka**

**Mama nakushigha mwenye eetoe**  
**Natonga lanye etoe kureyowa**  
**Bhaa mndwetu eetoe natonga**  
**Bhaa mndwetu natonga yoo kureyowa**

**Bhala bharela ng'ombe ngwa**  
**Bhachike kinugu eeh saa ighembe**  
**Ighembe lishonwa yoo**  
**Ighembe lishonwa eto ni mshana**

**Mshana mangeri eetoo arufure**  
**Aachiku kinugu etoo sa ighembe**  
**Mala magheri ee iyo mrefika**

**Iya na papa eetoo twaaghana**  
**Iya wangu etoo twaaghana**  
**Ekubaiya lukwi etoo ni ani**

**Iya wangu eto nakushigha**  
**Ekutongia ngondeni eto ni wakweani**  
**Hee iya wangu eto nakushigha**  
**Ekuetic idio etoo ni wakweani**

**Nafika kichini eto kureyowa**  
**Nirepimiwa kijo eto na madio**  
**Hee, nitara etoo bwasi bwangu**  
**Hee, niketeze bhome bwasi bwangu**

**Ekuwura tauni eto papa ni wakweani**  
**Hee natonga kichini eto kureyoa**  
**Reguree ngoo eto ikubhure tauni eto ee**  
**Hee iya wangu eto twaaghana**

**Ekuhaghia iyanda eto niwakweani ee**  
**Nashigha hetu heteka ee hee**  
**Natonga kurekija hengi iya ee hee**  
**Natikwa kichini etoo kureyowa**

**Papa wangu etoo twaaghana**  
**Hee ekukezia etoo ni wakweani**  
**Kana ekubighia kibulu eto ni wakweani**  
**Natikwa kichini etoo kureyowa**

**Eee mala magheri etoo marefika**  
**Hee irika letu etoo twaaghana**  
**Nineseka na ani etoo wasiwi bwangu**  
**Hee natikwa kichini etoo kureyowa**

**Jila ndamwena chetu ee chatera**  
**Nashighwa mkibha etoo bhwasi bhwangu**  
**Mwikae nenzu ee kiboheni**  
**Hee, natikwa kichini etoo kureyowa**

## **TAFSIRI KWA KISWAHILI**

**Ile siku jamani imefika**

**Kwenda naenda jamani kuangalia**

**Kuangalia iliyokomaa na mbichi**

**Ili isiyokomaa niweze kurudi**

**Ndugu zangu nimenda**

**Ndugu zangu nimenda leo kutazama**

**Wale waliokula ng'ombe wa watu**

**Wakatike katikati kama mpini wa jembe**

**Siku jamani imefika**

**Mama na baba jamani twaagana**

**Mama yangu jamani twaagana**

**Atakayekuvunjia kuni jamani ni nani**

**Mamangu jamani nakuacha**

**Atakayekwenda shambani jamani ni nani**

**Hee mama yangu jamani nakuacha**

**Atakaekuletea ndizi jamani ni nani**

**Naenda ubayani jamani kutazama**

**Nitapimiwa chakula jamani tabu zangu**

**Hee nitahesabiwa jamani hata na ndizi**

**Hee nifanye nini tabu zangu**

**Atakayekwambia pole ukitoka kusaga ni nani**

**Hee naenda ubayani jamani kuangalia**

**Ukashike tumbiri akuambie pole jamani**

**Hee, mama yangu jamani twaagana**

**Atakaye kufagilia nyumba ni nani**

**Naacha kwetu kukipotea jamani ee**

**Naenda kujenga kwingine jamani ee hee**

**Napelekwa kubaya jamani kuangalia**

**Baba yangu jamani twaagana**  
**Yule atakayekukusalimia ni nani**  
**Ama atakayekukutengenezea uji ni nani**  
**Hee nimepelekwa ubayani jamani kuangalia**

**Ehee kumbe ile siku jamani imefika**  
**Hee rika letu jamani tunaagana**  
**Nitacheza na nani jamani tabu zangu**  
**Hee nimepelekwa ubayani jamani kutazama**

**Napelekwa ubayani jamani kuangalia**  
**Ile michezo yetu sasa imehairishwa**  
**Nimeachwa masikini jamani tabu zangu**

### **3. MWAI WETU**

**Mwai wetu ee**  
**Mwai wetu mauwa**  
**Mwai wetu ee**  
**Mwai wetu motomoto**  
**Mwai wetu mauwa**

**Kiratu chake ee**  
**Kiratu chake mauwa**  
**Kiratu chake ee**  
**Kiratu chake motomoto**  
**Kiratu chake mauwa**

**Suka yake ee**  
**Suke yake mauwa**  
**Suke yake ee**  
**Suke yake motomoto**  
**Suke yake mauwa**

**Ndondo yetu ee**  
**Ndondo yetu mauwa**  
**Ndondo yetu ee**  
**Ndondo yetu motomoto**  
**Ndondo yetu mauwa**

**Ifundi letu ee**  
**Ifundi letu mauwa**  
**Ifundi letuee**  
**Ifundi letu motomoto**  
**Ifundi letu mauwa**

### **TAFSIRI**

**Bibi harusi wetu ee**  
**Bibi harusi wetu mauwa**  
**Bibiharusi wetu ee**  
**Bibi harusi wetu moto moto**  
**Bibi harusi wetu mauwa**

**Kiatu chake ee**  
**Kiatu chake mauwa**  
**Kiatu chake ee**  
**Kiatu chake moto moto**  
**Kiatu chake mauwa**

**Nguo yake ee**  
**Nguo yake mauwa**  
**Nguo yake ee**  
**Nguo yake moto moto**  
**Nguo yake mauwa**

**Nyota yetu ee**  
**Nyota yetu mauwa**  
**Nyota yetu ee**

**Nyota yetu moto moto**  
**Nyota yetu mauwa**  
**Mrembo wetu ee**  
**Mrembo wetu mauwa**  
**Mrembo wetu ee**  
**Mrembo wetu moto moto**  
**Mrembo wetu mauwa**

#### **4. HALEE-E HALE KISAMO**

**Halee-e hale kisamo**  
**Halee-e hale kisamo**  
**Hoolele holele kisamo**  
**Heee haleee hale kisamo.**

**Funga Mburi wededewa kisamo, heee**  
**Hoyehoo, hale kisamo.**

**Makurukuru Masinde kisamo, hee**  
**Hoyehoo, hale kisamo.**

**Mfurunganje ruruma kisamo,hee**  
**Hoyehoo, hale kisamo.**

**Mwari wetu etonga ededwa kisamo,hee**  
**Hoyehoo, hale kisamo.**

**Mtongorito shombeni kisamo, hee**  
**Hoyehoo, hale kisamo**  
**Kwanyika wandu kwarighia kisamo,hee**  
**Hoyehoo, hale kisamo.**  
**Endamara, wededewa kisamo,hee**  
**Hoyehoo, hale kisamo.**

**Irika langu natonga kisamo,hee  
Hoyehoo, hale kisamo.**

**Wakora nyungu, shidongu kisamo,hee  
Hoyehoo, hale kisamo.**

**Funga mburi walia kisamo,hee  
Hoo hoyehoo, hale kisamo.**

**Hake Metinyoki ni rungu ya chuma,hee  
Hoyeo, hale kisamo.**

**Hake Lesareyo ni rungu ya mwingo,hee  
Hoyeo, hale kisamo.**

#### **TAFSIRI**

**Hoyee-e hoye burudani  
Hoyee-e hoye burudani  
Hooye hoyeho burudani  
Heee hayee ndio burudani**

**Ukifunga mbuzi unasengenywa burudani,hee  
Hooheyo ndio burudani**

**Kukurukakara furahia burudani,hee  
Hooheyo ndio burudani**

**Mvule nguruma burudani,hee  
Hooheyo ndio burudani**

**Bibi harusi wetu anatembea akisengenywa burudani,hee  
Hooheyo ndio burudani**

**Bwana harusi ugenini burudani,hee**

**Hooheyo ndio burudani**

**Watu wametawala burudani,hee**

**Hooheyo ndio burudani**

**Unapika huku wasengenywa burudani,hee**

**Hooheyo ndio burudani**

**Rika langu limekwenda burudani,hee**

**Hooheyo ndio burudani**

**Wasafisha chungu, watukanwa burudani,hee**

**Hooheyo ndio burudani**

**Unafunga mbuzi ukilia burudani,hee**

**Hooheyo ndio burudani**

**Kwa Metinyoki ni rungu la chuma,hee**

**Hooheyo ndio burudani**

**Kwa Lesareyo ni rungu la mti wa mpingo,hee**

**Hooheyo ndio burudani**

## **(ii) NYIMBO ZA WASWAHILI**

### **1.0 PAKA MAPEPE**

**Paka mapepe huyoox6**

**Paka mapepe usimwandame**

**Usiache akuchunge**

**Paka mapepe**

**Huyo hamjui mume**

**Paka mapepe huyo**

**Ukifika kwake gume**

**Paka mapepe huyo**

**Paka mapepe usimwandame**

**Paka mapepe huyo**

**Usiache akuchunge**

**Paka mapepe huyo**

**Huyo hamjui mume**

**Paka mapepe huyo**

**Ukifika kwake dume**

**Paka mapepe huyo**

**Akipenda msukume x2**

**Tena sikusalimu**

**Mkomeshe akukome**

**Atabaki alalame**

**Habibi mimi niko**

**Siku zote mi ni wako**

**Sitoe mtu kwako**

**Fanya ufanyavyo fanya**

**Umweke umwekavyo**

**Nilikwisha kukanya**

**Huyo si wa kuridhisha**

**Leo atawachanganya**  
**Mwana wa shangazi na paka**  
**Tena kisha atapenya**  
**Na baba atamtaka**

**Atafanya lakufanya**  
**Mwisho atakasirika-aa**  
**Hafai huyo hafai**  
**Kwangu mimi nifurahi**

**Paka huyo paka**  
**Paka mapepe**  
**Umpe kuku na bata**  
**Bure hatosheki**

**Umpe japo siteki huyo paka**  
**Hatakushukuru huyo paka**  
**Atakutoroka huyo paka**  
**Akimwona panya huyo paka**

**Kila mtendeavyo**  
**Bado atalalamika**  
**Wivi kwa kila njia**  
**Mwisho atakutoroka**  
**Bure kumkubali**  
**Kufanya anavyotaka-aa**  
**Hafai huyo hafai x2**  
**Kwangu mimi mfurahi**  
**Paka huyo paka**  
**Paka mapepe paka**  
**Uuze kuku na bata**  
**Hawezi kutosheka**

## **2.0 TUTABANANA HAPA HAPA**

**Mapenzi huipati raha nazijulia**

**Penzi nampa lote ye ye ana furahia**

**Wewe hujui chochote**

**Mimi ninavyosikia**

**Na kupika si yako kazi**

**Kibichi wampikia**

**Ndio maana siku zote huja kwangu kujilia x2**

**Twabanana hapa hapa sote wa mume mmoja**

**Lala naye siku mbili na kwangu alale mbili x2**

**Siku moja kizidisha cha moto utakiona x2**

**Ni hapa hapa si banduki ubavuni x2**

**Nakukumbasha umbea kutuma watu nyumbani x2**

**Kuja kwangu kuchunguza nakula mlo gani**

**Pia wataka kujua navaa viwalo gani**

**Mume hubajeti sawa wivu na choyo cha nini**

**Hakuna cha peke yako hususa hapa mjini**

**Kugawana na wenzako siku hizi ni fesheni**

**Tutabanana hapa hapa hunipiku asilani**

**BBC ni jiwe juu kama moto wa kivuu**

**Msisumbue cheo chetu ni kimoja**

**Tabananana hapa kwa mwanamume mmoja x2**

**Sote tule kwa pamoja x2**

**Ndani ni matusi ugomvi na mabishano**

**Kama wewe ni mkewe mimi pia keshanioa**

**Ndani ni masama twaweza kujuliana**

**Kama wewe ni wa nyumba kubwa mimi ni wa nyumba ndogo**

**Tutabanana hapa hapa niko na wewe beneti**

**Tutabanana hapa hapa niko na wewe sikuachilii**

**Na ukizubaa**

**Niko hapa hapa**

**Ukirejea**

**Nje nakutupa**

**Usijitie kibuhuti tunakula pleti moja**

**Wachonga kwa tahastiti twacheza raundi moja**

**Mimi ndio supa binti ananipenda zaidi**

**Talaka mimi sipewi kama kupewa ni wewe**

**Ahaa kazi kwako nina hisa kwake x2**

**Ayee ananipenda miye**

**Ayee natamba naye**

**Ayee natanua naye**

**Ayee nakula naye**

**Ayee nacheza naye**

**Ayee nacheza rumba**

### **3. MASO MASO**

**Ayee maso maso ee mwanangu asimwone**

**Maso maso ee mwanangu asimwone x2**

**Jicho la hasidi ee mwenetu asimwone x2**

**Maso maso ee mwanangu asimwone**

**Ayee maso maso ee mwanasimwone**

**Mwanangu asimwone**

**Maso maso ee mwanangu asimwone**  
**Jicho la hasidi ee mwenetu asimwone**  
**Maso maso ee mwanangu asimwone**

**Wala la mbaya wetu ee mwanangu asimwone**

**Masoooo**  
**Mwanangu asimwone**  
**Masooo ee**  
**Mwanangu asimwone**  
**Eee masooo mwanangu**  
**Mwanangu asimwone**

**Hongera mwanangu ee hongera x2**

**Nami ni mamaye hongera x2**  
**Asema name ni mamaye hongera x2**  
**Sisi ni wazazi ee hongera**  
**Asema hongera mwanangu ee hongera**  
**Na mimi mamaye hongera**

**Mwana wa uchungu wangu ee hongera**  
**Asema nami ni mamaye hongera**  
**Asema yuapi ee mama harusi**  
**Aje hapa tuhangaike naye**

**Yuwapi ee yuwapi mama harusi aje tuhangaike naye**  
**Asema jamani ee yuwapi bibi harusi tuhangaike naye**  
**Aje hapa**  
**Tuhangaike naye**  
**Ohoo aje hapa**

**Kina mama harusi waje hapa tuhangaike naye**  
**Tuhangaike naye**

**Dadake harusi naye yuko wapi aje hapa tuhangaike naye**

**Tuhangaike naye**

**Bibi harusi naye yuko wapi aje hapa tuhangaike naye**

**Tuhangaike naye**

**Somo yake bibi harusi aje tumfunze mwari asiende kufedheheka**

**Ukiitwa na mumeo mama ni wajibu kuitika**

**Wewe bibi umwitike bwana labeka**

**Umridhie mumeo kwa kila analolitaka**

**Aati aje hapa tuhangaike naye**

**Ati aje hapa**

**Tuhangaike naye**

**Ijapokuwa na mwao sitaki munitukane**

**Nawaita wazazi waje hapa tuonane**

**Wanipe mkaja wangu zipatazo mia nane**

**Niziweke mchangani mwari aje aseme za semi**

**Winue uso nyuma wahisani wakuone**

**Uangaze kila pembe na wabaya uwaone**

**Anapokuja mumeo nyumbani habari muulizane**

**Mpokee mkoba mama kilo ndani ukione**

**Utahadhari na shoga usije wakakunyanganya**

**Sarumberu njiani wengine si wanaume**

**Leo umepata wako mama mahawara nawakome**

**Ati aje hapa tuhangaike naye**

**Tuhangaike naye**

#### **4. HARUSI CHOONI**

**Howa marashi howa**

**Mavumba na udi howa**

**Na mavumba mema howa**

**Yanukayo oto howa**

**Harusi chooni Howa.**

**Ni tumujiyani mwanangu kiyawa tawalipa**

**Tawalipa, tawalipa siwa, tawalipa siwa**

**Kile kikapu cha mbale tawanyiya walezi**

**Tawanyima walezi, walezi wa mwana**

**Huwa mpaji apeleo na mwandi hamwanda**

**Mwandi hamwanda, hamwanda na mwandi hamwandaliza**

**Harusi chooni Howa.**

**Huo wiya wa mwana wa wiya**

**Wiya wa mwana umetenda nganu na mpunga**

**Hai kanga wangu ndokose ye pweke maindoni**

**Mwana kanga ndokose ye pweke maindoni**

**Harusi chooni Howa.**

**Hamlisha limawisha nganu na mpunga**

**Mwana kanga kuku wakwe atambua wenye**

**Nipani kiwanda niteze pole pole mtu mweni**

**Huno utumweni wangu si wenyeji wenu**

**Harusi chooni Howa.**

**Mtumweni yutimbile kisima**

**Kawanwisha wenyejiwe maji**

**Akima kupata maji akapiga panda**

**Aketa wana wa nyema wakija wakima na kulia**

**Ya kushindwa ndio ada ya waume**

**Harusi chooni Howa.**

## **5. NAUPIGA PAPAPA**

**Naupiga papapa**

**Naupiga lololo**

**Naupiga lololo**

**Naupiga papapa**

**Usione mkono umeng'ara**

**Si kazi yangu kazi ya sonara**

**Usione watu kutandika**

**Kutandika kuna maana yake**

**Naupiga papapa**

**Naupiga lololo**

**Ukitaka mumeo asitoke**

**Akilala mguu mpachike**

**Kumea mvi si utu uzima**

**Bora mashine kuwa nzima**

**Kwenda na gogo si utu uzima**

**Bora kijiti kuwa kizima**

**Naupiga papapa**

**Naupiga lololo**

**(iii) PICHA ZA HARUSI ZA JAMII YA WATAVETA**



**Picha 001: Kina Mama Wakisheherekea Kuwasili Kwa Bibi Harusi Nyumbani  
Kwa Bwana Harusi**



**Picha 002: Mtafiti Akihudhuria Sherehe Ya Kumwaga Bibi Harusi Nyumbani Kwao.**



Picha 003: Bibi Harusi Katika Sherehe Ya Kitamaduni Ya Kitaveta.



Picha 004: Mtafiti Akishiriki Katika Sherehe Ya Harusi.




**Picha 005: Maharusi Wakiwa Kanisani**

**(iv) PICHA ZA HARUSI ZA JAMII YA WASWAHILI**



**Picha 001: Goma la Waswahili**



**Picha 002: Bwana na Bi. Harusi Katika Ukumbi wa Kokni (Majengo Stadium) Mombasa. Katika Hafla ya Kupokea Mkono Baada ya Nikaha.**



**Picha 003: Bi. Harusi Katika Ukumbi wa Kokni (Majengo Stadium) Mombasa.**



**Picha 004: Bwana na Bibi Harusi na Jamaa za Bi. Harusi**



**Picha 005: Mtafiti Akiwa na Maharusi Katika Ukumbi wa Kokni (Majengo Stadium) Mombasa.**



**Picha 006: Mtafiti Akiwa na Bwana Harusi Katika Msikiti wa Shibu Mwembe Tayari.**

## v) ORODHA YA MAJINA YA WALIOHOJIWA

### **1. Pili Merenga:**

Ni mkulima na mfugaji wa ng'ombe na huishi Kiwalwa.Ni mwimbaji wa nyimbo za urwasi.

### **2. Raymond Mnene:**

Alikuwa padre wa kanisa la Katoliki.Ni msomi mwenye kumbukizi nyingi kuhusu utamaduni wa Wataveta.Anatoka eneo la Mahoo.

### **3. Julius Jumapili.**

Ni mzaliwawaKiwalwa anayeishi Msheghesheni.Ni mshauri katika maswala ya taratibu za maswala ya ndoa.

### **4. Leah Nyangandu:**

Ni mama mkulima na mshauri kuhusu masuala ya miiko na ndoa ya Wataveta.

### **5. Leah Baraza:**

Ni mzaliwa wa Mereeni lakini anaishi Kidong'u.Ni mshauri katika masuala ya ndoa katika jamii ya Wataveta.

### **6. Makange Ledemi..**

Ni mkulima na mfugaji wa mifugo na nyuki na anaishi Kiwalwa.Alishiriki katika masuala ya ulipaji mahari.

### **7. Sauda Ali.**

Ni mzaliwa wa Mkanyageni (Mji wa kale).Ni mshauri wa masuala ya utamaduni na ndoa katika jamii ya Waswahili.

### **8. Abdalla Mmbwana.**

Ni mzaliwa wa Mkanyageni (Mji wa Kale).Alifanya kazi na shirika la utangazaji la Kenya (VOK).Ni mshauri wa mambo ya ndoa na utamaduni.

### **9. Amira Musellem Said.**

Ni mzaliwa wa Bahani (Mji wa Kale).Ni mwimbaji,mtafiti wa masuala ya wanawake na mwandishi wa vitabu.

### **10. Ahmed Slim Khalili.**

Ni mzaliwa wa Mkanyageni (Mji wa Kale).AmehamiaTaveta na anaishi Mahoo.Ni mwalimu mstaifu.

### **11. Leila Ahmed**

Ni mzaliwa wa Mkanyageni (Mji wa Kale).Anaishi Taveta-Mahoo.Ni mshauri wa masuala ya ndoa.